ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne – Tarehe 20 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi sheria Nam. 2 ya 2006. Naomba kuwasilisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ame Haji Ali: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati wa Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Chakula ba Vipodozi Sheria Nam.2 ya 2006. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Nam. 76

Upandishaji vyeo Idara Maalum

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kusimamia Utawala Bora kupitia Idara Maalum za SMZ, kwa kusimamia Vikosi vyake kwa ufanisi na kwa taaluma za kisasa katika kazi zake ambapo kuna wapiganaji waadilifu na wenye kujitolea kwa ujuzi na kwa imani ya nchi.

(a) Je, Serikali inawapandisha vyeo au kuwapa mafunzo wapiganaji kila baada ya miaka mingapi.
(b) Je, kuna utaratibu gani wa kupata tunzo au kupandishwa vyeo wapiganaji wanaojitolea kufanya kazi zaidi zisizo za kawaida.
(c) Je, Serikali inawapa adhabu gani wapiganaji wasio waadilifu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu Mhe. Suleiman Sarahan SaidMwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake Nam. 76 lenye vifungu (a), (b), na (c) lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Moh'd Shein ambaye ndie Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ kwa hatua mbali mbali anazozichukua za kuwaendeleza Maofisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ.

Idara Maalum za SMZ zimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 121(1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambapo majukumu makubwa ya Idara hizi ni kudumisha ulinzi na usalama wa wananchi wa Zanzibar na mali zao.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Idara hizi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbali mbali ili kuboresha maslahi kwa lengo la kuleta utendaji wenye tija. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa vifaa mbali mbali ili kurahisisha utendaji.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 76 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali imeandaa utaratibu maalum wa kuwapa motisha watumishi wa Idara Maalum ikiwa ni pamoja na kuwapandisha vyeo na kuwapa mafunzo mbali mbali ili kuwajenga na kuwaendeleza kwa makusudi ya kutoa tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Malengo maalumu ya kuwapa mafunzo wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ ni:-

(a) Kuendeleza ujuzi na ubora;
(b) Kukuza vipaji na utendaji wa uongozi;
(c) Kuhakikisha wapiganaji wetu wanaenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na teknolojia.

Aidha, wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ hupandishwa vyeo katika kufanikisha malengo yafuatayo:-

(a) Kuwapa motisha;
(b) Kujaza nafasi za kiuongozi zilizowachwa wazi kutokana na muundo wa Idara husika.

Hivyo, suala la kuwapandisha vyeo au kuwapa mafunzo wapiganaji wa Idara Maalum ni suala endelevu na halina muda maalum isipokuwa kila Idara Maalum imepanga utaratibu wake wa kuwapeleka masomoni Maofisa na Wapiganaji wake. Suala la kuwapandisha vyeo au kuwapeleka masomoni wapiganaji linategemea mambo mbali mbali kama vile:-

- Upatikanaji wa fedha
- Mahitaji ya Idara Maalum; na
- Kutekeleza matakwa ya Kanuni za Idara Maalum za SMZ.

(b) Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa kutoa tunzo na kuwapandishwa vyeo wapiganaji wanaojitolea kufanya kazi zaidi zisizo za kawaida unatumika kwa lengo la kuwapa motisha watumishi wa Idara Maalum ambao hupewa motisha ili kuongeza moyo na ari ya uwajibikaji na kuwa kigezo kwa watumishi wengine. Endapo mpiganaji atapewa motisha atatekeleza kazi yake kwa moyo mmoja na kuona kuwa amethaminiwa na Wakuu wake kutokana na mchango wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Idara Maalum za SMZ, utaratibu huu upo Kisheria na umeelezwa vizuri katika kifungu cha 5(4) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya 2008 kinachoelezea kuwa Waziri atakuwa na uwezo wa kutoa mapendekezo ya kuwapandisha cheo Askari wa Idara Maalum kama tunzo maalum ya ujasiri, kujitolea au kutokana na matokeo maalum. Aidha, Mkuu wa Idara Maalum ana uwezo wa kumpandisha cheo Askari kutoka cheo cha Koplo hadi "*Warrant Officer"* baada ya kupata mapendekezo ya Kamati Tendaji ya Idara Maalum husika.

(c) Mhe. Naibu Spika, kama zilivyo Taasisi nyengine katika Utumishi wa Umma, Idara Maalum za SMZ zinafuata misingi ya Utawala Bora. Miongoni mwa misingi hiyo ni kuhakikisha kila mpiganaji anafuata Sheria na Kanuni zilizowekwa na endapo mpiganaji huyo atavunja maadili ya kazi, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Zipo

Sheria zinazotumika katika kushughulikia makosa ya kinidhamu kwa wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ.

Kwa mfano Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum Nam. 6 ya 2007 pamoja na Kanuni zake za 2008. Aidha, kila Idara Maalum imeundwa na Sheria yake inayoeleza utaratibu wa kuendesha masuala hayo ya kinidhamu. Endapo Mpiganaji atathibitika kufanya makosa atachukuliwa hatua mbali mbali za kama vile:-

(a) Kupewa onyo
(b) Kupewa onyo la maandishi
(c) Kukatishwa mkataba wa kazi
(d) Kupunguzwa mshahara
(e) Kushushwa cheo
(f) Kuachishwa kazi
(g) Kufukuzwa kazi

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali na nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwamba vikosi vyetu naweza kusema kwamba mara nyingi tunatumia zaidi kupunguza au kuwa walinzi sana katika maeneo yetu ya ndani hasa kwa raia wetu wa ndani. Sasa si vyema sana kuwa tunajifunza mafunzo sana ya silaha zaidi kuliko mikono.

(a) Je, anacho kikosi cha Komando kile kinachotumia mikono.

(b) Kama hanacho je, ni lini atatumia kikosi kile ili kikiingia kwenye mji watu wapoe hawana silaha lakini fujo watalituliza. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu fasaha kabisa ambayo ameyatoa. Nataka nimuhakikishie Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba ndani ya Idara Maalum tunavyo Vikosi kama hivyo vingi tu ambavyo vinaweza vikakabiliana na tatizo lolote pale haja inapotokezea kufanya hivyo.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali dogo la nyongeza, naomba kwa heshima yako kubwa uniruhusu kutoa pongezi za dhati kwa Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa Diwani Ndagoni. Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo kwa Diwani

mteule wa Chama cha Mapinduzi naomba sasa kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa suala la kuwapandisha vyeo limekuwa lina manun'guniko katika vikosi vyetu mbali mbali kwa muda mrefu na sio Vikosi vya SMZ hata Vikosi vya Tanzania JWTZ na Polisi na kwa kuwa katika manun'guniko hayo yalikuwa yanapelekea kuonekana kwamba watu wanapelekwa kozi za kupandishwa vyeo kwa ubinafsi, udugu, rushwa nyengine zilizokuwa hazistahiki na kwa kuwa wenzetu wa JWTZ wameanzisha mfumo maalum wa kupeleka kozi za kupanda vyeo kutokana na muda wa kuingia katika Jeshi yaani wanapeleka *intake* kwamba wameingia mwaka 1086 basi unakwenda mwaka 1987.

Je, utaratibu huu wa kwenda kozi za lazima kutokana na muda maalum wa kuingia katika ajira ya Jeshi ni lini Vikosi vya SMZ vitaanza kufuata utaratibu huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, tukianza na maelezo kwamba kuwepo na manun'guniko na vile vile kupandishwa vyeo kwa ubinafsi katika vikosi vyetu naomba nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba ni kweli inawezekana manun'guniko hayo yapo na yanaweza kuendelea kuwepo kwa kadiri siku zinatakavyokuwa zikisonga kutokana na kwamba tabia ya wapiganaji wetu miongoni mwao wanapenda kupata fursa, lakini wakati mwengine kama tulivyoeleza kwamba kuna sheria mbali mbali ambazo zinatumika ambazo zinamfanya mtu aweze kupata hiyo fursa ya kupandishwa cheo.

Nadhani tumesema kwamba kila kikosi kina utaratibu wake nadhani suala hili ni ile *interest* tu kwamba kila mtu anataka aweko juu hata kama vigezo na masharti hajavifikia. Sasa niombe tu Mheshimiwa Mwakilishi tuendelee kuwa wadau katika kuwasaidia vijana wetu katika kuelimisha katika suala hili na taasisi zenyewe zitakuwa zikichukuwa juhudi ya kuona kwamba tunaleta ufafanuzi ili na wao waweze kutambua na warudi kwenye mstari ambao wa kiutumishi kwa mujibu wa kazi zao

Lakini vile suala la hatua na ulazima wa kuwapeleka kozi askari wetu katika utaratibu unaotumika kama katika upande wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Mimi niseme tu kwamba taratibu mbali mbali kama vile za kijeshi au Jeshi jengine ndani ya Jeshi letu ni kwamba taratibu hizo pia zinafanywa. Lakini kwa zile ambazo kwa kweli kuna baadhi ya mambo tukafanana moja kwa moja.

Lakini tutachukuwa kama kuna mambo ambayo yanahitaji kuboreshwa zaidi tuone kwamba na sisi tunaenda ili tuone kwamba kuna lile lengo la serikali na ile dhana ya ulinzi iweze kufikiwa kwa mujibu wa taratibu za kijeshi kama vile sehemu nyengine. Dhamira ni ulinzi kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa majibu ya nyongeza baada ya majibu mazuri sana ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu waziri wangu.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuongezea ni kwamba katika utaratibu wa vikosi vyote duniani vyeo vinatolewa kulingana na muundo na ukubwa wa vikosi vyenyewe na mahitaji ya vikosi vyenyewe kila cheo kina idadi maalum ya uongozi kuwaongoza askari. Kwa hivyo, huwezi kutoa cheo kwa mfano cha Koplo katika askari ambao wanaongozwa na koplo. Lazima idadi hiyo iwepo ya askari, kwa hivyo, vyeo vinategemea pia na ukubwa wa kikosi, ukubwa wa jeshi na mahitaji yaliopo na kila cheo kinahitaji kusomewa hata kama sheria zetu zinatambua kwa mfano kama Waziri anaweza akatoa tunzo Rais akatoa tunzo kama tunzo hiyo itakuwa ni cheo basi cheo hicho lazima kikasomewe na cheo hicho kinaposomewa lazima ile nafasi ya kuwepo hicho cheo iwepo na sio kupandisha vyeo tu kwa sababu ya kuangalia namna ya askari walivyo. Unapandisha vyeo kulingana na mahitaji ya uongozi ndani ya kikosi husika. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali yetu kwa jitihada kubwa ambazo zinaendeleza askari wetu wa Vikosi vyetu vya SMZ kwa kuhakikisha kwamba vikosi vyetu vinakuwa imara na kufanya kazi zao kwa ufanisi, hasa tukizingatia kwamba sare zao zinakubalika. Lakini pia vipando vya magari hili ni suala kubwa ambalo wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa naipongeza serikali. Kuwa na vifaa ni sehemu moja lakini kuvitunza ni sehemu ya pili.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinakuwa salama ili vitumike kwa muda mrefu.

(b) Kuna tuhuma baadhi ya maaskari, maafisa wetu na wapiganaji wanajihusisha na mambo ya siasa na kuleta adha katika upembuzi wa kutafuta watu kupandishwa vyeo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu kuanzia hili la mwisho, kuhusiana na watendaji wetu au watumishi wetu katika Vikosi vyetu vya Idara Maalum kwamba labda kuwa na tuhuma za kushiriki kwenye masuala ya siasa.

Naomba nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kwanza taarifa hiyo inawezekana kama ipo ama inawezekana kama vile ambavyo tumesema kwamba ni tuhuma. Lakini tu kiufupi ni kwamba tuna muongozo wa sheria ambao tukiangalia katika Katiba ya mwaka 1984 ya Zanzibar, kifungu cha 121;

Kifungu cha 121 cha Katiba

"Mtu yeyote ambaye ni mtumishi katika Idara Maalum", Kwa hivyo, hatakiwi kujishughulisha na masuala ya kisiasa, na badala yake yeye anachoruhusiwa ni fursa ya kwenda kushiriki katika kupiga kura, hakuna jengine kati ya hilo. Kwa hivyo, naomba hilo Mhe. Mwakilishi ufahamu hilo na kama wapo ni vyema ukatusaidia tukaweza kuwabaini na hatua kali zinaweza zikachukuliwa au zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria au na miongozo tuliyokuwanayo. *(Makofi)*

Lakini suala la kuwa na vifaa na kuvitunza, pia ni suala jengine. Mkakati katika idara zetu ni kwamba uko madhubuti na vifaa vinakuwa vinahifadhiwa kwa mujibu wa taratibu, ila kuhusu baadhi ya wakati inawezekana pengine hatujafikia kiwango kile ambacho pengine kingekuwa kikubwa zaidi kama vile nchi nyengine, lakini ukweli ni kwamba vifaa vyetu viko salama na vinatunzwa vizuri. Endapo tutapata taarifa ya kwamba kuna *misused* kwenye vifaa vyetu, basi hatua kama ambavyo tumeweza kueleza katika majibu mengine, basi zitachukuliwa kwa mujibu wa muundo wa kiaskari au kiutumishi. Ahsante.

Nam. 47

Usumbufu Kwa Wawekezaji Kupata Vibali Vya Kuwekeza

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza nchini hasa kuhusu usumbufu wa kupata vibali mbali mbali ili kuwekeza nchini hali inayochochea kukwama kwa baadhi ya miradi ya uwekezaji.

a) Je, hatua zipi zinachukuliwa kuondoa hali hiyo.

b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na kituo kimoja cha kutoa vibali (*One stop center*) kama zilivyo nchi nyengine duniani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali nambari 47 la Mhe. Abadalla Maulid Diwani Mwajilishi wa Jimbo la Jang'ombe, naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uwekezaji una mahitaji mengi ambayo yanahusisha maamuzi ya taasisi nyingi, zinazosimamia sheria tofauti. Miongoni mambo yanayohitaji maamuzi tofauti ni mikataba ya ardhi, vibali vya ujenzi, leseni za biashara kutegemeana na aina ya uwekezaji, kibali cha ukaazi na kibali cha kufanya kazi kwa raia wa kigeni, lakini vile vile maombi ya huduma mbali mbali kutoka taasisi tofauti kama vile umeme, maji na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Abadalla Maulid Diwani lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kwa kuelewa umuhimu wa kuratibu masuala muhimu ya utoaji wa vibali vya uwekezaji, serikali ilizitaka Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi na wizara inayosimamia ardhi kuweka maofisa wake katika Ofisi za *ZIPA*, kwa lengo la kuharakisha upatikanaji vibali vya uwekezaji nchini. Nikiri kwamba pamoja na hatua hiyo yenye dhamira nzuri, bado kumeendelea kuwepo changamoto kwa *ZIPA*, kutoweza kufanyakazi kama kituo kimoja cha kufanikisha miradi *(One Stop Centre).*

b) Katika kufanikisha azma hiyo ya serikali ya kuwa na kituo kimoja cha ufanikishaji miradi *One Stop Centre.* Hivi sasa Kamati ya Wataalamu kutoka taasisi zote husika imeundwa, na ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti yake. Mapendekezo ya Kamati hiyo ya Wataalamu yatasaidia katika kuifanya *ZIPA* kuwa kituo kimoja cha ufanikishaji miradi *One Stop Centre* kwa kuzingatia sheria ziliopo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri yasiyokuwa na ukakasi katika hili, kama kwamba imekuwa ni nyimbo ya muda ambayo inakosa msikilizaji kwa kufunguliwa kituo cha *One Stop Centre* hapa Zanzibar.

a) Je, lini serikali hii itatoa maelekezo kwamba baada ya miezi miwili, mitatu au sita kwamba kituo kile kinafunguliwa ili kuwaondoshea matatizo wawekezaji wetu.

b) Vile vile kumekuwa kuna malalamiko kwa wawekezaji hawa juu ya kadhia nzima ya kulipishwa kodi za mapatano, *negotiation* kodi. Mtu anakwenda, kuna wageni wangapi vyumbani anapatana, andika watatu wawili nipe mimi.

   Je, wizara yako ina mikakati gani ya kuondoa changamoto hiyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza kama nilivyosema kwamba kamati hii imeundwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Kamati inafanyakazi zake, na hivi karibuni kama nilivyokwishakueleza itawasilisha vipoti yake. Ripoti ya awali imeshakamika kuna mambo ambayo yanawekwa sawa. Kwa hivyo, Mhe. Abdalla Diwani namuomba astahamili sio muda mrefu sana ripoti hiyo itapatikana.

Jambo la pili kuhusiana na kodi ya mapatano. Sina hakika kwa sababu ndani ya sheria sijaiona kodi ya mapatano, lakini ninachojua kwamba zipo kodi za hoteli ndogo ndogo, ambazo zinalipa *hotel levy*, na ndani ya sheria ya *hotel levy Act* kifungu kidogo cha (3) kinampa mamlaka waziri, kwa kushauriana na Kamishna wa Mapato, kuweka kodi maalum kwa maana ya *fixed rate*, lakini sio ya mapatano, ni *fixed rate* kwa kutegemeana na kazi anayoifanya au biashara inayofanywa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kama itawezekana hayo maswali mawili ya nyongeza nipewe mimi yote mawili, naomba niulize maswali mawili badala ya moja (a) na (b).

Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri aliyotoa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na pia nimpongeze kwa maelezo mazuri. Lakini napenda nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu viwili.

a) Kwa kuwa hii *ZIPA*, yaani *Zanzibar Investment Promotion Agency*, ni taasisi ambayo iliwekwa kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani na wa nje, lakini pia kuwaunganisha kwa mahitaji mengi waliokuwa wanahitaji. Kwa miaka nenda miaka rudi hii taasisi kwa kweli malengo ambayo yalikuwa yamewekewa, yameshindwa kufikia na hata wawekezaji ambao tuseme hao ni *Foreign Direct Investors (FDI)*

kutoka nje, wamepoteza matumaini katika hii taasisi na wamelalamikiwa mara nyingi.

Sasa labda nimuulize Mhe. Waziri, je ni lini atapiga fagio la chuma na kutumbua majipu ambayo yamekuwa kero kwa wawekezaji wa ndani na wa nje, na kuwacha kutuletea maneno mengi mengi hapa na majibu mazuri madogo madogo. Lakini aende akasafishe na kuweka mambo sawa, ambapo Rais wetu aliwaahidi wananchi pamoja na wawekezaji.

b) Wawekezaji wa ndani na wa nje hupata fursa ya kuonana kwa pamoja katika Baraza la Biashara. Lakini Baraza hili halijakutana muda mrefu na makero yamekuwa ni mengi. Lakini hata hivyo Rais wetu wa Zanzibar katika mazingira ya kujenga *spirit* ya umoja *Public Private Partnership*, ni lini Mhe. Waziri atawaalika japo wawekezaji kunywa chai pamoja na Mhe. Rais, ili kuonesha umoja wa hiyo *spirit* ya *Public Private Partnership*. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme siamini kama kuna tatizo hilo la uwekezaji nchini, na kama lipo basi ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi akatueleza kwamba ni wawekezaji gani ambao wameshindwa kupata vibali, au wamekuwa na vikwazo mbali mbali. Lakini hiyo ilinganishwe na wale wawekezaji ambao wamepata vibali na wanaendesha shughuli zao bila ya vikwazo vyovyote. Takwimu hiyo ingetusaidia tungeweza kuelewa.

Pia niseme kwamba mimi ofisi yangu bado sijapata malalamiko hayo. Hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na kikao na wawekezaji pale Maruhubi, ni karibu mwezi mmoja uliopita na tulikuwa na majadiliano mazuri. Hawakuwa wakionesha malalamiko ya maana ya kwamba *ZIPA*, lakini walikuwa wakionesha malalamiko ya kuwekwa ada, nakusudia kusema kuweka kodi vizuri. Hilo ndio lilikuwa lalamiko lao kubwa, na hilo tuliahidiana nao kwamba tutalifanyia kazi.

Vile vile tuliwaahidi kwamba ziko *forum* nyingi, na kabla wakati wa *budget* kunakuwepo na *budget dialogue* ambayo inawashirikisha wafanyabiashara na wawekezaji wote, nayo ni fursa muhimu ya kueleza kasoro zilizopo, changamoto wanazozipata. Nadhani huko ndio pahala ambapo tungezitumia *forum* hizo kuzungumzia changamoto hizo kwa mustakabali wa kupata ufumbuzi wake.

Lakini vile vile niseme kwamba Baraza la Biashara, *Zanzibar Business Council* lipo, Mwenyekiti wake yupo, na huko nyuma limekuwa likikutana na kadiri hali itakavyoruhusu na mahitaji yatakayokuwepo, basi Baraza la Biashara litakutana. Lakini Baraza hilo hilo la Biashara ambalo liliagiza Wizara yetu ya Fedha na Mipango na wizara nyengine, kuhakikisha kwamba tunakuwa na vikao vya mara kwa mara na wafanyabiashara na wawekezaji, ili kuweza kusaidia kutatua changamoto zake.

Kwa hivyo, Mhe. Simai Mohammed asiwe na wasiwasi, hivi sasa serikali iko katika utaratibu wa kuifanyia marekebisho sheria ya kuanzishwa *Zanzibar Business Council*, ili *Business Council* hii iweze kufanyakazi zake vizuri kwa mujibu wa sheria itakayotungwa. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango lenye vifungu (a) na (b)**.**

(a) Kwa kuwa wizara yako ya fedha kwa kupitia *ZRB* inadai fedha nyingi kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka 10, 5, 7 kwenye mahoteli na biashara nyengine kwa kodi ambazo ni za nyuma.

Je, ni lini sasa wewe mwenyewe Mhe. Waziri kwa kupitia taasisi au ofisi yako ya *ZRB*, itahakikisha kwamba wale wote ambao wanadaiwa madeni ya siku nyingi, na mengine ambayo yanasababishwa na watu ambao waliokodi na wakawaingizia madeni wale wamiliki kwa njia ya *penalt*. Kuna *penalt* zinakuwa nyingi na kuna kodi yenyewe ambayo unataka kuipata inakuwepo, ni mambo mawili tofauti.

Sasa ni lini mtakaa kuhakikisha kwamba yale madeni yanalipwa, lakini mkawasamehe zile penalt ambazo zilizosababishwa ama na taasisi yako ya *ZRB*, au na wale watu ambao walokodi nyuma wakasababisha madeni yakawa ya muda mrefu.

(b) Ni lini wizara yako itaweka *fixed rate* katika mahoteli, badala ya watu wako wa *ZRB* kupita kila siku kwenda kuuliza vyumba, kukagua vyumba na kuhoji, na wengine kutaka kufungua vyumba. Ni lini sasa wizara yako itaweka *fixed rate* kulipisha mahoteli ya mjini na mashamba ili kuondosha usumbufu kwa wageni, wenye mahoteli pamoja na wizara yako.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru.

(a) Mhe. Naibu Spika, kuhusu malimbikizo ya madeni. Naamini *ZRB* kwa kufuata sheria imeshawajulisha wote wenye malimbikizo ya madeni kwa maana ya kwamba kuwataka walipe madeni yao. Kwa wale ambao wana malalamiko, naamini walitokea kama wawili au watatu wenye malalamiko, kutokana na malimbikizo ya madeni hayo waliwasilisha malalamiko yao hayo kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Mimi nilichukua juhudi ya kuwaita *ZRB*, tukakaa na hao waliolalamika na tukaweza kuondoa kasoro hiyo na tatizo hilo.

Sasa kama wapo ambao bado na wao wana malalamiko kama hayo, wangefuata taratibu za kisheria. Sio busara kwamba wao walalamikaji tukawa tunawalalamikia ndani ya Baraza hili. Utaratibu upo wa kisheria, mwenye malalamiko awasilishe malalamiko yake tutayasikiliza, na kama tutahisi kwamba kweli hawakufanyiwa haki, basi tutawatafutia haki zao.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu ni lini tutaweka *fixed rate* ili kuondosha usumbufu. Niseme kwamba kodi zote zinazotozwa, zinatozwa kwa mujibu wa sheria ziliopo. Tuna sheria ya *VAT* ya mwaka 1998, ambayo imepitishwa ndani ya Baraza hili.

Vile vile tuna sheria ya *hotel levy* ambayo imepitishwa na Baraza hili. Sheria zote mbili hizo zimeweka utaratibu maalum. Kwa wale wanaotumia *VAT* kuna utaratibu maalum na kuna *threshold* kiwango cha milioni 30. Kwa maana kwamba wale *VAT registered* wanaovuka *sells* zao, *sells over* zao za mwaka milioni 30 na kuna *rate* ambayo wanatoza kwa chumba dola 100, hawa wana utaratibu wao ikiwemo ku-*claim back* ile *input VAT*. Lakini utaratibu wa hizi hoteli ambazo hazifikii kiwango hicho cha milioni 30 na hawatozi *rate* hiyo, nao wana utaratibu wao kwa mujibu wa sheria.

Sasa iwapo tunahisi sheria hizi zina kasoro, basi Baraza hili sasa ni la kupendekeza kutungwa kwa sheria nyengine ambayo itazingatiwa. Lakini kwa sasa taratibu za kisheria zilizopo ndizo zinazotumika katika kuweka viwango, lakini pia katika kuweka utaratibu wa malipo ya kodi mbali mbali za serikali. *(Makofi)*

Nam. 104

Changamoto Katika Vituo Vya Kulea Watoto Yatima

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:-

Kwa kuwa kuna changamoto nyingi zinazovikabili vituo vya kulelea watoto mayatima hapa Zanzibar ikiwa ni pamoja na mazingira yasiyoridhisha ya majengo yanayotumika kama vituo vya kulelea watoto na kadhalika.

(a) Je, Wizara inachangia kiasi gani cha fedha kwa kila mwaka kwa wamiliki wa majengo yanayotumika kulelea watoto mayatima na wenye mazingira magumu.

(b) Je, Wizara ina mpango gani kwa upande wa Pemba kupata majengo yake ili kuondokana na kuwaweka watoto kwenye majengo ambayo hayakidhi kiwango.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye na yeye anaendelea kutupa pumzi zake asubuhi hii tukakutana hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niweze kutoa neno la shukrani kabla ya kujibu swali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wenye majimbo pamoja na wabunge ambao wameweza kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, juu ya suala zima la kuwawezesha wazee wetu kwa kuwaenzi kwa ajili ya kuwapatia bima za afya. Naomba kwa niaba ya wizara nitowe shukrani hizi, na pia niwaombe wale ambao hawajaanza kutekeleza suala hili basi tuombe kwa Mwenyezi Mungu na wao awape nguvu na uwezo ili waweze kutekeleza ili na wao waweze kuwaenzi wazee wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani zangu hizo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Jimbo la Konde swali lake Namba 104 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kutumia Sheria ya Watoto Namba 6 ya mwaka 2011 imempa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii kushughulikia suala la ulinzi na ustawi wa watoto ili kuhakikisha maslahi bora ya watoto yanafikiwa.

Mhe. Spika, hakuna fungu wala kifungu kinachotumika kuchangia kiasi cha fedha kwa kila mwaka kwa wamiliki wa majengo hayo yanayotumika kulelea watoto mayatima na wenye mazingira magumu, isipokuwa kwa kile kituo kimoja tu kinachoendeshwa na Serikali kwa usimamizi wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inathamini sana mchango wa Taasisi na Watu binafsi katika kutoa huduma za kulelea watoto katika vituo hivyo. Wajibu wa Wizara hii kuratibu taratibu za malezi na huduma za kulelea watoto mayatima katika vituo hivyo.

(b) Mhe. Spika, kwa sasa Wizara haina mpango wa kujenga nyumba ya kulelea watoto Pemba kwa sababu nyumba ya Serikali iliyokuwepo Mazizini ina watoto wachache ikilinganishwa na uwezo iliyonayo wa kuhifadhi watoto wengi zaidi. Aidha napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa maamuzi ya kumuweka mtoto katika kituo yanapaswa kuwa ni suluhisho la mwisho ambapo mibadala yote mengine ya kumpa malezi na makuzi ya mtoto husika ndani ya familia yake kushindikana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi niungane nae kwa kumtaja Mwenyezi Mungu, lakini swali langu lenye vifungu (a) na (b) naomba nilinukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

" Wizara ya Uwezeshaji vijana Wanawake na Watoto kwa kutumia Sheria No. 6 ya Mwaka 2011 imempa Mkurugenzi wa Idara ya Wazee kushughulikia suala la ulinzi na Ustawi wa Watoto".

a) Mhe. Naibu Spika, kuna sheria gani inayosema mtoto kulelewa nyumba za wazee akapelekwa Wizarani na baadae hakurudi kuna sheria gani inayosababisha vile na mtoto yule yuko wapi nyumba ya mayatima.

b) Mhe. Naibu Waziri yeye mweyewe shahidi hivi juzi mmefungua kituo Pemba sijui kama kunaitwa Mabaoni au Vitongoji kule, hebu tueleze sababu gani za kufungua kituo kile masafa kutoka Pemba kuja huku ni makubwa na ndugu zetu wa Pemba ni wakarimu wamejitolea kule kwa hali na mali. Hebu toa sababu za msingi wananchi wapate kujua kituo ulichokifunga.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri swali la mwanzo sikuruhusu kujibu kwa sababu halifanani na swali la msingi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku suala hilo……

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Suala la msingi liangalie kwenye hii *Order Paper* limezungumza vipi.

Mhe. Naibu Spika: Nataka suala la pili Mhe. Waziri ujibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mayatima hapa Zanzibar ilivyoandikwa kwenye *Order Paper.*

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, sababu zipi zilizopelekea kukifunga Kituo cha Kulelea watoto cha Mabaoni. Sababu za msingi zilizonipelekea kufunga Kituo kile cha Kulelea Watoto hivi karibuni nilifanya ziara ya kwenda Pemba na kutembelea vituo vile, niliona mimi kama mzazi hali halisi ya mazingira katika kituo kile haifai kabisa kuishi watoto na ndio sababu iliyopelekea kufungwa kwa kituo kile.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali inathamini sana mchango wa taasisi za watu binafsi katika kutoa huduma za kulelea watoto. Je, Mhe. Waziri kuna vituo vingapi vya watu binafsi vya kulelea watoto vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Naomba niungane kwanza na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli Serikali inathamini sana juhudi za watu binafsi katika kulea watoto mayatima na walio

katika mazingira magumu. Vituo tulivyonavyo vya watu binafsi ni 10 ambapo Unguja kuna vituo 7 na Pemba kuna vituo 3.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Wakati wa ufunguzi wa sherehe za mtoto pale Gombani mwaka 2016 Mhe. Waziri alikiri kuwa kuna baadhi ya vituo vya kulelea watoto havina viwango, na alisema kwamba vituo hivyo atavichukulia hatua ikiwemo na baadhi ya vituo hivyo kuvifunga.

a) Je, ni vituo vingapi ambavyo vilichukuliwa hatua ni hatua gani, na vituo vingapi ambavyo vilifungwa.

   Pia katika jibu lako mama ulisema kuwa hakuna haja ya kujenga vituo hivi Pemba.

b) Je. Mhe. Waziri Serikali haioni kuwa kuna mpango wa kusaidia watoto yatima kwa upande wa Pemba ili nao wanufaike na hifadhi hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kidogo arudie suala la mwanzo.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Siku ya sherehe za watoto pale katika Uwanja wa Gombani Mwaka huu 2016 uliopita, alikiri kuwa kuna baadhi ya vituo vya kulelea watoto hawa havina viwango na alisema kwamba vituo hivyo atavichukulia hatua na katika baadhi ya hatua hizo ni kuvifungia vituo hivi. Je, atueleze hadi sasa ni hatua gani ambazo amechukua na je, ni vituo vingapi ambavyo amevifunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Katika jitihada zilizochukuliwa na Mhe. Waziri, moja ni kuvifunga vituo hivyo ambavyo hivi karibuni hata vyombo vya habari vimeripoti kufungwa kwa Kituo cha Mabaoni, na kituo chengine ambacho nilitembelea kikiwa hakiridhishi cha Mabaoni katika ziara yangu niliyotembelea Pemba nimefika mimi mwenyewe na kuona kwamba sasa hivi kituo kile kina sifa na kila aina ya kuweza kuhudumia watoto hawa.

Suala lako la pili ulilosema kwamba Wizara haioni sababu ya kujenga nyumba Pemba kwa ajili ya kuhudumia watoto yatima niseme kwamba nyumba yetu ya kulelea watoto mayatima iliyokuwepo Mazizini inatosheleza kulea watoto hivi sasa kwa Unguja na Pemba, ukiangalia nyumba ile hivi sasa ina idadi ya watoto kidogo na inaweza kubeba watoto wengi yaani watoto 70 hadi 100 kwa sasa na hivi sasa kituo kile kina watoto 26, ambapo bado kina uwezo wa kuweza kuhudumia watoto Unguja na Pemba.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utataribu kanuni ya 63, sijui nina haja ya kuisoma au utakuwa ushaielewa kwa vile wewe ni mzoefu.

Mhe. Naibu Spika: Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muongozo wako Suala la msingi naomba nilinukuu.

"Kwa kuwa kuna changamoto nyingi zinazokabili vituo vya kulelea watoto mayatima hapa Zanzibar".

Ikiwemo cha Mazizini kipo Zanzibar ndio suala langu Mheshimiwa sasa nashangaa unamkinga Mhe. Waziri nataka muongozo wa kiti chako.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri una majibu yoyote kuhusu hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, sitokuwa na jibu jengine la kuweza kumjibu Mhe. Muwakilishi, kwa sababu kama nilivyojibu kwenye suala langu mama kwa sasa Wizara haina mpango wa kujenga nyumba ya kulelea watoto Pemba kwa sababu nyumba yetu iliyokuwepo Mazizini ina sifa za kulea watoto wote na wala nyumba ya Mazizini haina tatizo lolote kama anavyosema Mhe. Mwakilishi.

Nam. 6

Uvamizi wa Maeneo Mbali Mbali ya Ardhi

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-
Mara nyingi tumeona uvamizi wa maeneo mbali mbali ya Mawizara, Ofisi za Serikali, majengo ya afya na mengineo, jambo ambalo halipendezi na linapelekea kupungua maeneo hayo siku hadi siku.

(a) Je ni lini Wizara itajenga uzio katika skuli ya Chwaka Tumbe ya ili kupambana na uvamizi huo.

(b) Je Wizara haioni kuwa kuchelewa kujenga uzio huo kutapelekea watu kusogea na wanyama kufungwa, na mandhari ya skuli kuharibika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa naomba utulivu wenu tusikilizane.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 6 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa hatusikilizani kelele zimezidi tafadhalini Waheshimiwa kelele zimezidi hatusikilizani, hatumsikii Mhe Waziri anavyojibu. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kabla ya kujibu swali hilo naomba nitoe maelezo ya utangulizi.

Ni kweli kwamba migogoro ya uvamizi wa ardhi katika maeneo ya skuli zetu yamekuwa yakijitokeza; pia, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa ujenzi wa uzio unaweza kupunguza uvamizi wa maeneo muhimu yakiwemo skuli na vituo vya afya na Ofisi za taasisi za Serikali. Wizara yangu imeliona hilo na inatoa umuhimu mkubwa katika kuyalinda maeneo ya skuli zetu. Hata hivyo gharama za kuzungusha uzio katika skuli zetu ni kubwa mno kutokana na wingi wa skuli na kwa hivi sasa Wizara haina uwezo wa kutosha wa kuzijengea uzio skuli zetu zote. Ili kuepusha migogoro ya uvamizi wa ardhi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nishati, Maji na Mazingira inaendelea na juhudi ya kuyapima maeneo ya skuli na kuzipatia hatimiliki. Pia, Walimu Wakuu kwa kushirikiana na Kamati zao za Skuli zimetakiwa kuweka uzio kwa kupanda miti kuzunguka eneo lote la Skuli. Baada ya maelezo hayo naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara imeweka kipaumbele ujenzi wa uzio katika Skuli ya Sekondari ya Chwaka Tumbe katika Wilaya ya Micheweni Pemba. Kwa hivi sasa, Wizara haina fedha za kutekeleza ujenzi huo lakini napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Ujenzi wa Uzio utafanyika, hali ya kifedha itakaporuhusu. Pia, napenda kutoa wito kwa wananchi kuendelea kuyalinda maeneo ya skuli zao na wasikubali watu wachache kuyavamia maeneo hayo.

(b) Ni kweli kuchelewa kujenga uzio kunaweza kupelekea watu wachache kuyavamia maeneo ya skuli ama kwa ujenzi holela au ufungaji wa wanyama. Kama nilivyotangulia kusema Wizara inawaomba wananchi waendelee na juhudi ya kuyalinda na kuyadhibiti maeneo ya skuli kwa kuwaelimisha wananchi kupitia kamati za skuli na uongozi wa skuli. Wizara itaendelea na taratibu za kuwachukulia hatua kali za kisheria watu watakaovamia maeneo ya skuli zetu kwa kisingizio chochote.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza suala moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri, Skuli ya Sekondari ya Chwaka Tumbe, Pandani na Konde zilijengwa kwa madhumuni ya shughuli hizi kuchukua wanafunzi maalum wa vipawa kwa ajili ya kufundishia pale au kupata elimu, lakini tumeona baadhi ya skuli nyengine kukosa mabweni na kupelekea wanafunzi wale kukosa sehemu ya kukaa ili kupata elimu ile.

Je, ni lini sasa Wizara yako itajenga mabweni katika skuli zile ambazo tokea hapo mwanzo ilikuwa ni adhima ya Serikali kujenga mabweni hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli adhma ya Serikali ni kuzijengea mabweni Skuli hizi, lakini kutokana na uchache wa fedha imekuwa ni vigumu lakini hata hivyo niseme kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itawajengea mabweni hayo wakati hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, na mimi napenda nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kuna mgogoro katika skuli ya Kiwengwa Cairo kwa muda mrefu kuna muwekezaji amechukua eneo hili, Je, ni lini mgogoro huo utaisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli mgogoro huo upo na hivi sasa tunakusudia kukutana Wizara tatu kuweza kuupatia suluhisho mgogoro huu ikiwemo Wizara ya Elimu, Wizara inayoshughulikia Ardhi pamoja na Uwakilishi wa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa hivyo hapo

tutakapokutana tukalijadili na kutafakati nadhani suala la mgogoro huo litapatiwa suluhisho.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba uvamizi wa maeneo ya skuli upo lakini Skuli ya Ndagoni hadi sasa mipaka yake bado haijajulikana kutokana na sitofahamu ya wale waliotoa eneo kutokulipwa fidia yao.

Je, ni lini wananchi wale wahisani wale waliotoa eneo lile watapatiwa fidia yao ili Skuli ya Ndagoni kupatiwa mipaka yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Suala la Skuli ya Ndagoni limepimwa na *site plan* Wizara tunayo. Pili mgogoro wa warithi au wanaodai kumiliki eneo lile sisi Wizara baada ya kuona kwamba vielelezo vya warithi haviridhishi, na narejea tena wanaodai eneo lile waraka waliokuja nao Wizarani unasema kwamba wanadai eneo la Ndagoni lakini wakara eneo la Shungi, kwa hivyo tukahisi hapa pana kitu hakifahamiki na kwa maana hiyo Wizara haikukaa kimya hivi sasa imeunda kamati ya kuchunguza suala hili na baadae taarifa zake zitaletwa Wizarani na litazungumzwa katika kamati ya uongozi wa Wizara.

Muongozo

Mhe. Suleiman Makame Ali: Kanuni ya 37 Waziri au Mjumbe yoyote aliyeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, namuomba Mhe. Naibu Waziri kwamba Skuli ya Ndagoni sawa lakini wakfu wamethibitisha barua yao hii hapa kwamba lile eneo ni lao, na pia vile vile kwamba lile eneo halijapimwa dokezo hili limetoka Ofisini kwako kwa Katibu Mkuu ni kwamba eneo lile bado lisiachwe kupimwa mpaka itakapokamilika. Sasa nataka kujua kwamba wakfu ni *HO* katika serikali hii kwa sababu wakfu wao wamethibitisha na barua hii hapa ninayo. Lakini pia vile vile pia nataka nikukabidhi hizi ili tukae kwa pamoja tuzione mimi na wewe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Waziri majibu lakini pia anasemea anataka kukukabidhi karatasi zile kwa sababu kuna malalamiko na barua ipo. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa anataka umjibu sahihi.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kutokana na mkanganyiko wa hizo nyaraka tunazo nyaraka mbali mbali, tunazo ambazo ziko katika *file* la Wizara ya Elimu ambao ni waraka rasmi umetafsiriwa katika Ofisi rasmi ya kutafsiri inaeleza kama nilivyoeleza na *site plan* ipo na maombi mengine yote yapo ndio nikasema sasa ili kupata jawabu sahihi wizara imeunda kamati kujiridhisha na hizi nyaraka zilizopo asubiri matokeo ya utafiti wenyewe na taarifa tutatoa. Akisema nyaraka na sisi tunazo na zetu ni halali zaidi kuliko alizonazo yeye. (*Makofi*)

Nam. 16

Serikali Kuanzisha Mabasi ya Mwendokasi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Mji wa Zanzibar umeanza kuwa na ongezeko kubwa la magari.

(a) Je, Serikali imeanza kuchukua hatua gani ya kuwa na Mradi wa mabasi ya mwendo kasi kwa kutenga njia maalum katika siku za baadae ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayohitajika.

(b) Kwa kuwa huduma nyingi za kijamii ziko katikati ya Mji wa Zanzibar Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo la msongamano wa magari ambao umeshaanza kuathiri baadhi ya maeneo na kusababisha watu kuchukua muda mwingi wa kuingia na kutoka mjini.

(c) Serikali ina mpango gani wa kutengeneza njia mbili kwa barabara ya Bububu ambayo ni nyembamba pamoja na barabara kuu ya kuingia na kutoka mjini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake Nambari 16 ambalo lina vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali tayari inayo mawazo ya kuwa na usafiri wa umma ambao ni bora zaidi utakaohudumia wananchi wengi hasa wanafunzi na wazee. Hivi sasa tumejipanga kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi

yakinifu *Feasibility Study* ili kupata kujua njia bora itakayotumika kuboresha usafiri wa umma yaani *Public Transport*

(b) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Manispaa ya Mji wa Zanzibar ina mpango wa kutafuta njia bora zaidi ya kuondosha kabisa tatizo la msongamano wa magari ambao umeanza kujitokeza kwenye baadhi ya maeneo ya Mji wa Zanzibar hasa wakati wa kwenda na kutoka kazini na wakati wa kufika na kuondoka kwa vyombo vya majini katika eneo la Bandari ya Malindi.

(c) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali ina mpango wa kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za hapa mjini na tayari kazi hiyo imeshafanywa katika barabara za Fuoni – Kidongochekundu, pamoja na barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni ambapo barabara hizi zimejengwa njia mbili kwa fedha za Mfuko wa Barabara na kwa sasa barabara hizo zinapitika vizuri kabisa na wao ni mashahidi. Barabara ya Bububu nayo itafanyiwa matengenezo makubwa mara tu fedha zitakapopatikana. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika kwanza niendelee kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu swali la msingi umejibu vizuri sana Mhe. Naibu Waziri nikupongeze kwa hili "mnyonge mnyongeni haki yake mpeni." Naomba kuuliza swali lenye vifungu (a) na (b)

(a) Uchambuzi yakinifu utachukuwa muda gani kukamilika ili utekelezaji wake uanze na wananchi wapate matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(b) Barabara ya Malindi wakati mwengine hufungwa lakini kuna baadhi ya magari mahasusi huwa yanapita kutumia barabara ile na Katiba ya Zanzibar inasema binaadamu wote ni sawa mbele ya sheria. Lakini vile vile umeona wapi Bandari kuwa karibu na barabara hamuoni msongomano na mkafanya maarifa kwenda kutanua Bandari zaidi kule kwenye sehemu za majahazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

(a) Mhe. Naibu Spika, nataka kumuhakikishia kwamba sisi tutahakikisha huu uchambuzi yakinifu tunautayarisha kwa haraka zaidi ili kama anavyosema hayo matatizo ambayo yamejitokeza hasa huu msongamano wa magari unaondoka na vile vile kunakuwepo na usafiri wa umma kwa ajili ya kuwasaidia zaidi wanafunzi na wazee.

Kuhusu hili suala la pili tumelichukuwa na tutalifanyia kazi Mhe. Naibu Spika. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, naomba kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukishuhudia msongamano mkubwa wa magari ya abiria umaarufu daladala pale Afisi Kuu ya CCM.

Je, lini serikali itajenga kituo cha gari za abiria daladala pale Kijangwani ambapo tayari pameshavunjwa, lini ujenzi utaanza?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa serikali inatambua kwamba zile gari ambazo ziko pale ni kero kwa wapita kwa miguu na wanafunzi na hata wananchi wa kawaida. Lakini akumbuke kwamba mipango yote inapangwa na vile vile kuna hatua zimeshaanza kuchukuliwa. Ni karibuni tu tumeshaanza kusafisha eneo la Kijangwani pale kwa ajili ya baadae kuwa kituo cha usafiri wa daladala.

Kwa hivyo, tunamuomba asubiri wakati tunahakikisha kwamba ule usumbufu pale tutauondosha. Ni jambo ambalo limewekewa mikakati na mimi niipongeze sana Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kuchukuwa hatua kutaka kuhakikisha kwamba ile kero inaondoka kwa kushirikiana na wizara yetu na vile vile Wizara ya Ardhi.

Kwa hivyo, mimi napenda kumwambia kwamba atustahamilie na karibuni tu hizo hatua zitachukuliwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Utaratibu

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni lini ujenzi wa kituo cha daladala utaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba ujenzi utaanza pale ambapo fedha zitapatikana kwa ajili ya ujenzi huo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa katika maeneo ambayo yanatumika sana magari kuja mjini maeneo ya

Mji Mkongwe. Lakini maeneo ya Mji Mkongwe ni eneo ambalo linapata *pressure* tano.

- Ni eneo ambalo wawekezaji wanafanya shughuli zao.
- Wazanzibari wanaishi
- Wananchi pia hufata huduma mbali mbali zikiwemo Hospitali pamoja na mabeki.
- Pia ni eneo ambalo lina taasisi na Wizara za Serikali.

(a) Ni lini Serikali itaondoa Idara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Ardhi kupeleka maeneo mengine kwa sababu Wazanzibari wengi wamekuwa wanaingia na magari kufuata huduma hii na kukosa maeneo ya kuegesha magari na tunajua kwamba wizara hii inabeba maji, inabeba ardhi na pia inabeba masuala ya umeme. Kwa hivyo, kero nyingi za wananchi zinakuja hapa na kusababisha vurumai kubwa. Je, serikali haina mpango kuondoa Idara yake pamoja na Wizara katika kuihamisha nje ya maeneo ya mjini.

(b) Tumeona pia katika mwaka 2006 aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano Mhe. Adam Mwakanjuki alifanya mkutano katika eneo la Hoteli ya Bwawani na kuangaliauwezekano wa Serikali kuhamisha wizara zake pia nje ya mji. Lakini pia yalitoka mawazo kutumia iliyokuwa hoteli ya Bwawani kuzigeuza japo wizara sita kuzihamisha pale ambazo uingiliaji wake utakuwa kwa eneo la Malindi na kutoka Gulioni. Sasa kwa kweli jengo sasa hivi limegeuka kuwa Gofu Wazanzibari hawaelewi ni lini litakwenda. Je, serikali haioni umuhimu wa kulitumia hili eneo sasa kuzipeleka serikali zao ili kupunguza magari na kero ambazo wananchi wanazipata katika huduma mbali mbali hasa hili jengo la Hoteli za Bwawani sasa limekuwa linatuzomea linazidi kuwa sasa kichaka na wengine wanaanza kuogopa kwamba sasa litakuwa limejaa mashetani mle ndani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nataka kumwambia kwamba uwepo wa wizara yoyote katika maeneo ya Mji Mkongwe ni wao wanaoamua na vile vile nataka kumwambia kwamba si idara zote zinakuwepo pale idara zimegawika sehemu tafauti na kama Wizara ya Ardhi itakuwa na mpango wa kutaka kuhamia maeneo mengine basi huo ni uamuzi wa Wizara ya Ardhi. Lakini sisi tunalozungumza zaidi ni msongamano uliopo ndani ya Mji Mkongwe.

Sisi tumejipanga na baadae tutakuja na hatua muafaka baada ya kupata ruhusa serikalini ili kuhakikisha ule msongamano unaondoshwa na moja wapo ya mapendekezo yetu ni kuhakikisha kwamba gari zinaingia kwa vibali maalum na vile vile tunaweza kutoza japo aina fulani hivi kwa ajili ya zile gari wanazo-park kule Mji Mkongwe kwa sababu nazo hizo zinasababisha msongamano wa magari.

Kuhusu jengo la Bwawani sote tunajua kwamba lipo katika hatua za ujenzi na kama kutatokea tatizo lolote basi wao wajenzi ndio watatuarifu. Kwa hiyo, mimi siwezi kusema kwamba kuna vichaka vya wahalifu au vya uchafu kule Bwawani kwa sababu serikali ina muundo mzuri na Tawala za Mikoa wanahakikisha kwamba pamoja na kutumia polisi, ulinzi wa wananchi na vile vile unafanyika kila wakati kwa kupitia doria na kuondosha kichaka chochote kile cha wahalifu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 18

Uimarishaji wa huduma za Usafiri wa Baharini

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Nchi ya Zanzibar imezungukwa na bahari na wananchi wake wanatumia usafiri wa anga na wa baharini ambapo biashara ya kutoa huduma za usafiri wa baharini inaendeshwa na wafanyabiashara binafsi kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, Serikali haioni kuwa suala la usafiri kwa wananchi wake si suala la kuwaaachia wafanyabiashara peke yao kutokana na umuhimu wa suala hili.
(b) Je, Serikali imejipanga vipi kununua boti kubwa za abiria na zinazokwenda kasi inayoendana na wakati ili kumudu ushindani wa kibiashara katika sekta hii ya usafiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake Nambari 18 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kuzingatia maslahi ya Wananchi wake ikiwemo usalama wa maisha yao na unafuu wa huduma za usafiri,

pamoja na Sekta hii kuhusisha Sekta binafsi kwa kiasi kikubwa serikali bado inashiriki kikamilifu katika huduma za Usafirishaji hususan kwa njia ya bahari na ndio sababu Kuu iliyopelekea kununua meli mpya na ya Kisasa MV. Mapinduzi II ndani ya mwaka 2015 - 2016.

Aidha katika mwaka 2017 - 2018 serikali inategemea kukamilisha utaratibu wa ujenzi wa meli nyengine mpya ya abiria na mizigo kwa lengo hilo hilo la kusimamia sekta hii ya usafirishaji.

(b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (a), serikali katika kuhamasisha Shirika lake la Meli hivi sasa inakamilisha taratibu za ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo, ambapo pamoja na Meli hiyo kuwa kubwa inatarajiwa kuwa ya mwendo kasi kulingana na vigezo vilivyotayarishwa na kukubaliwa na Wajenzi husika. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Suleiman Sarahan Said ambapo juzi tulijibu vizuri suala hili alikuwa hayupo atusubirie nina hakika hii kazi inaendelea vizuri na hii kero anayosema ya usafiri Baharini itaondoka kwa upande wa serikali. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri pamoja na kwamba juzi nilikuwa sipo kwa majibu hayo, lakini mimi nataka nizungumze kwa nia njema Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohd Shein alifanya kwa makusudi kununua meli moja mpya ya Mapinduzi II, kwa kweli inafanya kazi lakini inavyoonesha vigezo vyake vya ufanyaji kazi havitoshelezi kwa upande wa kushindana kibiashara.

(a) Mhe. Naibu Spika, hili Shirika sasa hivi linajiendesha kibiashara meli ambazo tulizozizoea za Mapinduzi, Maendeleo au Mapinduzi II ni meli ambazo zinachukuwa muda mkubwa karibu siku nzima kutoka Unguja na Pemba pahali pa dakika 30 mpaka masaa mawili. Je, Mhe. Naibu una mpango gani wa kununua boti mpya za kisasa zinazokwenda kwa kasi ili kuokoa muda wa wananchi wake.

(b) Meli ambayo unataka kutengeneza ya kisasa itakidhi haja isije ikawa kama Mapinduzi II ikawa mlango haufunguki mpaka iwekewe chelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kusahihisha kidogo kwamba meli yetu ya MV Mapinduzi II haichukuwi masaa anayoyasema yeye ni katika meli bora na zenye viwango

na kwa ukanda huu wa Zanzibar ndio meli inaenda kwa kasi zaidi kuliko hata hizo meli za *AZAM Marine*. Isipokuwa kama tulivyosema kuna upungufu fulani ambapo hii meli imetengenezwa zaidi kitaalamu na kisasa kwa hiyo ndio maana unakuta kwamba mlango wake unakuwa mmoja na vile vile *ram* zake kama ulivyosema zinakuwa zinahitaji viwepo na vituo maalum ambapo sisi tuko katika mpango wa kizitengeneza.

Mimi nataka kumwambia kwamba tuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba hiyo meli tutakayoinunua itakuwa ni meli ya kisasa na vile vile kama tulivyomwambia atusubiri na mimi nina imani kubwa sana wakandarasi watakaopewa kazi hii wataifanya kazi kwa viwango vya kimataifa na hii meli itakuwa ni meli ya kipekee katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Tokea wiki iliyopita huwa anaeleza kuwa serikali ina mpango wa kuleta meli ya MV. Maendeleo II. Nataka atuambie ni bajeti gani ambayo imeidhinisha fedha ya serikali kwenda kununuliwa hiyo meli ya MV. II.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, sote ni mashuhuda wakati tulipokuwa tukinunua meli ya MV. Mapinduzi II sote tulishuhudia Baraza hili la Wawakilishi likipitisha Bajeti ya vile vile serikali kupitia Wizara ya Fedha ilikuja na mpango mkakati ukiwemo wa kubana matumizi.

Mimi nataka kumwambia wakati sisi tunaendelea na mchakato huo katika bajeti yetu inayokuja tutaainisha wapi pesa tutakazozitoa kwa ajili ya kununua meli hiyo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa yasiyokuwa na ukakasi.

(a) Ni kweli katika vyombo vya baharini vinavyofanyakazi katika usafiri wa Unguja na Pemba Zanzibar kuna Meli ya MV. Maendeleo na MV. Serengeti meli hizi ni za muda mrefu sana na inaelekea kuwa hatarishi juu ya usafiri wake. Je, maisha ya kudumu zile meli bado yanakidhi kuwemo katika biashara hiyo ya ushindani Zanzibar na je, ukaguzi wa mwisho wa meli zile zilifanyiwa lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa meli ya MV.Serengeti hivi sasa tumeisimamisha isifanye safari kutokana na kwamba haiko katika hali ya kuridhisha. Kwa hiyo, kupitia mamlaka ya usafiri baharini tumekuwa tukizikagua meli hizi kila wakati na hivi karibuni tu meli ya *MV Seagull* ilikuwa imeshaanza kazi lakini baada ya kukaguliwa ikaonekana kwamba haina vigezo, kwa hiyo wamepewa ushauri waufuate na baada ya hapo itaendelea kufanyakazi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Mamlaka ya usafiri baharini meli hizi huwa tunazikagua kila wakati nataka kumuhakikishia kwamba MV. Maendeleo ni meli ambayo ni yetu sisi kama serikali vile vile nayo tunaikagua na pale ambapo itakuwa ina kasoro zozote basi na wao tutawasimamisha wasifanye kazi. Ahsante Mhe. NAibu Spika.

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, suala langu linauliza ni lini zimekaguliwa meli zile MV. Serengeti amenambia tayari imeshatolewa katika safari kwa sababu ni kongwe MV. Maendeleo ni lini imekaguliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, inawezekana hakunifahamu nimemwambia kwamba ni karibuni tu meli ya Serengeti imekaguliwa ndio maana ikazuiliwa isifanye kazi na vile vile Seagul imekaguliwa isifanye kazi. Kwa hivyo inaonekana hakunisikiliza vizuri. Meli yetu ya MV Maendeleo inakaguliwa wakati wowote na kwa sasa hivi kwa muda mrefu haijafanya kazi kutokana kwamba kuna vifaa viko matengenezoni. Kwa hivyo sisi kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini kila wakati tunakagua meli zetu na pale tunapopata taarifa kwa sababu hata katika hizo baadhi ya meli kuna watu wetu mule wanatwambia bwana meli hii ina kasoro fulani, sisi tunatoa wakaguzi wetu kupitia Mamlaka ya Usafiri baharini wanakwenda kufanya ukaguzi. Kwa hivyo tuna wajibu wa kufanya *routine* ya kuhakikisha kwamba meli zote hizi tunazikaguliwa na zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria za mamlaka usafiri baharini.

Nam. 10

Utaratibu wa Kukodisha Mikarafuu Kizimbani

Mhe. Naibu Masoud Abrahman Masoud - Aliuliza:-
Eneo la Utafiti lililoko Kizimbani linalomilikiwa na Wizara ya Kilimo lina mikarafuu ambayo Serikali imeamua kuikodisha wakati inapozaa.

Je, ni utaratibu upi unaotumika kukodisha mikarafuu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mwakilishi wa Jimbo la Bububu swali lake nambari 10 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliyopo Kizimbani inayo mikarafuu ambayo inakodishwa wakati inapozaa.

Hata hivyo, ukodishwaji wa mikarafuu hiyo unafuata utaratibu kwa mujibu wa sheria namba 9 ya manunuzi ya uhaulishaji mali za Serikali ya mwaka 2005 kwa kupitia bodi ya Zabuni ya Wizara ambayo hutangaza idadi ya mashamba yatakayokodishwa ili wanaotaka kukodi waende kuyakagua na hatimaye utaratibu wa kuwaalika kwa kila anayetaka kukodi kufikia katika mnada kwa tarehe iliyopangwa.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Katika maelezo yake kasema kuwa wananchi wanatakiwa wende kukagua na baadae kukodisha. Ni kweli wananchi huwa wanaondoka na kwenda kukagua mikarafuu hiyo lakini naomba aniambie.

(a) Je, ni utaratibu wa tenda, mnada au vyenginevyo inavyotumika ili wananchi wakodishwe.

(b) Naomba anitajie watu gani waliomba kukodishwa na nani alibarikiwa mikarafuu hiyo kwa mwaka jana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

(a) Uuaratibu unaotumika ni wa kutangaza tenda na baadae tenda hizo zitafunguliwa mbele za hawa walioomba na yule ambaye ame-*bid* katika amount kubwa zaidi ndie ambaye anapata nafasi.

(b) Data kamili ya ambao walioshiriki na wakashinda katika tenda ya mwaka uliopita nitaomba nimletee kwa maandishi.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri umetwambia kwamba mashamba haya ya Serikali yanapokuwa tayari wakati wa kukodishwa mazao yake yanatangazwa na wananchi huwa wanakwenda kwa ajili ya kukodi mashamba haya. Lakini kuna maneno yanayozungumzwa kwamba mashamba haya ya Serikali, shamba ambalo lina mishokishoki 40 au mikarafuu 50 basi linakodishwa kwa bei ya mshokishoki mmoja au mkarafuu mmoja. Je, suala hili lina ukweli na kama halina ukweli, hebu twambie hizi bei ambazo zinakodishiwa haya mazao ya Serikali kunakuwa kuna nini ndani yake mbona inakuwa hatufahamu kitu ambacho kinakuwa kinatuumiza akili sisi wananchi. Kwa sababu unakuta vile vitu mpaka vinaoza havichumwi wala havishughulikiwi hujui kama vimekodishwa au la.

(b) Tunafahamu kwamba eneo la Kizimbani lina vitu vingi vya kukodisha lakini tunafahamu sasa hivi pia kuna milangi langi mingi ambayo ipo na hii milangi langi sasa hivi ni sehemu kubwa ya mapato na mambo ya urembo na manukato. Je, kuna utaratibu gani juu ya uimarishaji wa hii milangi langi na ukodishaji na kuhifadhi hii harufu na ladha na uzuri uliopo wa hii milangi langi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, swali lake lenye kipengele namba (a) hiki ulichokisema hakina ukweli. Vile vile bei inayokodishwa mashamba haya inategemea na yale mazao yenyewe yalivyozaa na bei ya soko la Serikali ilivyo na ukubwa wa lile shamba lenyewe.

(b)Tutajitahidi katika wizara yangu kuboresha katika suala hili la milangi langi na vile vile kuwapa elimu wale wananchi kuhusiana na miti hii ya milangi langi jinsi gani ya kuitumia na kuihifadhi na kuienzi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ni matarajio yangu na mimi ninachokisema kina ukweli na Mhe. Waziri ataweza kunisaidia. Mhe. Naibu Spika, kwa miaka nenda miaka rudi Zanzibar imejipatia sifa ikijulikana duniani na kwengine kote kwamba *the spice island*. Moja katika sifa ambazo tulikuwa tunazo ni kuhusu hizi spice zote ambazo zinapatikana katika maeneo ya Kizimbani na mashamba yaliyokuwepo huko.

Lakini moja katika sifa ambayo tuliyoipata Zanzibar tunajitegemea sasa hivi kwa mapato yetu ni suala la biashara ya utalii. Lakini mgeni anapofika

Zanzibar anapotembelea maeneo haya ya Kizimbani *the spice island* kwenda kuangalia mashamba ya *spices* kwa kweli sifa ambayo inayozungumzwa nje na hali unayoikuta ni vitu viwili tofauti.

Kwamba hatuna shamba ambalo ni kubwa unaingia unakuta hizo *nutmeg, cardamom, cinnamon* na mengi ambayo tunatarajia. Je katika haya maeneo Serikali yanahodhi sasa hivi maeneo ya Kizimbani ambalo ni eneo kubwa sana ni lini Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Serikali na Wizara nyengine husika watajenga shamba ambalo mgeni anapokuja anaweza kuona haya yote yanayopangwa pamoja na juzi Mhe. Waziri wa Afya aliyataja, pilipili doria na mengine ili tuweze kutambulikana huko nje kutokana na sifa ambayo Serikali hii inajigamba kwa pamoja huko duniani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, shamba letu hili lina kila aina ya miche vile vile tungeshauri kwamba upende kutembelea halafu baadae ujue kwamba miche mingapi ipo. Kuhusu hiyo mipilipili doria pia ipo Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana nataka kuongezea majibu kwanza nataka niwashukuru sana wananchi ambao wao wenyewe wameanzisha vitalu, wameanzisha mashamba mbali mbali ya kuendeleza biashara ya *spices*.

Nataka niwashukuru vile vile wahisani mbali mbali ambao sana wamewezesha Serikali yetu kuingia katika biashara ya kuendeleza mazao haya ya *spices* kwa maana tu mbali ya kuzalisha na kuona watalii lakini vile vile katika kuingia masoko ya nje. Hili ni jambo ambalo nataka nimpongeze vile vile Waziri wa Viwanda na Biashara katika kazi moja aliyoifanya ya ku-*promote spices* zetu ziweze kusafirishwa mpaka nje.

Kwa hivyo yapo mashamba mengi sasa hivi ya wananchi mbali yale ya serikali ambayo wanasafirisha *spices* na watalii wana fursa za kwenda kuona. Kwa hivyo sio tu kwamba tunayo kwenye wizara lakini vile vile na wananchi wanafanya na Serikali inajaribu ku-*encourage* wananchi wafanye na waingie katika masoko ya nje sio masoko ya ndani tu peke yake.

Nam. 40

Kufungwa Milango ya Uwanja wa Amani

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza:-

Mlango mkubwa wa kuingilia Uwanja wa Amani uliopo katika barabara ya Muembeladu na Welezo una milango mdogo ya chuma 4. Mara zote milango hiyo midogo huwa haifunguliwi wakati wa kuingia na kutoka mpirani kiasi cha kusababisha msongamano mkubwa hasa wakati wa kutoka.

a) Sababu gani za msingi zinazopelekea milango hiyo midogo kutofunguliwa.

b) Kwanini uongozi wa Uwanja unaruhusu wafanyabiashara kuuza bidhaa zao chini ya milango hiyo midogo na kuzidi kusababisha msongamano wa Magari, Vespa na watembea kwa miguuu wanaowania mlango mmoja tu kutoka nje.

c) Ni lini Wizara itasimamia uondoshwaji wa magari yanayoegeshwa mbele ya mlango mkubwa unaotokea barabara ya Magogoni kwa Mabata na kufungua mlango huo ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame swali lake nambari 40 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kufunguliwa na kufungwa kwa milango midogo iliopo Uwanja wa Amani inategemea aina ya shughuli inayofanyika. Inapofanyika shughuli kubwa milango yote mikubwa na midogo hufunguliwa.

b) Uongozi wa Uwanja wa Amani haujaruhusu wafanya biashara kuuza bidhaa zao chini ya milango. Kinachojitokeza ni ukaidi wa wafanyabiashara hao kukaidi katazo au Amri ya Uongozi. Hata hivyo uongozi utashirikiana na vyombo vya Dola kuhakikisha wafanyabiashara hao wanatii amri hiyo.

c) Mhe. Naibu Spika, suala la magari yaliyoegeshwa mbele ya mlango mkubwa unaotokea barabara ya Magogoni kwa mabata ni suala sugu na ni la muda mrefu. Wizara kupitia Uongozi wa Uwanja wa Amani utaendelea kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya na Mkoa na kuhakikisha magari yaliyoegeshwa yanaondoshwa.

Kuhusu mlango mkuu na mdogo kwa upande huo wa Magogoni unakuwa wazi wakati zinapofanyika mechi na shughuli nyenginezo. Ahsante.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na sina budi kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ameeleza kwenye jibu lake kwamba mara zote milango midogo huwa inafunguliwa wakati wa shughuli kubwa. Mimi swali langu limejikita kwenye shughuli za mpira wa miguu yaani kwenye mechi za mpira wa miguu mara nyingi milango ile inafungwa, inakuwa mlango mmoja tu uwazi. Tunashukuru kwenye shughuli kubwa alizozieleza Mhe. Waziri kweli milango inafunguliwa. Lakini kwenye mpira wa miguu mlango unaokuwa wazi ni mmoja tu.

Sasa ninamuuliza Mhe. Waziri kama kakubali rai hii je, lini ataifungua milango hiyo kwa mechi za mpira wa miguu ili kupunguza msongamano wa magari wakati wa kutoka na kuingia uwanjani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na Mhe. Mwakilishi kusema kwamba swali lake limejikita zaidi katika milango midogo. Lakini na mimi pia katika majibu nimemwambia kwamba milango hii midogo lakini pia nikaongezea kuwa uwanja ule na milango mikubwa pia ipo. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba milango hii inafunguliwa wakati wote wa timu zile za mchezo wa mpira ila jamii yetu ya Wazanzibari hatuna utamaduni wa kuangalia timu hizi za mipira. Kwa hivyo inategemea na mechi zenyewe. Ikiwa mechi ina idadi ya watu milango ile hufunguliwa mikubwa na midogo pia na yote hutumika. Lakini wakati mwengine pia na vyombo vyetu vya ulinzi wakati mwengine inabidi kutumia mlango mkubwa kwa kutaka watu waingie kwa utaratibu maalum wanao-*support* wao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pembezoni mwa uwanja wa Amani upande wa Magogoni kuna jengo la ghorofa la siku nyingi ambalo lilikuwa na mgogoro kati ya Serikali na mmiliki. Je, Mhe. Waziri mgogoro ule umefikiwa wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba jengo lile lilikuwa na mgogoro lakini naomba nimjibu mwakilishi kwamba sijafuatilia kwa kina mgogoro huo kwa hivyo nimuombe sana awe na ustahmilivu nitafatilia kwa kina hatima yake nitampatia majibu yaliyo sahihi. Kwa kuwa tumetakiwa tujibu kwa usahihi. Nimuombe sana, natarajia apate majibu ya usahihi na uhakika nitafatiliwa zaidi hatima yake ninampatia majibu ya usahihi na kwa ufupi.

Mhe. Mohammed Said Dimwa: Mhe. Naibu Spika, nishukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu marefu yasiyoleta afya na tija naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwenye jibu lake mama kuwa vijana wale ni wakorofi na wanaleta adha wakati wa kupita na kutoka katika uwanja ni lini Serikali itawafikiria kuwajengea sehemu mbadala ya kuweza kuweka zile biashara ambazo zinavutia katika mechi zetu.

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa amekiri kuwa hakulifatilia suala la mgogoro lililotokea ni waziri gani anayelijua lini wanaweza wakalifatilia na tukapata majibu ya uhakika katika Baraza hili la wananchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kutoa majibu ambayo yamefatiliwa na yamefanyiwa utafiti wa kutosha na kuyawasilisha hapa yakiwa sahihi na yameelezwa tofauti na anavyoeleza Mhe. Dimwa. Pia nakuomba sana Mhe. Naibu Spika, kuwaomba waheshimiwa wenzangu pamoja na kwamba masuala wanayowasilisha yanalenga lile swali ambalo wanaliuliza basi ni vyema wakawa na ile taratibu na lugha ambayo inakwenda sambamba na uhalisia ulivyo.

Baada ya hayo naomba sasa nimjibu Mhe. Dimwa wa Jimbo la Mpendae swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mheshimiwa amependa kujua kwamba ni lini watu wale wakaidi wakorofi, ambao wapo pale watapatiwa sehemu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu hii kumekuwa na watu ambao hawapendi kufuata sheria. Mifano mizuri imewahi kutokea kwa watu wakorofi kama hawa, magereji mengi yamekuwa maeneo ya mjini yakiwemo sehemu za Mjimkongwe, yakiwemo maeneo ya Kwahani na wote wale walipatiwa nafasi wakaondoshwa wakapelekwa sehemu nyengine za kufanya gereji lakini bado wana tabia za kuvamia maeneo amabayo hawakuruhusiwa, ulifika wakati Mhe. Naibu Spika, wameondoshwa wote wale katika maeneo ya Amani na kupatiwa sehemu za kufanya gereji zao zilizikuweko nje ya mji lakini bado wamerejea na kuendeleza zile shughuli. Kwa hivyo, kama alivyosema Naibu Spika, katika

jibu mama kwamba utaratibu kwa kushirikiana na vyombo vya dola utaendelea kufanyika, utaendelea kuwaondosha na sasa hivi hatutaweza kuwapatia sehemu kila wanapodai waweze kupatiwa sehemu.

Kuhusu swali la (b) kwamba mzozo wa nyumba ililokuweko kwa upande wa Magogoni kama tulivyosema mzozo huo ni wa serikali na kama upo unaendelea kuwepo Serikali unaendelea kufanya tararibu zake za kuufatilia, na hapo tutakapokamilisha majibu ya matokeo tuliyoyafikia basi tutawasilisha katika Baraza lako tukufu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Nam. 21

Utaratibu wa Wananchi Kupeleka Mahitaji Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kabla ya kuuliza suala langu Namba 21 naomba uniruhusu kutoa pole kwa Mhe. Abdalla Diwani na Mhe. Hassan Hafidh kwa mkasa uliowakuta juu ya suala hili naomba serikali itowe majibu muafaka kuhusu suala hili.

Pamoja na Wizara ya Afya kuweka utaratibu wa kutumia walinzi kwa wananchi wanaoingia na kutoka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, bado malalamiko yamekuwa makubwa kwa wananchi wanaofika hospitalini kupeleka mahitaji ambapo wakati mwengine wananchi huzuiwa kutoa fedha za mahitaji na chakula kwa wagonjwa wao. Kwa kuwa wananchi wengine wanatoka mbali ya Mji na huduma wanazozipeleka ni muhimu kwa wagonjwa wao.

a) Kwanini wananchi hawaruhusiwi kupeleka mahitaji kwa wagonjwa wao ambazo ni muhimu na ndio yanayosaidia matibabu yenyewe.

b) Kwanini wananchi kama hao wasiwekewe utaratibu maalum wa kuwasaidia badala ya kuwekwa hadi jioni wakati wanatoka maeneo ya mbali kama Makunduchi, Muyuni nakadhalika.

c) Lini Wizara itachukua hatua za haraka za kuwaelimisha askari wanaoshughulikia shughuli za ulinzi hospitalini hapo ili waweze

kutekeleza majukumu yao bila ya kuwepo mivutano na wananchi na kutumia lugha za kiungwana na hekima.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake Nam. 21 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina utaratibu maalum wa kuwaona wagonjwa na kukaa nao ikibidi hasa kwa wagonjwa wenye mahitaji maalum kwa mujibu wa utaratibu wa huduma za afya. Hospitali imeweka walinzi katika mlango mkuu na baadhi ya sehemu kwa lengo la kuleta utulivu wa wagonjwa na ufanisi wa utendaji wa wafanyakazi wanaotoa huduma kwa wagonjwa hao. Utaratibu huu ni wa kawaida katika mifumo wa uendeshaji wa hospitali kwa lengo la kuhakikisha utulivu katika eneo husika pia husaidia sana kuzuwia udhururaji na upotevu wa vitu mbali ndani ya hospitali.

Mhe Naibu Spika, Hospitali imeweka muda maalum kwa ajili ya kuangalia na kupeleka mahitaji kwa wagonjwa hao, nao ni saa 12:00 hadi saa 1:00 za asubuhi, saa 7:00 hadi saa 8:00 za mchana na 10:00 hadi saa 12:00 jioni.

Mhe Naibu Spika, suala la kuweka utaratibu maalum ambao utakuwa tofauti na utaratibu uliopo sasa kwa jamaa wanaochelewa kupeleka mahitaji kwa wagonjwa wao, swali hili linaweza kuleta usumbufu mkubwa kwa wagonjwa wenyewe lakini pia kwa *staff* ambao mara baada ya kumaliza muda wa kuangalia na kupeleka mahitaji kwa wagonjwa wao huendelea kutoa huduma kwa wagonjwa. Huduma ambazo zinapaswa kutolewa huku kukiwa na utulivu na faragha baina ya mgonjwa na daktari au *nurse* anayetoa huduma hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na ushauri Mhe. Mwakilishi wa kuwasaidia jamaa wa wagonjwa wanaotoka maeneo ya mbali mfano Makunduchi, Muyuni, Uroa na kadhalika, ili kuweza kufikisha mahitaji ya wagonjwa wao mara wanapofika. Kwa kuzingatia ushauri huo Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imefanya mazungumzo na viongozi wa walinzi na kuwataka kutumia ubinadamu zaidi inapojitokeza hali kama hiyo au dharura nyengine.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu inapenda kutoa wito kwa wananchi yaani jamaa wa wagonjwa kutoitegemea sana fursa hii bali wajihimu kwa kutumia muda maalum uliwekwa kwani licha ya kupeleka mahitaji ya wagonjwa wao

pia wanapata nafasi ya kutosha ya kuweza kujua hali halisi ya mgonjwa inavyoendelea. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Naibu Waziri utanisamehe nikuombe radhi na niseme tena unisamehe kwa kuomba radhi, tunamsaidia Dk. Ali Mohamed Shein kazi aliyoifanya katika Wizara ya Afya tutakuwa hatujafanya haki kama hatujamsifu. *(Makofi)*

Kazi anayofanya Rais wetu kama hatukuitangaza tutakuwa hatukumfanyika haki na wewe shahidi na wajumbe wote shahidi ikiwepo Hospitali aliyofungua juzi ya Abdalla Mzee kujenga *ICU*, huduma za wazazi kuweka bure, hospitali aliyofungua juzi Mnazi Mmoja tumeiona lakini bado hali hairidhishi. Sijui tuseme lugha gani hapa niseme uzembe, uwajibikaji, sijui lugha gani. Hospitali ya Mnazi Mmoja hichi kituo kirefu ili kutoa pole Mhe. Abdalla Diwani, Mhe. Hassan Hafidh yamewakuta mimi nakwambia tena Mhe. Naibu Waziri jana saa 5:00 usiku na leo asubuhi nimeenda kulifanyia kazi suala hili bado elimu yenu sijui mnatoa kwa lugha gani, kizungu, kinyamwezi, kihindi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza swali, nimekupa nafasi ya kuuliza swali sio kutoa tena hotuba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Elimu alotoa sijui lugha gani atufahamishe hili Baraza kwa lugha gani anawapa elimu watendaji wale nina uhakika nilokuwa nao hamjawaita wafanyakazi mtakuwa mmemuagiza msimamizi mmoja tu, elimu mliyotoa haifiki bado unyanyasaji mpaka jana upo nakwambia upo mimi jana nilitaka kufungiwa honda yangu usiku.

a) Ni lini mtachukua utaratibu wa kuwafahamisha kweli lakini kama hapo patakuwa hapatoshi.

b) Kwa kuwa uzembe unaoendeshwa na Wizara yako umenza kusababisha hata vifo katika mwezi huu watoto waliozaliwa kiwango chao hakikufika wakawekwa katika *Incubator* kwa kukosa *oxygen* wawili wamekufa. Mmeunda tume hiyo na suala hili linahusu Mnazi Mmoja lini mtawajibika kuwafahamisha hawa watu, Rais anafanya kazi kubwa lakini bado utendaji wenu haufiki pahali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika naomba niseme kweli kwamba maelezo alivyoyatoa mengi sikupata swali liko wapi, naomba arudie swali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku nafikiri ulikuwa zaidi uulize maswali kuliko maelezo umetoa maelezo mengi mpaka Mheshimiwa anasema hajakufahamu, hujauliza hata swali moja uliza maswali yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika kwanza nitulie kidogo lugha nitayotumia Mhe. Naibu Waziri lugha, umesema mmekaa na wafanyakazi wahusika kuwafahamisha nataka kujua lugha gani mnayowafahamisha ya kiswahili, ya kizungu, ya kinyamwezi ya kihindi ili wapate kufahamu hili tukio linaendelea mpaka hivi leo asubuhi linaendelea. Sasa nataka kufahamu hiyo lugha mliyowaambia wakawa hawasikii wale watendaji wenu lakini kama hapo hapatoshi la pili uzembe huu unaoendeshwa na hospitali tumepiga kelele mara nyingi humu ndani hivi juzi kumetokea tukio watoto wawili wamezaliwa muda wao hawakufika wakatiwa katika *incubator* kwa sababu ya kukosa *oxygen* wakafariki watoto hatua gani mliyochukua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba nimjibu Mhe. Jaku kama ifuatavyo:-

Mhe. huwa tunatumia lugha ya kiswahili kuzungumza na wafanyakazi wetu kuwaelimisha kwa lolote ambalo linatokea huwa tunatumia zaidi lugha ya kiswahili lakini kuhusu hili kwamba uzembe uliotokea Mhe. kuhusu hilo ambalo amelizungumza maelezo zaidi yatatolewa baada ya kukamilisha kwa utafiti, lakini Mhe. Waziri anaweza akatoa maelezo zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mwanana aliyotoa Mhe. Naibu Waziri naomba nitowe nyongeza ya majibu hayo kwa maswali yote mawili aliyouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub la msingi pamoja na la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme sheria zinatutaka sisi tutekeleze sheria hasa za afya zinatutaka sisi tutekeleze kwa ushahidi namshukuru sana Mhe. Hassan Hafidhi alifika kuniona akaleta ushahidi kwamba kulikuwa na mzazi alotokea jimboni kwake ambaye ameletwa na gari aina ya *carry* na watu ambao wamemsindikiza, na mimi nimelifanyia kazi mimi mwenyewe binafsi nimekwenda nikakaa na Uongozi wa Mnazi Mmoja, nimekaa na viongozi wa walinzi hao, nimekaa na walinzi wote tumewaita kwa pamoja nimekaa nao chini ya mti tumezungumza ushahidi alowasilisha Mhe. Hassan Hafidh ni wa kweli na hilo tukio lilitokea naomba tuambizane ukweli ushahidi aliowasilisha ni wa ukweli na hilo tukio lilitokea.

Tukawapa nafasi walinzi nao watoe hoja zao walichokosea walinzi ile *carry* ilikuja na watu takriban watu 20 wao wakawaambia wanataka kumruhusu mzazi na watu wawili tu waingie ndani kwa *time* ile ya usiku wasiruhusiwe watu wote 20 kuingia. Ilikuwa busara itumike na mabishano yasitokezee ili watu 18 wabaki waingie wawili pamoja na kumsindikiza yule mzazi, hapo ndiyo sintofahamu ilipotokezea ya Mnazi Mmoja. Tumewapa walinzi wetu onyo na tumewaambia kwamba watumie busara wanapoona gari imekuja na mgonjwa na ikiwa imekuja na watu wengi kwa kutumia lugha nzuri ya kuweza wale watu kupungua, waingie wale ambao wanamsindikiza mgonjwa tu hilo limefanyika la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, lilofanyika ni kwamba tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi kwamba wanapoleta mgonjwa wasiwe wakali kama wameruhusiwa watu wawili wakubali watu wawili kuingia, katika ukoo watu hamsini wakiruhusiwa wanne waridhike kwa sababu Mnazi Mmoja haiwezi kuchukua watu wote hamsini kwa mgonjwa mmoja akazungukiwa kwenye kitanda. Tunaelewa familia zetu ni kubwa na kila moja anataka kwenda kumuangalia mgonjwa, kwa hivyo naomba waridhike. Walinzi walicholalamika kwetu sisi ni kwamba wakija pale wasindikizaji wagonjwa wanakuwa wakali mno na mmoja alikuwa na kisu na wametuomba sisi tuwasaidie kupata silaha lakini sisi tukawaambia eneo la hospitali sisi hatukubali silaha ya aina yoyote kwa sababu ni eneo la kutoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar.

Sasa narudi kwa Mhe. Jaku kesi hii ya watoto wawili inashughulikiwa sitopenda kutoa taarifa zozote kwa sababu uchunguzi unaendelea na uchunguzi huo umehusisha ngazi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hatufanyi sisi peke yetu kuna vyombo vyengine vya ziada ambavyo vinafanya kazi hiyo. Kwa hivyo, siwezi kuizungumzia hapa wala siwezi kutoa maelezo yoyote na ninaomba sana asiendelee kuizungumzia kesi hiyo kwa sababu inashughulikiwa. Ni sawa sawa kitu kiko kwenye uchunguzi ataharibu uchunguzi wetu tunataka kuwasaidia wananchi walomtuma yeye kuja humu ndani.

Lakini jengine Mheshimiwa, Mhe. Jaku Hashim Ayoub amekuwa akileta shutma nyingi lakini mpaka leo hajawahi kuwasilisha ushahidi hata mmoja, amekuwa akitoa shutma nyingi sana sisi tunatambua Dk. Shein mambo anayofanya katika Wizara ya Afya na tupo kufanya kazi na kumsaidia Dk. Ali Mohmmed Shein katika kutimiza malengo yake katika sekta ya Afya. Lakini shutma hizi zote mpaka leo haujawasilishwa ushahidi naomba niseme hao watoto wawili, watoto wawili hao waliofariki babu yao kawasilisha ushahidi

kamili na mama yao kenda kufanyiwa *interview* na timu yetu nzima ya kutoka Wizara ya Afya pamoja na vyombo vyengine husika.

Kwa hivyo, kama ana ushahidi wa walinzi Mhe. Hassan Hafidh aliwasilisha ushahidi na katika vikao vyetu nje ya Baraza hili pia ambao tumekaa kawasilisha Mhe. Hassan Hafidh ushahidi naomba awasilishe ushahidi mbele yako hapo ili tuweze kutekeleza. Haya maneno ya kutoa shutma bila kuwasilisha ushahidi yanawavunja moyo sana wafanyakazi wetu na wanatulalamikia sisi jamani mkizungumza kwenye Baraza toweni na ushahidi, ili tuweze kuchukuliwa hatua *otherwise* tunakuwa tunasingiziwa sisi wafanyakazi wa Wizara ya Afya tunaonekana kwamba tunavunjika moyo katika kuwatumikia wananchi.

Kwa hivyo naomba Mhe. awasilishe ushahidi huo aliokuwa nao kama walivyo wenzake na kama walivyofanya kwa ajili ya hizi kesi zinazoendelea. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru nasimamia kanuni ya 59 (3) Mhe. Naibu Spika, mimi sijawahi kulewa wala sijawahi kuvuta bangi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba arekebishe kauli yake hakuna aliyelewa wala kuvuta bangi naomba arekebishe kauli yake tafadhali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hajaambiwa mtu wewe kiswahili nafikiri hakijui Mheshimiwa ninachozungumza nasema mimi mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Kiswahili nakijua na ninazungumza lugha saba.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku sijakuruhusu kusema Waheshimiwa Wajumbe kipindi cha maswali na majibu kimemalizika. *(Makofi)*

Sasa baadaye nitampisha Mhe. Mwenyekiti aje aendelee na utaratibu mwengine lakini waheshimiwa wajumbe kabla ya kuondoka naomba nitowe matangazo machache. Kwanza kabisa naomba niwatambulishe waheshimiwa wajumbe naomba utulivu naomba utulivu sana kwa sababu naona kama minong'ono imekuwa mingi.

Naomba kuwatambulisha wageni wetu leo ambao ni wageni wa Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jang'ombe pamoja na Mhe. Hassan Hafidh (Diaspora) wa Jimbo la Welezo.

Wageni hao wanatoka *World Venture Club* majina yao ni:

1. Dr. Jumanne Said Alawi,
2. Ndugu Asifiwe Kiyofika Kiberenza,
3. Ndugu Loice Mushi,
4. Ndugu Salim Juma Kula,
5. Ndugu Sara Isack Tarimo,
6. Ndugu Evelin Kakwezi,
7. Ndugu Hashim Migoda Mataka,
8. Ndugu Maneno Khamis

Waheshimiwa Wajumbe, hawa wageni wetu wana nafasi kubwa sana katika kuwasaidia Wanzanzibari na Watanzania wote kwa jumla hasa wanaposafiri nje ya nchi kwa makaazi na fursa nyengine za kibiashara. Kwa hivyo, mnapewa fursa hiyo ya kuitumia waheshimiwa. Karibuni sana wageni wetu.

Tangazo jengine ni taarifa ya upigaji wa picha za vitambulisho vya kazi kwa wajumbe na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi, waheshimiwa wajumbe pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi tunaarifiwa kwamba kutakuwa na zoezi la upigaji wa picha za vitambulisho vyetu vya kazi kwa wale ambao hawana kabisa vimepotea au vina makosa. Wapigaji picha hizo tayari wapo chumba cha kusomea juu *reading room.* Kwa hiyo tunaombwa tuitumie fursa hiyo pia.

Tangazo jengine Waheshimiwa Wajumbe kutakuwa na kamati ni wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wakutane katika ukumbi chumba namba tatu juu.

Na tangazo la mwisho Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Zulfa anaomba wawakilishi wanawake wanaotokea Pemba tukimaliza kikao hiki maana saa 7:00 tukimaliza wabakie kwa ajili ya kikao kidogo.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nampisha Mwenyekiti aweze kuendeleaa na utaratibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa na afya njema na wazima kushiriki Baraza hili tukufu katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niwasilishe hotuba yangu ya kuwasilisha Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya 2006.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi (*ZFDB*) yaani Zanzibar Food and Drug Board ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya 2006. Sheria ilifuta sheria ya madawa na madawa hatari ya wakati huo, sheria Nam. 6 ya 1986 na Sheria ya Afya ya Jamii, Sura ya 73 iliyokuwa ikisimamia usalama wa chakula hapa Zanzibar. Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ilianza kufanya kazi rasmi mnamo mwaka 2007.

Mhe. Mwenyekiti, dhamana kubwa ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ni kusimamia ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi na vifaa tiba na ufanisi wa dawa kama ilivyoanishwa katika sera ya udhibiti ya *ZFDB* ya 2013.

Tangu kuanza kufanya kazi kwake hapo 2007, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi imejitahidi sana kufanya kazi zake na kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa na kufikia malengo yake iliyojiwekea, yaani kulinda afya za wananchi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo, taratibu sanifu za kiutendaji na viwango husika vilivyowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi chote ambacho bodi hii imefanya kazi zake imeweza kufikia mafanikio mbali mbali kama ifuatavyo:

Miundombinu

Kama inavyokumbukwa kuwa bodi ilianza kufanya kazi katika kontena lilokuwepo hapo Majestic Cinema pembeni na kuhamishiwa katika

kilichokuwa Kiwanda cha Madawa ambayo sasa ni hospitali yetu inayotoa huduma kwa mama wajawazito pamoja na watoto. Baada ya hapo wamehamia katika jengo lilokuwa la uchapaji cha *Al-Khayria Press* maeneo ya Mombasa Unguja. Baada ya kulifanyia ukarabati mkubwa ambapo imepatikana nafasi ya kutosha kwa ajili ya wafanyakazi na maabara kubwa na ya kisasa ambayo inatarajia kupata ithibati ya kimataifa ifikapo Julai, 2017 *inshaallah*.

Katika kuimarisha kazi zake za kila siku bodi iliweza pia kutengeneza kanuni na miongozo mbali mbali inayohusiana na udhibiti wa dawa, chakula na vipodozi na vifaa tiba ili iweze kurasisha utendaji wake.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, bodi imeweza kushiriki kikamilifu katika uwiano wa usajili wa dawa katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki ambapo Zanzibar imeingia kama mwanachama anayejitegemea, lengo likiwa ni kuhakikisha tunapata dawa zilizokuwa bora, salama na sanifu kwa bei nafuu. Mradi huu umeiwezesha bodi kujiimarisha katika nyanja za usajili, ukaguzi, teknolojia ya habari ya mawasiliano pamoja na maabara.

Mhe. Mwenyekiti, miongozo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusajili dawa na ukaguzi wa viwanda vya dawa imeanza kutumika kwa mashirikiano makubwa katika tathmini ya pamoja ya dawa (*Join Medicines Evaluation*) na ukaguzi wa pamoja wa dawa (*Joint Medical Inspection*). Aidha, uanzishwaji wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma (*Quality Management System*) na mfumo wa habari kwa elektoroniki (*Information Management System*) umeweza kuweka taratibu sanifu za utendaji kazi (*SOP's*) zilizo imara ambazo zimeongeza ufanisi wa hali ya juu katika kufanikisha matarajio ya wateja wetu.

Rasilimaliwatu

Mhe. Mwenyekiti, rasilimali watu ni nyenzo muhimu kwa taasisi katika kutekeleza na kufikia malengo yake. Bodi wakati inaanzishwa mwaka 2007 ilikuwa na wafanyakazi 40, na kwa sasa ina jumla ya wafanyakazi 85 ikijumuisha wataalamu katika fani mbali mbali za udhibiti kama vile Wafamasia, Wataalamu wa Chakula, Mabwana na Mabibi Afya, Wahandisi, Wataalamu wa Maabara na Wakaguzi wa Nyama na Maziwa.

Bodi za *ZFDB*

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa maamuzi ya kiutendaji ulisimamiwa na bodi ambayo inajumuisha wajumbe kutoka taasisi mbali mbali za umma, sekta

binafsi ambao kwa ujumla walitekeleza majukumu yao kwa misingi ya uwazi na kufata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Bodi ya mwisho Mhe. Mwenyekiti, iliyomaliza muda wake mnamo mwezi wa Oktoba, 2016 ilikuwa na wajumbe wafuatao:

1. Dkt. Jamala Adam Taib ambaye alikuwa ni Mwenyekiti, yeye ni Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya.
2. Dkt. Burhan Othman Simai alikuwa ni Katibu wa Bodi anaingia kwa nafasi yake kama Mrajis Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi.
3. Bi. Chai Ali Mohammed, yeye ni Mjumbe kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa sheria hiyo
4. Dkt. Fadhil Mohammed Abdalla, Mkurugenzi Kinga kutoka Wizara ya Afya, anaingia kwa mujibu wa sheria hiyo kwa nafasi yake.
5. Dkt. Yussuf Haji Khamis, Mjumbe yeye anatokea Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi anaingia kwa nafasi yake ya kuwa Mkurugenzi Uzalishaji na Utatibu.
6. Dkt. Habib Ali Sharif kutoka Wizara ya Afya anaingia kama Mfamasia Mkuu.
7. Dkt. Abdalla Sharif Maalim anatokea Ofisi ya Mfamasia Mkuu, Pemba anaingia kwa nafasi yake kama Afisa.
8. Dkt. Slim Rashid Juma kutoka Wizara ya Afya anaingia kama Mkemia Mkuu wa Serikali katika bodi hiyo.
9. Ndg. Mohammed Jafar Jumanne, Mjumbe yeye anatokea Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko anaingia kwa nafasi iliyotajwa katika sheria hiyo iliyokuwepo.
10. Bi. Mwanaidi Ali Khatib, Wizara ya Kilimo Mifugo, Maliasili na Uvuvi, Mtaalamu wa Chakula.
11. Bi. Sada Issa Omar, Mjumbe Mamlaka ya Kusimamia Mazingira anaingia kutoka Idara ya Mazingira.
12. Bwana Hiti Baran Silo yeye ni Mkurugenzi Mkuu *Tanzania Food and Drugs Authority*, Mamlaka kama hii iliyokuweko Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaingia kama Mjumbe na
13. Ndg. Juma Hamad Juma kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara kama ni mwanachama wa Jumuiya hiyo *ZNCCIA*

Mhe. Mwenyekiti, utagundua kwamba marekebisho haya yanayoletwa kwetu hapa mbele yetu leo yatapunguza bodi hii takriban nusu kutoka wajumbe hao 13 hadi kufikia wajumbe 7 kwa mara hii ambao wengi wao watakuwa hawamo tena na watakuwepo wale mahsusi wanaohusiana na masuala haya moja kwa moja.

Kazi za Udhibiti

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 10 tokea kuanzishwa kwake Bodi hii ya Chakula, Dawa na Vipodozi imeendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika kufikia lengo lake la kuhakikisha kuwa bidhaa za chukula, dawa na vipodozi zilizopo kwenye soko la Zanzibar ni bora na salama kwa matumizi ya wananchi wote. Hii inajumuisha shughuli mbali mbali zikiwemo ukaguzi na usajili.

Hadi kufikia mwaka 2017, maduka ya chakula 1179 yameweza kukaguliwa, maduka ya dawa (*Pharmacy na OTC*) 346 yameweza kukaguliwa, maduka ya vipodozi, 101 yameweza kukaguliwa, maduka ya vifaa tiba 4 yameweza kukaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine kuanzia mwaka 2015 ukaguzi wa bidhaa (*inspection*) za chakula zinazoingia nchini umeendelea katika nchi mbali mbali ambazo bidhaa hizo huzalishwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa chakula, dawa na vipodozi na vifaa tiba vimetoka kwenye vyanzo vinavyoaminika na vinatengenezwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita jumla ya viwanda 15 vya chakula na viwanda 15 vya dawa vilikaguliwa katika nchi mbali mbali zikiwemo India, China, Morocco, Marekani, Oman, Urusi, Brazil, Afrika ya Kusini na Poland ili kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo zinazokuja hapa nchini kwetu kwa ajili ya kumlinda mwananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuweza kufatilia kwa karibu mwenendo wa biashara za chakula, dawa na vipodozi na vifaa tiba. *Zanzibar Food and Drugs Board* ina wajibu wa kuwasajili wafanyabiashara wote na bidhaa zinazodhibitiwa na bodi moja kwa moja ili kuhakikisha wanaendelea kukidhi vigezo kama ilivyoelekezwa katika sheria, kanuni na miongozo ya *Zanzibar Food and Drugs Board.*

Kwa muda wa miaka 10 hivi sasa idadi ya biashara na bidhaa zinazodhibitiwa na *ZFDB* imekuwa ikiongezeka sana na hii imepelekea kufikia maduka ya chakula 852 mnamo Januari, 2017 kutoka maduka 67, maduka ya dawa yamefikia 235 kutoka 250, maduka ya vipodozi yamefikia maduka 34 kutoka maduka 13, maduka ya vifaa tiba yamefikia 6 kutoka palipokuwa hakuna duka hata moja hapo kabla, bidhaa za chakula ya yamefikia maduka 37, dawa maduka 20, virutubishi maduka 8, vifaa tiba maduka 11.

Mhe. Mwenyekiti, tokea kuanzishwa kwa *ZFDB* mpaka kufikia mwezi wa Januari, 2017 jumla ya tani 1,472 za chakula na tani 20 za dawa na vipodozi ziliteketezwa baada ya kuonekana zitaleta madhara kwa binadamu.

Aidha, jumla ya tani 2,802 za chakula zilirejeshwa katika nchi zilizokotoka baada ya kubainika kuwa haziko salama kwa matumizi ya binadamu hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada iliyokuwa nayo *ZFDB* katika kuwaelimisha wananchi na wafanyabiashara juu ya taratibu mbali mbali zinazohusiana na biashara na bidhaa zinazodhibitiwa na *ZFDB*, bado kuna watu kwa makusudi wameendelea kuvunja taratibu hizo.

Hatua mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa kama vile kuwaandikia barua za onyo wanaokiuka taratibu kufunga kwa muda au moja kwa moja maeneo yao ya biashara na kuwafungulia kesi za mashtaka moja kwa moja. Ambapo jumla ya kesi 10 zimepelekwa Mahakamani na kutolewa hukumu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mashirikiano na taasisi nyengine za serikali suala la udhibiti wa chakula ni la kitaifa, hivyo *Zanzibar Food and Drugs Board*, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi imekuwa ikishirikiana na taasisi mbali mbali ili kuongeza ufanisi katika kazi za udhibiti na taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Biashara kupitia taasisi yake ya *TBS* Mhe. Waziri wa Biashara juzi alijibu hapa katika swali la nyongeza juu ya mashirikiano baina ya *TBS* na *ZFDB*, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Kusimamia Mazingira *ZEMA* na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Katika kutekeleza kikamilifu kanunu za nyama na maziwa, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi iliwahamasisha wakaguzi wa nyama sita kwa kudumu na wakaguzi wanane wa muda kuja Wizara ya Afya ili kuimarisha ukaguzi wa bidhaa za chakula zitokanazo na mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya marekebisho ya sheria hii ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kwa lengo la kuanzishwa wakala wa serikali ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa chakula, ubora na ufanisi wa dawa za binadamu na mifugo na ubora na usalama wa vipodozi hasa akina mama na vifaa tiba. Marekebisho haya yanaenda sambamba na mapendekezo yaliyotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo sisi tunashiriki moja kwa moja kama mjumbe pamoja na Umoja wa Afrika *(AU)* ambapo kwa pamoja jumuiya hizo zimetunga sheria (*Model Law*) inayoweka

mfumo wa usimamizi wa shughuli zote zinazohusiana na usimamizi wa chakula, dawa na vipodozi katika nchi wanachama wa jumuiya.

Mhe. Mwenyekiti, chini ya mapendekezo hayo, inaelezwa kwamba kila nchi mwanachama anapaswa kuwa na chombo chenye muundo wa mamlaka au wakala wa serikali. Chombo ambacho kitakuwa na kazi ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi ndani ya nchi husika na ndani ya jumuiya kwa ujumla.

Kufuatia mapendekezo hayo ambayo Tanzania imetia saini moja kwa moja mswada unapendekeza kubadili muundo wa bodi na badala yake sasa kuwa Wakala, Wakala wa Serikali kama ilivyopendekezwa na kukubaliwa pia na Baraza la Mapinduzi katika kikao chake cha tarehe 17/8/2016 ambacho kiliiagiza wizara kuwasilisha mapendekezo haya na marekebisho haya ya sheria mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo hayo ya Jumuiya ya Afrika pamoja na Afrika Mashariki, pamoja na mapendekezo ya Baraza la Mapinduzi Mtendaji Mkuu wa Bodi atakuwa sasa Mkurugenzi Mtendaji badala ya Mrajis nafasi aliyonayo hivi sasa baada ya sheria hii kupitishwa na Baraza. Na ambao uteuzi wake utafanyika moja kwa moja na Mhe. Rais badala ya waziri kama ilivyokuwa hivi sasa.

Vile vile Wajumbe wa Bodi watatoka katika taasisi ambazo kimsingi ndio wadau wakuu ama wahusika wakuu wa shughuli za bodi kama ilivyopendekezwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Afrika katika mlolongo wa masharti hayo ambayo Tanzania imeridhia.

Vile vile, mswada huu unakusudia kuimarisha mashirikiano ya kikanda, uwiano wa udhibiti wa bidhaa zinazosimamiwa na *ZFDB* kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Bara zima la Afrika. Hapa nitaomba kidogo nitoe maelezo ya ziada ya Mhe. Mwenyekiti ili ifahamike vizuri zaidi kwa nini tunatoka kwenye bodi tunaelekea kwenye uwakala na Mwenyezi Mungu akitujaalia siku za usoni itakuwa mamlaka ambayo itakuwa inadhibiti mamlaka yenyewe yenye kudhibiti vyakula, dawa na vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili nataka kutoa maelezo kidogo nchi zote wanachama ambao wame-*sign* mkataba huu wanahofu kwamba kama na sisi hatujenda kwenye uwakala zile dawa feki na bidhaa nyengine, vipodozi feki

vinaweza kupenya kupitia soko la kwetu. Kwa sababu kote watakuwa wamekinga lakini sisi kama hatujabadilisha sheria zitaweza kupenyea huko. K wa hivyo, kuekwa uwakala kutasaidia kwenda sambamba na sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki nzima, ambapo bidhaa sasa hivi kama mnavyoona, bidhaa kutoka nchi mbali mbali zinaingia. Wengine wanatumia *Colgate* hapa, wengine wanatumia Kimbo na vifaa mbali mbali vinavyotokea nchi jirani. Kwa hivyo, lengo kuu ni kuipeleka kwenye uwakala ambayo itakuwa na mamlaka makubwa zaidi kuliko bodi ya kuweza kufanya udhibiti huo huo pamoja na huyu Mkurugenzi Mtendaji sasa kuteuliwa kuwa na uteuzi wa Mhe. Rais moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umegawika katika sehemu kuu mbili:

Sehemu ya Kwanza

Sehemu ya kwanza kabisa inajieleza juu ya jina la sheria ambalo litasomeka sambamba na sheria Nam. 2 ya 2006 pamoja na marekebisho ya kifungu cha 2 ambapo kinaeleza maana ya maneno mbali mbali ikijumuisha, kufuta neno "Mrajis" na badala yake sasa kuweka maneno "Mkurugenzi Mtendaji" anapanda cheo kidogo huyu, anatoka kwenye *registrar* sasa anakuwa *Managing Director,* Mkurugenzi Mtendaji.

Aidha, kifungu hiki pia kimefuta neno "Bodi" na badala yake sasa kuwa "Wakala" yaani *agency*. Vile vile, neno "chakula" kwa matumzi ya sheria hii limetafsiriwa kuwa ni kitu chochote ukiacha dawa, kipodozi ama tumbaku, yaani tumbaku sio chakula, kipodozi sio chakula na dawa sio chakula ambacho kitatumika kama chakula au kinywaji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na inajumuisha kitu chochote kitakachotumika katika kuzalisha au kutengeneza chakula. Naomba hii tafsiri tulijadiliana sana na kamati chakula kilichotafsiriwa hapo ni pamoja na vinywaji. Kwa hivyo, kama mtu anakunywa soda yake katika sheria hii ile soda ni chakula. Kipodozi kimetafsiriwa kama ni kitu chochote kitakachotumika kwa njia ya kupaka, kusugua, kumimina, kujifukiza, kujifukizia, kunyunyizia, *perfum* hiyo, kupulizia kwenye mwili au sehemu ya mwili wa binadamu moja kwa moja kwa lengo la aidha kusafisha, kupendezesha, kun'garisha, kuvutia, kubadilisha rangi, kuubadilisha muonekano halisi na inajumuisha kitu chochote kinachotumika kutengeneza kipodozi hicho pamoja na kemikali.

Sehemu ya Pili

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii inaeleza marekebisho ya vifungu mbali mbali vinavyoelezea uanzishwaji wa wakala wa chakula, dawa na vipodozi, uanzishwaji wa idara za wakala wa chakula, dawa na vipodozi yaani kutakuwa na idara sasa sio idara hizi zilizokuwepo, uteuzi wa mkurugenzi mtendaji wa wakala, uansihwaji wa bodi ya ushauri ya wakala pamoja na majukumu na kazi ya bodi hiyo ya ushauri.

Sehemu hii pia imeelezea uteuzi wa wachunguzi wa maabara ya wakala katika eneo la chakula, dawa na vipodozi. Makosa yanayohusu umiliki usiokuwa halali wa alama kama vile *label*, uwasilishwaji wa kesi zinazotokana na athari za dawa kutoka katika vituo vya afya vya serikali na vile binafsi, yaani mtu amekwenda ametumia dawa au ametumia mkorogo amebabuka ngozi nzima au sura nzima imebadilika, basi hii pia nayo itahudumiwa na sheria hii.

Uwezo wa wakala pia kutoza faini moja kwa moja kwa wale wote watakaokwenda kinyume na sheria hii *(compounding of offences).*

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii pia imeeleza adhabu zitakazotozwa kwa watendaji wa makosa, ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa za dawa sokoni, uwazi na ubadilishaji wa taarifa, ufuatiliaji, ufanisi na utekelezaji wa kazi za wakala.

Sehemu hii pia imeelezea udhibiti wa uuzwaji na ununuaji wa bidhaa kupitia kitandao bila ya kujali usalama na ubora wa bidhaa. Kuna wafanyabiashara wengi wamegundulika wananunua bidhaa hizi hasa *cosmetics* dawa zinazopendezesha kama ilivyoandikwa kwenye mswada huu unaopendekezwa kwamba hizi zinzonunuliwa kupitia mitandao wakati mwengine ubora wake unakuwa haujaangaliwa ama kiwanda chake hakijajulikana au wa kwenda kukaguliwa.

Udhibiti wa vyakula vya mifugo visivyokuwa salama kwa wanyama pia nalo limo. Tunaelewa hivi karibuni palikamatwa vyakula vya mifugo ambavyo kule Bara wenzetu waliingiza dawa ambazo zinasababisha mabadiliko katika mwili wa binadamu, yaani mwanamke kuota ndevu pamoja na walaji au wanyama hao. Uondoshwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango na bidhaa bandia katika soko. Ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa za dawa na ulinzi wa upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na bidhaa zinazosimamiwa na itakayoitwa *ZFBA (Zanzibar Food and Drugs Agency)* badala ya bodi.

Sehemu hii pia imeelezea ufutwaji wa baadhi ya vifungu vinavyoshughulikia masuala ya kodi, usajili wa waganga wa kienyeji, waganga wa tiba asilia na tiba mbadala. Nadhani wengi mtakuwa mnawajua wanakuwa maarufu sana hawa mara nyingi. Utengenezaji wa viwango na masuala ya dawa za kilimo *Agrochemicals*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maelezo ya hapo juu, maelezo haya mafupi kabisa wizara inaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili mswada huu na hatimaye tunaomba waukubali kuupitisha kwa ajili ya kuanzisha wakala huu mpya wa serikali utakaokuwa na nguvu zaidi juu ya kudhibiti bidhaa za chakula, dawa na vipodozi na vifaa tiba kwenda kuwatumikia wananchi wote pamoja na wale wananchi ambao Mhe. Jaku Hashim Ayouba amewataja asubuhi hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupitie mswada huu, waujadili na kuupitisha ipasavyo. Naomba sana kuwasilisha kwa heshima na taadhima. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja rasmi juu ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ili ujadiliwe na kuweza kupitishwa. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii naye aje asome hotuba yake.

Mhe. Ame Haji Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Naomba kuwasilisha maoni ya Kamati juu ya Marekebisho ya Mswada wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima wa afya ili tukaweza kukutana hapa na kufanya kazi hii muhimu ya kuwasilisha Marekebisho ya Mswada huu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa umakini imeupitia Mswada wa marekebisho ulioletwa mbele ya Baraza lako

tukufu kwa madhumuni ya kuimarisha sekta ya afya Zanzibar. Kimsingi, baada ya marekebisho machache, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaunga mkono hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila endapo sitowashukuru wadau ambao kamati yetu ilikutana nao kuujadili Mswada huu kwa undani na kutupatia maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisadia kamati kutoa mapendekezo muhimu katika marekebisho yanayoyafanywa.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la Mswada huu wa marekebisho ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mapendekezo ya Sheria ya Usimamizi wa Baadhi ya Tiba ya Umoja wa Afrika pamoja na mapendekezo ya Baraza la Kisekta la Sheria na masuala ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki linafanikiwa. Aidha, imekubalika kuwa kila nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika na Jumuiya za Afrika Mashariki inapaswa kuanzisha taasisi inayojitegemea, ili kusimamia utengenezaji na uingizaji wa bidhaa mbali mbali kwa umakini mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho yaliyofanywa katika Mswada huu yana lengo la kuimarisha Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi itakayokuwa na nguvu ya kusimamia vyema mfumo wa utoaji huduma za afya na ubora wa dawa za binaadamu na wanyama, pamoja na chakula kilicho salama kwa maisha yetu. Faida nyengine za marekebisho ya sheria hii ni pamoja na:

1. Kusimamia vyema uagizaji wa bidhaa za chakula zinazotoka nje ya nchi.
2. Kusimamia vyema uingizaji wa dawa za binaadamu na mifugo.
3. Kusimamia vyema matumizi ya vipodozi kwamba havitumiki vibaya kwa wananchi wetu na kuathiri afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Mswada huu, naomba sasa nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
4. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
5. Mhe. Massoud Abrahman Massoud - Mjumbe
6. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe

9. Ndg. Aziza Waziri Kheir - Katibu
10. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu sasa nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo yaliyofanywa na Kamati yetu. Aidha, naomba niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kuwa, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo zaidi ya marekebisho na mapendekezo hayo naomba muangalie katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari wameshapatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu namba 7 cha Mswada huu kilichoongezwa vifungu vipya vya 5A na 5B ambapo kifungu cha 5A kinahusiana na Kuanzishwa kwa Bodi, kamati ilijadiliana na wizara na kukubaliana kuwa kifungu hiki kirekebishwe katika kifungu kidogo cha 5A(1)(d) na maneno "Wizara inayohusika na Fedha" yaondoke na badala yake yasomeke "Wizara ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Mazingira". Marekebisho haya yamekubalika kutokana na umuhimu wa watu wa sekta zote zilizotajwa katika utekelezaji wa sheria hii. Aidha, sekta hizo zimetajwa kwa pamoja ili endapo wahusika hao wapo katika Wizara tofauti iwe ni rahisi kutambulika umuhimu wao na kwamba wote wanahitaji kuwemo katika sheria hii ili utekelezaji wake usigongane katika maamuzi ya kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia imependekeza katika kifungu cha 5(3) cha Mswada huu mwishoni mwa kifungu hiki yaongezwe maneno "na itazingatia jinsia". Kamati imependekeza hivyo ili kutotoa nafasi kwa Mhe. Waziri kufanya uteuzi ambao hautozingatia jinsia ambao utaathiri kwa namna moja ama nyengine utekelezaji wa sheria hii. Pia kamati inapendekeza hivyo kwa kuzingatia matakwa ya mikataba mbali mbali ya kimataifa ambayo inasisitiza suala zima la umuhimu wa ustawi wa jinsia katika mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 11 kamati imependekeza kifungu hichi kisomeke: "Mkurugenzi Mtendaji atapendekeza kwa Bodi na kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi la Serikali baada ya kuidhinishwa na Bodi, mtu mwenye sifa miongoni mwa wataalamu wa chakula, dawa, wafamasia, wataalamu wa elimu ya viumbe hai , mtaalamu wa teknolojia, mtaalamu wa maabara, mhandisi au mwenye taaluma yoyote inayolingana na hizo, kuwa Mchunguzi Mkuu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya sheria hii". Kamati imetoa mapendekezo haya ili kutotoa nafasi kwa Mkurugenzi Mtendaji kufanya upendeleo katika uteuzi wake na badala yake yeye apendekeze na bodi iidhinishe uteuzi uliofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia imependekeza marekebisho katika kifungu cha 17 ambapo kifungu hicho kinaongezewa maneno “kuzingatia miongozo ya kimazingira”. Kamati imetoa mapendekezo haya ili kutokana na umuhimu wa sekta ya mazingira katika utekelezaji wa sheria hii. Pamoja na kwamba wakala itakayoanzishwa itakua na wataalamu waliobobea katika uharibifu wa bidhaa za tiba, lakini ni muhimu wahusishwe watu wa mazingira ili na wao waelekeze uharibifu wa taka hizo kwa mujibu wa miongozo ya kimazingira ambayo haitoathiri mazingira na afya za wanaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa tunaiomba serikali kuyazingatia yale yote tuliyoyapendekezwa na kamati baada ya kupata ushauri mzuri wa wadau wa taasisi mbali mbali ambao kwa namna moja ama nyengine wamesaidia kutoa maoni yao ili kuifanya sheria hii itakapoanza kutumika iwe bora zaidi. Kufanya hivyo ni kuisaidia serikali na wakala husika inayoanzishwa kutengeneza misingi imara na ubora katika sekta ya afya kwa ajili ya vizazi vya sasa na vya baadae katika taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapenda kuishauri wizara kukipa meno chombo hiki ili kukitengea bajeti ya kutosha na kiweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wauchangie, waukosowe na waurekebishe mswada huu kwa kutoa mawazo yao yatakayoufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha ili usaidie kuleta ufanisi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu sasa kwa niaba ya kamati yangu natamka rasmi kwamba tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Nami binafsi kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Nungwi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa heshima na taadhima sasa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ame wa Jimbo la Nungwi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, na mimi pia niwapongeze kwa hotuba yenu. Sasa naomba niwaite wachangiaji wafuatao ambao wataanza kuchangia mswada huu. Kwanza naomba nimwite Mhe. Wanu Hafidh Ameir akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) ajitayarishe.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nikachangia machache katika mswada huu ulioletwa mbele yetu, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sheria Nam. 2 ya Mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhai kukutana hapa, lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipatia hii nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa muda mfupi kama alivyosema mwenyewe, lakini pili niipongeze Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na niseme naunga mkono marekebisho yale ambao kamati wameyaleta.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ushauri tu ingekuwa vyema kama kungekuwa kunaletwa *amendment* za jadweli ambalo wanakubaliana katika serikali ili tusiwe tunarudia mambo hayo hayo ambayo pengine wameshakubaliana halafu na sisi tunakuja hapa tunachangia hayo hayo. kwa hivyo, ni vyema serikali ingekuwa inaleta *schedule of amendment* ambayo wamekubaliana katika kamati ili kuepusha kurudia yale mambo ambayo tayari wameshakubaliana na kamati na badala yake tukawa tunarudia humo kwa humo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea mbele naomba nipongeze uongozi wa Baraza leo naona meza za mbele pamoja na kiti kumependeza kabisa wanawake, lakini pia nishukuru kwamba mmetuonesha kwamba wanawake tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba nianze na Sehemu ya Pili ya Marekebisho ambapo katika tafsiri ya Neno Bodi ya Ushauri wanasema kwamba Bodi ya Ushauri maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, *concerning* yangu ipo katika *reference* ambayo wameifanya katika kifungu cha 7. Ukiangalia kifungu cha 7 cha sheria hii hakianzishi bodi ya ushauri, badala yake kinaanzisha Wakala wa Chakula na Madawa. Kwa hivyo *reference* ya kifungu cha 7 cha sheria hii ningeomba ibadilike na badala yake isomeke kifungu 5A(i) ndicho ambacho kinaanzisha bodi ya ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, bado nipo katika tafsiri, ukiangalia neno "wakala" wanasema maana yake ni:

"Wakala" maana yake Wakala ya Kusimamia Chakula na Dawa ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii,"

Mimi nilikuwa naenda katika kifungu cha tafsiri ya Mkurugenzi Mtendaji. Ukiangalia maana ya Mkurugenzi Mtendaji inasema maana yake ni:

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria hii."

Pia ukiangalia *reference* ya kifungu cha 8, hiki hakianzishi Mkurugenzi Mtendaji, isipokuwa kifungu sahihi ambacho kinaelezea maana ya Mkurugenzi Mtendaji ni kifungu cha 6 cha sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niingie katika kifungu cha 5(a)(4) kinasema Bodi ya Ushauri itamteuwa mwanasheria na Wakala kuwa Katibu wa Bodi. Sasa ukisema itamteuwa Mwanasheria na Wakala ina maana bodi itateuwa Mwanasheria na itateuwa na wakala. Kwa hivyo kuweka maana sahihi ya kifungu hichi neno 'na' liwe neno 'wa'. Kwa hivyo lisomeke kwamba Bodi ya Ushauri itamteuwa Mwanasheria wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu kingine marekebisho ya 9 ambayo inarekebisha kifungu cha 7 cha sheria mama. Marekebisho haya Mhe. Mwenyekiti, yamefuta kifungu ambacho kinazungumzia *allowance* ya Bodi yaani malipo yale ambayo Bodi yatakayolipana. Ukiangalia kifungu hichi pamoja na kwamba kimefutwa lakini kina umuhimu wake. Umuhimu wake nilifikiria labda katika jaduweli la marekebisho ambalo linaleta mwenendo wa vikao vya Bodi ya Ushauri ni vyema kile kifungu kilichofutwa basi kikaingia katika jaduweli la mwenendo wa vikao vya Bodi ya Ushauri, kwa sababi ni lazima sisi tujue Bodi itaenda kulipana vipi na lazima sheria iweke utaratibu wa hizi Bodi kulipana kama zilivyo sheria nyengine katika utaratibu mzima wa mwenendo wa Bodi. Sasa kifungu kimefutwa na hakijawa *moved* kwenye jaduweli la marekebisho ya mwenendo wa Bodi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba pamoja na kwamba kifungu kile kimefutwa kina umuhimu wake, kwa sababu kinaelezea malipo ya bodi watakavyolipana yaani *source of fund.* Ni vizuri sheria ikaweka utaratibu ili watu wasende wakachukua pesa wakalipana ovyo ovyo. Pendekezo langu kwamba kifungu kile pamoja na kwamba kimefutwa kiingie kwenye jaduweli ya mwenendo wa vikao vya bodi, Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mwanasheria Mkuu ananisikia.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho yangu mengine yapo katika kifungu cha 15(a) ambapo hapa nakubaliana na marekebisho ya Kamati kwamba kifungu kinasema kwamba "Wakala itaanzisha mfumo wa usimamizi" na mimi nakubaliana nayo neno liwe itaanzisha kwa sababu katika Mswada wa Kizungu inasema kwamba Wakala "*may*" inaweza ikaanzisha lakini kamati pia ikaleta marekebisho kwamba iseme Wakala itaanzisha, kwa hivyo na mimi naungana mkono na Kamati lakini pia Mswada wa *English* kwa sababu hapa neno linalo-*appear* nitaanzisha kwa hivyo kule lisomeke "*shall*" na siyo "*may*" .

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 2 cha marekebisho kinasema kwamba Wakala itaweka mfumo utakaowezesha usimamizi wa utoaji wa habari ambao utawezesha ubadilishanaji wa habari za usimamizi wa bidhaa. Mimi naunga mkono na hili, lakini kuna baadhi ya tafsiri katika Mswada wa english umeachwa yaani kwenye kiswahili kuna maneno yameachwa wakati katika english iko *very clear and proper*. Kwa hivyo ningeomba sana kifungu cha 15(a)(2) kikaangaliwa tena na neno *regional information* ambalo limeachwa. Kwa sababu hapa imeandikwa tu "usimamizi wa utoaji wa habari" lakini kwenye *english* inasema *regional information* kwa hivyo neno *regional* limeachwa na mantiki yake inakubalika kabisa, hii inajumuisha kama Waziri alivyotuelezea lakini kama maelezo ya jana tulivyopata katika semina kwamba ni matakwa ya zile jumuia ya *East Africa* na *AU* na ndio maana nadhani wakaweka hichi kitu *regional information* kwa sababu ili tupate na zile taarifa za wenzetu ambapo tupo nao pamoja katika hizi jumuia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika usimamizi wa ubora katika kifungu cha 60(b) naipongeza serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuweka huu usimamizi bora wa madhara ambayo yatajitokeza. Lakini sasa wasiwasi wangu upo katika kifungu hichi kinachosema kwamba wakala inaweza kuanzisha mpango wa kupunguza madhara kwa kupima. Sasa mpango ni mzuri lakini Mswada unasema inaweza kuanzisha, kwa hivyo sio lazima unaweza kuanzisha au wanaweza wasianzishe.

Lakini mpango ambao wameuweka na hichi ni kifungu kipya nadhani mpango mzuri kwa hivyo ni vyema wakasema kwamba Wakala ianzishe ama itaanzisha badala ya kuweka inaweza kuanzisha, kama ni mpango mzuri wameuona halafu wanauleta na haukuwepo haina sababu ya kuweka inaweza kuanzisha wangeacha tu vile vile kama ilivyokuwa. Lakini kama ni mpango mzuri, wanaamini kwamba utaweka utaratibu mzuri wa kupunguza madhara, basi kifungu kisomeke kwamba "Wakala itaanzisha ili wakala ilazimike kuweka huu mpango wa kupunguza madhara". Kwa sababu madhara yapo na mengine

mengi yatajitokeza, kwa sababu dawa, vipodozi, vyakula ambavyo vimeshapitwa na wakati vinaingia na madhara haya yapo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 93(a) kinachozungumzia kuwa na alama ya dawa kinyume na sheria kinasema kwamba mtu anayehodhi alama ya dawa ambayo inadhaniwa kuwa siyo halali atakuwa ametenda kosa la jinai. Nilikuwa najiuliza kwamba kosa la jinai linakuwepo wakati panapokuwa na dhana, labda Mhe. Mwanasheria Mkuu aje anielezee. Kwamba hii ni dhana, kwa sababu sheria inasema alama ya dawa ambayo inadhaniwa kuwa siyo halali atakuwa ametenda kosa la jinai. Mimi nilifikiria kwamba ingesomeka "Mtu anayehodhi alama ya dawa ambayokuwa siyo halali atakuwa ametenda kosa la jinai kwa sababu dhana haiwezi kuwa kosa mpaka pale inapokuwa prooved, beyond without kwamba ni kosa kwa hivyo dhana haiwezi kuwa kosa. Mimi nilikuwa naomba hili neno "inadhaniwa" liondoke ili iwe kosa moja kwa moja kuwa na alama ambayo siyo halali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kifungu cha 22 kwenye *compounding and offence* yaani kumaliza kosa. Kwanza neno la kwanza kifungu cha 124(a)(1) neno "Kurugenzi Mtendaji" lisomeke Mkurugenzi Mtendaji kwa sababu katika Sheria hii hakuna kitu kama hicho Kurugenzi Mtendaji na katika tafsiri tumekuta Mkurugenzi Mtendaji. Pia nilikuwa naomba ufafanuzi kwa Waziri ama kwa Mwanasheria kwamba mnapo *compound* kwa kifungu hichi kilivyo hapa kinavyosema kwamba:

> "(a) Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukubali kumaliza kosa lililofanywa chini ya sheria hii au kanuni kwa kumuagiza mtu huyo kulipa faini iliyowekwa kwa kosa hilo, ikizingatiwa kwamba endapo mtu aliyefanya kosa amekubali kwa maandishi kwamba amefanya kosa na atachukua hatua za uangalifu ili asirudie kosa hilo.
>
> (b) Atalipa faini iliyowekwa na sheria hii au kanuni."

Sasa nilikuwa naona kama kifungu kinampa *power* Mkurugenzi Mtendaji moja kwa moja, yaani kinampa zile kazi za Mahakama za kutafsiri sheria, na kwa sababu imeelezwa kabisa kwamba atahukumu kwa mujibu wa sheria hii. Sasa hapa nataka kujua nani mwenye *power* ya kutafsiri hii sheria ni Mkurugenzi Mtendaji ama Mahakama.

Nafahamu kuna suala zima la kumaliza kosa lakini kumaliza kosa lisifanyike nje ya utaratibu nzima wa Mahakama kwamba Mkurugenzi yupo katika Ofisi mtu amefanya kosa kwa kuwa sheria inampa *power* kumaliza kosa anamaliza

kosa pale pale, *at least* awe anakiri pale kwa barua Mkurugenzi awe ana *proceed* na hatua nyengine na Mahakama kuliko kumpa *power* moja kwa moja ya kushtaki kesi katika mamlaka yake. Mimi ninavyoona kama misingi ya *separation of power* inakiukwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kifungu hichi hichi kifungu kidogo cha 2 kinasema kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha 1 cha kifungu hichi hakutakuwa na mashtaka ya jinai yatakayofunguliwa baadaye kwa kosa hilo dhidi ya mtu huyo. Yaani najaribu kujenga mashiko kwenye ile hoja yangu ya kwanza niliyosema kwamba inawezekana pia lile kosa likawa la jinai. Sasa kosa la jinai mnampa mtu akae kwenye ofisi alimalize pale pale. Mimi nafikiri hii haipo sawa itizamwe tena. Ndio kuna utaratibu wa kumaliza kosa lakini pia Mahakama kwa namna moja au nyengine iwe imeshirikishwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia inaonekana Mahakamani itakuwa ni *process* kubwa tuna Mahkama ya Biashara nakumbuka kama hivi tulianzisha sasa sijui kama bado ipo au inafanya kazi zake lakini mimi nadhani *power* hizi angenyang'anywa Mkurugenzi Mtendaji moja kwa moja kushtaki na Mahakama ikafanya kazi zake. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii na kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Sheria ya Chakula, Madawa na Vipodozi Nam. 2 ya Mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuona kwamba umefika wakati sasa hivi ni lazima turekebishe sheria zetu na kwenda sambamba na wakati tuliokuwa nao. Pili niishukuru Kamati ambayo nayo imekaa na kufanya marekebisho mazuri juu ya kuiweka vizuri sheria hii iwe rahisi kuitumia pindi kwa makosa yanayotokea katika watumiaji wanaohusika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze wizara kwa kuanzisha Bodi ya Ushauri ya Wakala kusimamia Chakula, Dawa…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Suleiman samahani kidogo, kuna taarifa kwamba Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora, Idara Maalum wanatakiwa kukutana katika chumba cha mkutano sasa hivi. Ahsanteni.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Kusimamia Chakula na Dawa ya Zanzibar hili ni suala muhimu hasa tukizingatia sasa hivi hali ya mabadiliko katika nchi au ulimwengu yamekithiri, udanganyifu unakuwa mwingi kuliko ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tumefikia wakati kwamba wananchi wengi wanakula bidhaa mbovu kwa mfano mchele, vitu vya makopo kama siagi, tomato, na mambo mengineyo. Naiomba bodi hii ifanye kazi zake ipasavyo. Nitatoa ushauri mwingi baadaye kuelezea jinsi ya usimamizi.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanaitegemea serikali yao kwa kila kinachoingia katika nchi yao ndio maana tukaweka milango ya kupitisha bidhaa halali, mfano Bandari na Uwanja wa ndege na kwengineko kama vimekuwa vimepitishwa kwa kupitisha bidhaa zile ili kumlinda mwananchi juu ya afya yake na usalama wake. Lakini tumeshuhudia hivi sasa katika nchi yetu mimi nazungumzia Zanzibar kwa asilimia 80 tunategemea chakula kutoka Tanzania Bara.

Naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthubutu na kuruhusu pamoja na matatizo yanayojitokeza kwa uhaba wa chakula baadhi ya maeneo kusema Zanzibar bado chakula kitoke Bara kije hapa na hawana pingamizi na hilo. Naishukuru Serikali yetu hiyo na huu ndio kuimarisha Muungano wetu wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, hii asilimia 20 iliyobakia tunategemea bidhaa kutoka nje ya nchi, hii inatuathiri kwa mambo. Mchele wa Mapembe tumeshuhudia kwa asilimia kubwa sana mchele wetu tunaoutegemea wa mapembe. Mchele huu huwa mara nyingi unapoingia katika nchi yetu unakuja vizuri baadaye nafikiri kwa utaalamu wa wafanyabiashara sisemi wote baadhi yao huwa wanaubadilisha mapolo wakiona kama *expire date* inakaribia wanaweka mapolo mapya ili kumbabaisha mtumiaji. Naiomba bodi inapoingia bidhaa hii ya chakula kutoka nje wawe waangalifu sana tarehe ya kuingia na tarehe ngapi za umaliziaji ili kunusuru afya za watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tumekumbwa na maradhi mengi na maradhi mengi tunayo ambayo sukari, saratani, *pressure* na mambo mengineyo, hii kwa asilimia kubwa za watafiti wanasema inatokana na chakula ambacho sio kizuri. Kwa hivyo niiombe sana Wizara, Bodi hii ipewe fursa kama ilivyoomba ifanye kazi zake kwa uangalifu na kuhakikisha kwamba kinachoingia hapa kinakuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi itakuwa na kazi ya kusimamia uingizwaji wa chakula chote kama nilivyosema itakuwa jukumu zuri au jukumu lake kubwa kuhakikisha kwamba salama kwanza kuliko mengineyo. Pili ni madawa, vipodozi, bodi hii itakuwa ndiyo inayohusika moja kwa moja katika kuhakikisha hivi vipodozi au madawa haya yapo salama. Nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia Bodi hii na kwa kuwa atakuwa na Mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi Mtendaji na Wajumbe ambao wanahusika na Wizara fulani ambao wanahusika vizuri tu kutokana na taaluma zao watusaidie sana kuokoa maisha ya watu wetu juu ya athari ambayo hatutegemei itokee katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Kitengo cha Chakula kitakuwa na jukumu kubwa sana kwa sababu hapa ndio mambo mengi yanapotokea na yanapofichwa fichwa, kwa hivyo wenzetu wapewe fursa ya ukaguzi, wawe na uwezo wa kusimamia, wawe na uwezo wa kuingiza na kurejesha. Maana yake nini? Bidhaa hii ikionekana ipo sahihi iingizwe lakini sio bidhaa inatoka mapakti zaidi ya laki tano au milioni moja yanaingizwa nchini umebakia mwezi mmoja tu, hayo yasiruhusiwe kuingia katika nchi yetu. Kwa sababu haya ndiyo yanakuja kubadilishwa yale ma-*packet* linawekwa polo jipya unaona linang'ara tu kumbe limeshamaliza muda wake. Naiomba sana serikali kwa kupitia bodi yetu hii ifanye kazi yake bila ya kumjali huyu nani, na kumuogopa huyu nani, kwa sababu wanafanyakazi ya kuokoa maisha ya watu wetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hawa wasafirishaji wanaoingiza mali, hawa lazima waangaliwe kwa sababu wao wenyewe watakuwa ndio wasababishaji wa mwanzo kutokana na bidhaa zao zinapoingia, wanajua bidhaa hii ni muda mfupi inamaliza wao wanaileta, basi wachukuliwe hatua kali ili kuliondoa tatizo hili katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la usimamizi ni gumu na ni kubwa sana katika nchi yetu. Kuna mahoteli na mikahawa, hii inataka kukaguliwa kila leo au kila mara ili kuhakikisha kwamba usafi na hali halisi iko vizuri juu ya huduma wanazotoa kwa ajili ya wananchi wetu, ili wapate huduma zinazokidhi haja.

Pia niseme kwamba *bakery* zetu Mhe. Mwenyekiti, ma-*bakery* ni sehemu moja wapo kunakozalishwa mali ya kila siku ambao wananchi wetu wanahitaji mikate, na mikate ni chakula kikubwa kwa Zanzibar hii, unaanzia mjini mpaka vijijini. Kwa hivyo, nayo iangaliwe ubora wake ili kuiweka bidhaa ile salama kwa ajili ya utumiaji kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jengine kubwa, bidhaa ya chakula ina mambo mengi. Kuna sehemu ya uchinjwaji wa ng'ombe, hasa *butcher* za nchi yetu. Zamani kulikuwa na butcher ambazo zinategemewa zimewekewa sehemu maalum.

Kwa mfano, Zanzibar mimi nakumbuka kule Kisakasaka, ilikuwa ng'ombe wa Zanzibar wote asilimia kama 80 ya nchi yetu, wanachinjwa Kisakasaka na wanasambazwa sehemu mbali mbali. Ng'ombe yule akishakuchinjwa, basi daktari muhusika anampiga muhuri na kitoweo kile kinatumika bila ya matatizo, lakini leo hakuna. Mwenyezi Mungu atuepushe mbali, sasa hivi machinjio yamekuwa mengi. Unakuta uwanja wa mpira ng'ombe kaibiwa keshachinjwa, hajulikani katokea wapi wala hajulikani usalama wake, basi anachinjwa na kwenda kuuzwa ng'ombe hatujui alikuwa na maradhi gani, ndio hayo yanawakuta watu mbali mbali kutokana na ukweli haupo.

Kwa hivyo, mimi niiombe wizara, lakini hii ni kwa kupitia kwa masheha wetu, lakini kupitia na kwa wananchi wetu wema bodi ifanye kazi zake kuwaelimisha wananchi juu ya athari ya ng'ombe, au wao wenyewe wawe na utaratibu wa ukaguzi, ambapo nasema tena itakuwa sio jambo rahisi. Kwa sababu Unguja na Pemba, mjini na vijijini ni sehemu kubwa. Leo machinjio haya, mimi nayaita machinjio haramu, maana hayakuhalalishwa yamekuwa mengi katika nchi yetu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri ana kazi nzito kwa kupitia bodi hii kufanyakazi zake kwa ufasaha.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni ghala zetu. Ghala lazima zikaguliwe ili zijulikane. Kila chakula kina miko yake. Chakula fulani kinafaa kukaa pahala fulani na chakula fulani hakifai kukaa pahala fulani. Kwa hivyo, hivi itakuwa ni njia nzuri sana, ghala zetu yaani store zetu ziwe ziko katika mazingira mazuri, juu ya kuhakikisha kwamba tunakuwa salama na chakula tunachokitumia sisi na wanachi wetu kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, vipodozi ni suala ambalo limeenea katika nchi yetu, na vipodozi huwezi kuvizuwia. Lakini narudia tena bado viangaliwe ubora wake na ukweli wake. Kwa sababu mara nyingi kuna mihuri ya bandia. Utakuta *expire date* inadanganya hivi kumbe kitu hicho kimeshaharibika miaka miwili nyuma au miaka mitatu nyuma. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wenzetu wawe wataalamu wa kufuatilia, wawe na muda mzuri wa kufanya kazi zao, hasa tukizingatia kwamba kazi hizi niomuombe sana Mhe. Waziri wizara zinazohusika zifanye kazi kwa pamoja ili tupate faida hii.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, ukitaka bodi hii ifanye kazi zake, basi wizara zinazohusika kama Wizara ya Biashara, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo

na Uvuvi, Mkemia Mkuu anahusika, *ZBS* yaani ofisi inayohusika na kuweka viwango inahusika, pia taasisi ya mtumiaji inahusika ili kazi zao ziende sambamba katika kuleta usalama kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa dhati kabisa, hili suala tulilokuwanalo katika nchi yetu bidhaa mbovu, vipodozi havifai, sijui madawa mabovu yamo mengi katika nchi yetu. Ndio maana Bodi hii itakuwa na kazi ya kuviharibu vitu vile ambavyo vinaingizwa katika nchi yetu ambapo muda wake umekaribia au umekwisha kabisa na kuhatarisha usalama wetu. Kwa hivyo, niiombe serikali Mhe. Mwenyekiti, kwa hili tusiregeze kamba tuwe waangalifu katika kuokoa maisha ya watu wetu.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba mimi naiomba wizara kwa kupitia sheria yetu hii, baraka zote wapewe na wafanye kazi zao ipasavyo, ili kuhakikisha kwamba lengo la serikali yetu kuweka mazingira salama ya afya za wananchi wetu, kuanzia chakula dawa za binadamu, pamoja na vipodozi, lakini usimamizi uwe mwanzo ili kuleta mafanikio kwa jamii yetu inayotutegemea kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele naunga mkono mswada huu, na nawaomba na wajumbe wenzangu waichangie na waiunge mkono, ili tuwape uwezo bodi ifanye kazi zake kwa usalama na kwa maisha ya wananchi wetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) wa Jimbo la Kijitoupele kwa mchango wako. Sasa namuomba Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo), akifuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi. Kama muda utaturuhusu Mhe. Asha Abdalla Mussa na yeye ajitayarishe.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mswada huu wa marekebisho ya chakula, dawa na vipodozi Sheria Namba 2 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuanza niipongeze wizara husika kwa kushirikiana na bodi kwa kutuletea mswada huu wenye faida na manufaa kwetu na kwa vizazi vyetu kwa jumla. Vile vile naipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao na marekebisho yao ambayo waliwasilisha kwetu, na wao wenyewe ambao waliyaona na wakaweza kuyafafanua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na kifungu cha 5(a)(1) kuhusu muundo wa bodi. Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na bodi husika imeona ni jinsi gani ambavyo wamejiandaa kupunguza hawa wajumbe, ili kuona kwamba hili suala linaweza kusimamiwa ipasavyo.

Lakini mimi hapa nina ushauri Mhe. Mwenyekiti, wa kuhusiana na hawa wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa na linahitaji mashirikiano ili tufikie pale ambapo tumekusudia. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kwamba kuna baadhi ya bandari bubu ambazo zimeibuka katika maeneo yetu. Kuna watu wanapitisha vyakula ambavyo havijafanyiwa uchunguzi. Wakati mwengine vyakula vile vinasafirishwa kwa majahazi vinatoka katika sehemu husika, vyakula vile vinakuja ndani ya nchi na wanunuzi ambao wanafanyabiashara wa maduka madogo madogo wanakwenda kununua bidhaa zile. Jambo ambalo siku nyengine katika usafirishaji wa bidhaa zile, pengine zimeingia maji chumvi na mtu akishafika nayo bidhaa yake hata kama imeingia maji chumvi, anasema aah! mimi siwezi kuitupa bidhaa hii, ina maana anaibadilisha polo.

Tuangalie pengine mchele umeingia maji chumvi, baada ya kuingia maji basi ubora wake umeshaondoka. Lakini atakayebadilisha polo auanike baadae watu wanakwenda kutumia, badala ya kuwa wanakula vitu ambavyo vinawaletea faida ndani ya mwili, sasa wanaanza kuingiza maradhi katika mwili. Kwa hivyo, huu ushauri wa kuunda hii bodi ambao umepunguzwa, mimi nashauri kwamba hebu tuige wale wenzetu ambao wameunda mambo ya askari jamii katika mashehia na wilaya, ili kupunguza kasi ya maambukizo ya madawa ya kulevya.

Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba hii bodi iandae au iendelee kuunda baadhi ya wajumbe ambao watakuwemo kwenye mashehia kuweza kusimamia hivi vyakula vinapoingia katika maeneo yetu, hususan kule kwenye maduka. Kwa hivyo, wataweza kusema kwamba aah! katika sehemu fulani kumeshuka mzigo na tulipokwenda kuuangalia mzigo huu hauna kiwango na uko hivi. Kwa sababu wakati mwengine tuangalieni jamani, wafanya biashara siku zote wao wanataka faida yao iwe kubwa. Kwa hivyo, wanaweza kwenda kuchukua kitu mfano Tanga au sehemu nyengine akapitisha kwa njia anayojua yeye, kumbe kitu kile kilikuwa kishafika katika hali ya ku-*expire*, anakuja nacho anakiteremsha bei na wananchi katika majimbo yetu tunaangalia jinsi gani ambavyo anaangalia kadhia ya maisha.

Mtu ana watoto ndani ya nyumba hawapungui saba au nane, anaona bora nikanunuwe bidhaa ile ambayo pengine inauzwa kwa kilo shilingi 800 au 700

ili nipate kula, kumbe hajui yeye kushushwa kwa bei ile ni kile kitu kwamba hakina ubora, lakini watu watakwenda kununua na kuanza kutumia. Kwa hivyo, nashauri hapa huu muundo wa hii bodi iongezwe na watendaji wengine ambao watasimamia katika shehia ili kuona kwamba hii hali tunapambana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye upande wa dawa. Mhe. Mwenyekiti, kama mazungumzo yangu ya mwanzo nilivyosema kwamba ni vyema kuwaweka hawa wajumbe ambao wanakuwemo katika shehia. Mimi nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, nadhani utakubaliana na mimi, kwenye viduka vyetu ambavyo tunavyo hivi hivi.

Nataka nikuambie kwamba hapo zamani nilipofikia miaka karibu 17, labda niwe na homa ile kubwa sana ndio mzazi wangu anaweza kunichukua na kunipeleka hospitali, huo ndio ukweli. Hili lipo katika sehemu zetu za vijijini. Kuna watu hospitali au *pharmacy* hawaijui mpaka labda maradhi yale yawazidi ndio waende wakalazwe hospitali. Mara nyingi mtu anaambiwa akachukuwe mchele, lakini hebu mwambie na mwenye duka akupe panadol 2 pamoja na action. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna dawa ambazo zimeingia. Sikusudii kutilia fitina kwa wale ambao wanauza zile dawa kwa kutoa huduma, lakini huu ndio ukweli. Kuna makopo ya dawa ndani ya maduka yetu ya vyakula yapo, watu wanauziwa hizi dawa, hazijulikani muda gani zina-*expire*, kile cha kuchotea kijiko hicho hicho kinafungiwa majani ya chai, hicho hicho na tangawizi, hicho hicho kinachotewa dawa.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Mwenyekiti, hii bodi ikaliona hili, la kuwaweka hawa watendaji waliomo kwenye mashehia pamoja na wilaya nyengine, ili kuongeza hii hali ya udhibiti wa haya masuala ya madawa pamoja na vyakula.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia nije kwenye upande wa vipodozi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba suala la vipodozi ni kweli ni biashara na ni vitu ambavyo wakati mwengine tunatoka katika ulimwengu uliokuwa wa zamani na sasa hivi tunaingia kwenye sayansi na teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, wimbi hili la utumiaji wa hivi vipodozi mara nyingi vinaonekana vikitumika katika maeneo ya mjini. Huko mashamba wazazi wetu mtoto mtu anaweza akamzaa akamkosha basi hata mafuta hampaki, lakini humu matumizi ya vipodozi kwa wenzetu wa kike yamekuwa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukapishana na dada hapo njiani amekaa kama kipepeo, jicho moja ana rangi saba hujui kama ni kipodozi gani labda angeanza nacho akajua mimi hiki kinanifaa au hakinifai. Baada ya siku mbili Mhe. Mwenyekiti, unamkuta mtu yule hata sura zake zimebadilika. Kwa hivyo, naiomba sana wizara isimamie hili. Kwa sababu hebu tuangalieni suala hili la madawa ya kulevya, tunasimamia kuondosha kadhia ambayo inawafanya vijana wetu waharibike. Sasa na hawa kama hatukusimamia basi wataendelea kutumia haya marangi baada ya kujipaka jicho moja rangi saba watachukua na mwilini wajipake nane, ilimradi mtu akikupitia kakaa kama popobawa humjui kama ni binadamu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba wizara iendelee kuliangalia hili kwamba vijana wetu wanaharibika. Baada ya suala hili kuna msemo mmoja wa Kiswahili unasema, "tumbili akisha miti aja mwilini". Kwa hivyo, ina maana wakimaliza huku mjini basi na huko vijijini watafika. Sasa itakuwa kuna baadhi ya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba vile vile kwamba bodi iangalie wale watu ambao wanaingiza haya mambo ya vipodozi, kuwe na utaratibu maalum wa ufanyaji wa hizi biashara. Watowe labda kanuni na taratibu zao kama mtu aliyekuwa anataka kufanya biashara basi apite kwao kwanza aende akachukuwe kibali maalum, kwa ajili ya kuwa akirudi kama ni risiti basi arejeshe pale kwamba mimi nimerudi na nimefanya hivi. Ni kheri ya hivyo Mhe. Mwenyekiti, watu wataendelea kufanya biashara hizi ambazo sio nzuri na zitapelekea watu wetu ambao wanatumia kuweza kupata matatizo yasiyotarajiwa.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda niwaasi ndugu zangu wa kike ambao wanatumia hivi vipodozi. Wao wanaona wameletewa mambo kwa ajili ya kujipamba kumbe wanajiharibu, badala ya kuwa mtu abakie na asili yake ile aliyokuwanayo ya rangi yake, basi anakwenda kujiongeza marangi ambayo hata siyo, baada ya siku mbili mtu yule alikuwa mweusi anaanza kuwa kama Mwarabu na hali alikuwa mweusi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kukemea na kukazia kwa msisitizo juu ya masuala mazuri ya utumiaji wa dawa. Ni shahidi kwamba siku ya kulifungua jengo la mama wajawazito pamoja na watoto pale Mnazi Mmoja, aliiagiza wizara pamoja na hawa watendaji wa bodi, kwamba ipite kwenye *pharmacy* na maduka mengine makubwa ya dawa, ili kuhakikisha kwamba zile dawa ambazo zinauzwa, kwanza bei yao haibadiliki, kama ni shilingi 500 ibaki 500,

sio asubuhi 500 jioni 1000. Lakini vile vile kuangalia ubora na matumizi ya ile hali halisi ya haya madawa.

Kwa hivyo, hili agizo lilitoka, nadhani sina uhakika kama bado linaendelea kufanikisha hivyo, lakini tu kwa uchunguzi wangu Mhe. Mwenyekiti, ambao nauona kidogo kwa kupitia jimboni kwangu na kwa baadhi ya sehemu husika, sijaona hata mtu mmoja kupita labda kwenye vile viduka vyetu vidogo vidogo baadhi ya mambo akaangalia na nikaona labda kuna mtu labda katiwa korokoroni mpaka leo, sijui hili agizo lilitoka. Sasa sijui wizara kama wamelifumbia macho au baada ya kwishachukua yale maagizo na kutolewa imekuwa wimbo wa taifa. Mhe. Mwenyekiti, naomba tumuunge mkono Rais wetu wa Zanzibar, ili kukemea haya mambo ambayo yanajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, michango ipo mingi na wenzangu vile vile wanataka wachangie. Mimi niliyojiandaa ni hayo kwa sasa ambayo nimeliona. Kwa hivyo, naunga mkono hoja na vile vile Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wenzangu tuendelee kuuchangia mswada huu ambao ni mkubwa. Kwa sababu huu unalenga moja kwa moja kwa watumiaji ambao ni sisi pamoja na wananchi wetu ambao wako katika majimbo yetu, na hususan tuwaangalie wananchi wetu ni masikini. Kwa hivyo, lazima tuangalie vile vyakula na madawa na jinsi gani ambavyo vina ubora. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni, akifuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu uhusianao na chakula, dawa na vipodozi. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya kwa kuweza kuwasilisha mswada huu kwa wakati muafaka, lakini pia na uwasilishaji wake.

Vile vile niwapongeze wafanyakazi wa wizara na watendaji wote wa wizara ya afya, kwa kuweza kumsaidia wazi katika kufanikisha kuuleta mswada huu. Niwapongeze vile vile Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na hususan mwasilishaji, Mhe. Ame Haji Ali Mwakilishi makini wa Jimbo la Nungwi.

Lakini pia niwapongeze wachangiaji wenzangu ambao wamenitangulia. Mhe. Mwenyekiti, michango yangu sio mirefu sana. Nianze moja kwa moja katika ukurasa wa 208 katika ufafanuzi wa maneno. Napendekeza katika ufafanuzi wa

maneno, neno "virutubisho" ambalo limetumika sana katika mswada huu, na virutubisho ni neno ambalo hivi sasa lina mapana yake. Kuna virutubisho vya mazao, kuna virutubisho vya mifugo, lakini kuna virutubisho hata vya miili ya wanadamu. Kwa hivyo, hili neno naomba litolewe ufafanuzi ili tunapoliona katika mswada huu tujuwe virutubisho ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 210 katika kifungu cha 5(a)(2) ambacho kinasomeka;

Kifungu cha 5(a)(2)

> "Mtu hatoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi isipokuwa mtu huyo awe na elimu na uzoefu usiopungua miaka". Wasiwasi wangu uko kwenye neno "bodi".
>
> Kwa sababu kwenye ufafanuzi wa maneno hakuna neno "bodi" iliyoko kwenye ufafanuzi wa maneno kuna bodi ya ushauri kwa hivyo hapa unapoisema bodi maana yake unaleta utata kwa sababu hilo neno huku haliko na tayari tumefuta bodi, kwa hivyo ningependa lisomeke bodi ya ushauri ambazo ndilo lipo katika ufafanuzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti vile vile nije katika ukurasa wa 211 katika kifungu cha 6 kinachozungumzia suala zima la uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Hapa kidogo kuna mashaka kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji hapa inasema Mkurugenzi Mkuu sasa ningependa kuwe na marekebisho, iwe uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na sio Mkurugenzi Mkuu kwa sababu kifungu kimemtaja Mkurugenzi Mtendaji.

Lakini vile vile kwenye sifa hapo za Mkurugenzi mtendaji isomeke Mzanzibari, lakini nikija kwenye kifungu kinasema:

"(c) awe na uzoefu wa kazi angalau kwa kipindi cha miaka saba".

Nilikuwa napendekeza kwamba isemwe hasa katika fani inayohusika kwa sababu inawezekana ana uzoefu wa miaka saba lakini kumbe katika miaka yake hiyo saba kuna miaka alifanyia katika fani nyengine, kwa hivyo ikisomeka katika fani inayohusika ambazo zimetajwa hapo itakuwa imekaa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti nije ukurasa wa 212 katika kifungu cha 13 hilo neno Bodi vile vile kama nilivyosema kule nyuma lisomeke Bodi ya Ushauri, ambapo

inasemwa Mkurugenzi Mtendaji anaweza baada ya kushauriana na bodi isomeke bodi ya ushauri.

Lakini suala la kifungu 13(A)(2) hapo imezungumziwa juu ya mchunguzi ambayo inasema:

> "13A (2) Mtu hatokuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mchunguzi chini ya kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki, ikiwa mtu huyo atakuwa na maslahi katika bidhaa za tiba …" kifungu kinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitoe wasiwasi wangu kidogo kwamba tunaweza tukamteua mtu akawa tayari ana vigezo vyote vya sifa na kwa wakati ule anaonekana hana maslahi yoyote katika bidhaa za tiba, lakini uzoefu unaonyesha kwamba watu wengi baada ya kuteuliwa hapo ndio wanaanza kutafuta maslahi, anaweza kutafuta sasa kuwa na mbia katika maduka ya madawa au vyenginevyo. Sasa nafikiria kwamba tuangalie kifungu cha kuweza kumbana mtu huyu atakapokuja kuingia kwenye maslahi wakati tumeshampa wadhifa huu, iwe kuna hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuchukuliwa dhidi yake. Kwa sababu tumemteua hana maslahi lakini baada ya kumpa wazifa yeye ndio akayatafuta maslahi na mifano iko hai.

Mhe. Mwenyekiti tukitoka hapo napenda sasa nije katika ukurasa wa 215 katika kifungu cha 124A kinachozungumzia Mkurugenzi, kwanza wenzetu wamesahihisha hiyo ilikuwa kurugenzi iwe Mkurugenzi, lakini inaeleza vile kwamba Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukubali kumaliza hapa kuna tatizo vile vile kumaliza kosa isomeke lililofanywa chini ya sheria au kanuni, marekebisho yafanyike hapo.

Lakini sasa kwa nini kuwe na sheria au kanuni mimi nafikiria ingeangalia mojawapo kama humu sheria zimetaja basi iwe katika sheria, na kama kwenye sheria haikutajwa basi iwe kwenye kanuni ambako ndiko pengine tutaweza kuona kitu hichi. Lakini kuweka vitu viwili sambamba kidogo sijui Mwanasheria anaweza kuja kuweka mantiki kwa nini vitu hivyo viwili vikawepo sambamba ili kuweza kuondosha utata.

Lakini chengine katika kifungu hicho hicho ni uwezo aliopewa huyu Mkurugenzi huu uwezo ni mkubwa, uwezo wa kuweza kumaliza kosa. Ningependa sana uwezo huu apunguziwe Mkurugenzi kwa sababu unaweza ukampelekea uwezo huu akaja akatumia kwa maslahi yake binafsi, au akaja akashawishika na vitendo vya rushwa na baadae anaweza akafuta kosa wakati kosa lile ilikuwa pengine linaweza kuleta madhara kwa nchi na hata kwa raia.

Kwa sababu masuala haya ya madawa na vipodozi kwa kweli ni tatizo sana pale ambapo yatakuwa yanatumika visivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 216 kifungu kinachozungumzia maamuzi ya bodi kifungu No.3 kidogo penye namba tatu, tamko la maandishi lisomeke hivyo lililowekwa saini na Wajumbe waliopo Zanzibar lakini wasipungue *statement* inaendelea, nilikuwa naulizia tu hapa kwa Mhe. Waziri kwamba hapa kuna wajumbe ambao wanatoka nje ya Zanzibar. Kwa sababu kama Wajumbe wote ni wa Zanzibar nafikiri hakuna ulazima kusema waliopo Zanzibar iwe inaweka tu kuweza kuondosha utata, kwa sababu tuna wasiwasi pengine kuna wajumbe labda wanatoka nje ya Zanzibar.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti niangalie kwenye suala la ukurasa 217 kwenye madhumuni na sababu katika mstari wa pili kutoka chini kabisa mwisho neno la nne lisomeke 'ubora' na sivyo lilivyo na naogopa kulitamka Mhe. Mwenyekiti lisomeke ubora sasa tulitizame limekaa vipi.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia na niwaombe na wenzangu wachangiaji basi kuweza kuupitisha mswada huu bila ya wasi wasi wowote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia mswada huu, kwa kuwa nimepata mafunzo na ufafanuzi wa kina kupitia Wizara ya Afya katika semina iliyofanyika *Z OCEAN* Kihinani, kwa hiyo sitokuwa na michango mingi.

Mhe. Mwenyekiti, kanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara kwa kuona mapungufu yaliyopo katika Sheria hii ya Na.2 ya mwaka 2006 ya Sheria ya Chakula Dawa pamoja na Vipodozi na badala yake niunge mkono kamati kwa kazi ngumu na kutoa mapendekezo yao katika mswada huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi pia katika mswada huu nimekifurahia sana kifungu cha 3(1) ambacho kinazungumzia kuanzishwa kwa wakala wa Chakula, madawa na vipodozi, naamini kuwa kifungu hichi kitatekeleza mambo mengi na ambayo yanaweza kuhakikisha kwamba madawa chakula pamoja na vipodozi vinavyoingizwa hapa Zanzibar vinakuwa bora zaidi. Kwa kuwa kumeanzishwa wakala wa chakula, madawa pamoja na vipodozi nashauri kwamba ufanyike utafiti wa kina kwa maeneo ambayo yasiyo rasmi

yanayoingiza madawa, vyakula pamoja na vipodozi kwani maaneo haya yanasababisha uingizwaji wa madawa au vyakula visivyo bora.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia badala ya kuhakikisha kwamba yameonekana ama yamethibitishwa maeneo ambayo si rasmi naomba itafutwe njia mbadala ya kudhibiti maeneo hayo. Pia nimekifurahia sana kifungu cha 73(a) ambacho kinazungumzia vituo vya afya vya Serikali pamoja na binafsi ambavyo vitatoa taarifa kwa wakala kuhusu madhara ya madawa ya hatari. Kifungu hichi kitaweza kutupunguzia madhara dhidi ya watumiaji ambao wanaathirika zaidi madawa haya ambayo ni tiba kwa binaadam.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka kuomba ufafanuzi utolewe haya ni madawa ambayo wataweza kutumia wakipatwa na madhara wanaweza kutoa taarifa kwa wakala, lakini je wananchi wetu watakapotumia vyakula ambavyo vitawaletea madhara, wananchi hawa waende wakatoe taarifa sehemu gani? Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho basi atupe maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kuna baadhi ya vyakula vinavyoingizwa hapa Zanzibar vinavyotoka nje vinaleta madhara kwa wananchi wetu ikiwemo hawa kuku ambao wanaingizwa hapa maarufu wanaitwa kuku wa *PEDUU.* Mhe. Mwenyekiti, hapo mwanzo tulikuwa tunatumia kuku ambao wa kienyeji ambao wanafugwa hapa Zanzibar na kulikuwa hakuna madhara yoyote. Lakini kwa sasa limeibuka wimbi kubwa la bidhaa hizi na maduka mengi ya kuku hawa wa *PEDUU* na kwa sasa wananchi wanasema kwamba hawana tija kwa afya zetu. Napendekeza kwamba kuwepo na udhibiti wa bidhaa ambazo hazina uhakika kwa afya za binaadam ili wananchi wetu wa hapa Zanzibar waweze kutengeneza bidhaa ambazo zilizokuwa bora.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba sheria zipo, mapungufu yapo, lakini na kila baada ya muda tunafanya marekebisho tunaletewa hapa Barazani tunafanya marekebisho ya sheria mbali mbali. Lakini kama utekelezaji wake hautokuwa wa uhakika basi kila siku tutakuja hapa kufanya marekebisho na madhara yanazidi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, niseme niwashukuru sana waandaaji wa huu mswada, lakini pia niwapongeze wale wote waliochangia mswada huu na mimi naungana mkono na wenzangu kwa kuupitisha mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya mwaka 2006. Mimi moja kwa moja niende tu katika mswada huu bila ya kupoteza dakika maana nina vitu vingi kidogo.

Kifungu cha 5A(1) mimi naomba hapa pia nikubaliane na marekebisho ya Kamati yaliyofanywa katika kifungu cha kirumi (ii) yasomeke kama vile ambavyo Kamati imesema hapa niwapongeze kamati.

Lakini niondoke hapo niende kifungu cha 4 ambacho kinaelezea bodi ya ushauri itateua mwanasheria wa Wakala kama marekebisho alivyosema Mhe. Wanu kama atakuwa ni sahihi wakala kuwa katibu wa bodi hiyo. Nikiangalia hii kuendelea kuwepo hapa sababu ni sehemu ya majukumu ya bodi naomba tuihamishe hapa ihamie katika kifungu cha Namba 5B(1) ambapo kunaoneshwa uwezo na wajibu wa bodi, sasa hii ni kazi ya kuteua na hapa zimeoneshwa kazi za bodi ikiwemo ile kushauri basi iondoke hapa na tukihamishie tu kiingie katika 5B ili kuainisha vizuri yale majukumu ya bodi kama ambavyo yametajwa katika kifungu cha 5B bila ya marekebisho kama kilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika hicho kifungu cha uwezo na wajibu wa bodi, katika tafsiri hii ya uwezo na wajibu wa bodi mimi kidogo kwa kuweka sawa zaidi naomba kisomeke kazi za bodi ya ushauri 5B(1). Lakini pia tafsiri iliyokuwepo pale ya kuwa bodi itakuwa na uwezo wa kushauri katika utendaji nilikuwa nasema kama tutakubaliana kuweka kifungu hiki kuwa kisomeke kwa kazi za bodi ya ushauri basi na maelezo pia yabadilike na yasomeke kama mapendekezo yangu ambayo nayasoma. Bodi ya ushauri katika kutekeleza kazi zake itakuwa na uwezo na wajibu kama ifutavyo, ikesha mtiririko uende tu kama kawaida walivyoupanga lakini pia kuna kazi mbele huku imetajwa ya kumchagua Makamo Mwenyekiti hatukuianisha, kwa bodi hii miongoni mwa kazi zake basi ziainishwe hapa kuwa itakuwa na uwezo wa kumchagua Makamo Mwenyekiti na tuihamishe kule ambako tumeiwekea na haikutulia vizuri.

Lakini jukumu jengine ambalo ningeomba sana kwa sababu tulipoangalia sehemu ya maaelezo haya mengi ni kushauri na chombo hichi ndio kitakachomsimamia wakala. Walaka kuna siku atavunja sheria kwa sababu na yeye ni binaadam sio kila siku atatekeleza sheria haikuonyeshwa hii bodi kama ina uwezo wa kuyafuta yale ya wakala ambayo kayafanya kinyume na sheria. Sasa lazima bodi tuipe mamlaka hayo tusiwe tunaanzisha chombo ambacho kitakuwa kunatekeleza ushauri tu.

Sasa ningependa Mhe. Waziri atakapokuja kwa sababu ya kutengeneza mamlaka ya chombo hichi kwa sababu hii bodi narejea tena isiwe bodi ya ushauri tu itakuwa kazi yake kushauri tu, lakini kuna siku huyu Mkurugenzi wa wakala anaweza kwenda kinyume na sheria tulizozitunga nani atafuta maamuzi yale. Sasa hapa Mhe. Waziri atakapokuja anijibu nani atafuta, lakini kwa mswada huu naomba tu tuongeze kifungu kuwa bodi itafuta maamuzi ya wakala pale ambapo atafanya maamuzi kinyume na sheria iliyopo, ili kuonekana hii bodi inamsimamia vizuri huyu Wakala.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningeona liingie katika kazi za Bodi itafanya maamuzi ya kuanzisha Kamati na Idara za Wakala. Nayasema haya kwa sababu leo hii tumeletewa mfumo wa Idara zipo hapa lakini kuna siku wanaweza kuongeza idara zaidi ya hizi zilizokuwepo hapa kwa hivyo tutakuwa hatuwezi kurudi Barazani. Angalau Bodi kwa yale mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji basi iwe na uwezo pia ya kuruhusu zile Kamati zinazoundwa maana ndani huku tutaona Kamati zile kwa ujumla wake tumemuachia tu Mkurugenzi Mtendaji ataandaa Kamati za Wataalamu.

Sasa Kamati anaweza kaziandaa lakini zikawa zina-*deal* na maslahi ya kwake haziendi na maslahi ya nchi. Lazima tufike pahali na yeye tum-*limit* siyo afike pahala tunampa madaraka yote, hakuna utaratibu wa sheria ambayo inampendelea mtu ndani ya nchi hii. Sasa lazima kuwe kuna taasisi iwe inakwenda kumsimamia.

Nilikuwa napendekeza tu kuwa Bodi hii itafanya maamuzi ya uwanzishwaji wa Idara na Kamati ambapo Mkurugenzi Mtendaji pale ambapo atataka kufanya maamuzi yale. Mhe. Waziri sasa hili katika utaratibu wapo utakaokuja lazima ulipokee vyenginevyo itakuwa Mkurugenzi Mtendaji hapa tumempa mamlaka ambayo anaweza akatusababishia matumizi ya uanzishwaji wa Kamati na matumizi ya pesa ambayo siyo ya lazima kwa serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna kifungu cha 6(1) kinazungumzia kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais, mimi sina tatizo na hapa. Tatizo langu katika kifungu cha 6(2)(b) elimu, tumeweka hapo Shahada ya Pili wakati hata ile Sheria na Katiba ya nchi unapomtafuta Rais wa Zanzibar anaanza na Shahada ya Mwanzo. Sasa tunakwenda kumtafuta Mkurugenzi Mtendaji tu unaanza na Shahada ya Pili. Maana wakati mwengine najaribu kujiuliza nasema Mhe. Waziri anapokuja kutuletea Mswada ambao unapingana wakati mwengine mpaka kumpata Rais wa nchi kuwa inaanza na Shahada ya Mwanzo sasa hii ile *logic* ni ipi.

Sasa mimi mapendekezo yangu basi kiwango cha elimu kiwe cha Shahadi ya Kwanza, lakini na hii fani pia nina matatizo nayo. Fani hii kwa sababu hii ni Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, yaani Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi. Hapa tumewalenga wafamasia watupu na kwenye bodi hii hawafanyi kazi peke yao, hapa kuna watu wa *nutrition* unawakuta hapa, lakini kuna watu ma-*health officer* unawakuta hapa, leo wewe unakwenda ku-*deal* na wafamasia wakati umezungumza dawa, dawa sawa zinashabihiana, lakini chakula je! Sasa na hawa wataalamu ambao wanaingia kwenda ku- *support* kufanya kazi ile wao tumekwenda kuwatengenezea tabaka. Kutunga Mswada wa aina hii tunaanzisha *interest* za kundi fulani, tutakwenda kuvunja yale madhumuni hasa ya kuwa na wataalamu wetu wa aina nyengine katika taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hii katika kuipitia nimeipitia karibu, ukiangalia hata ile ya TFBA hapa ipo Mhe. Waziri mimi nitakupa, uitizame vizuri haikulenga fani hii, kwa sababu hapa tuna *deal* na uongozi na uongozi huu angalau basi mimi napendekeza isomeke ili kuondoa ile tabaka ambalo sasa hivi nataka kulishauri Baraza hili litoe mapendekezo au lipitishe Mswada ambao unatabaka la kundi fulani na kazi hawafanyi katika sura hii ya matabaka. Hapa Mhe. Waziri usije ukafanya siasa kwa sababu una tabia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema katika utaratibu huo wa (b) elimu angalau ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu kinachotambulika katika fani ya afya. Sasa wote hawa kwa sababu tuna *deal* na uongozi utawaingiza hapa sasa tena huku tunakwenda kufanya tabaka la nini. Tunachukua tu wafamasia maana yake hata kama unazungumza katika sura ya wanaofanana na hawa ukimkosa Mfamasia huyu utakwenda kwenye Mfamasia yule ambaye anashughulikia madawa ya kienyeji. Maana yake wewe unawalenga tu hawa Wafamasia, hawa wengine serikali yao ipi, wanatetewa na nani?

Mhe. Waziri mimi nilikuwa nashangaa sana kipengele hichi unakileta. Lakini hata katika sheria ukiipitia hii Mwanasheria ya *African Union Modern Law on Medical Product Regulation East Africa*, hakuweka masharti hayo, tunakuja kuweka masharti Zanzibar ambapo tunajumuia nyingi ambazo tumeungana nazo katika kusimamia hizi taasisi. Tunakenda wapi Waziri? Hatuwezi kwenda hivyo, tusiunde matabaka katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende kifungu cha (c) kinaonyesha uzoefu angalau wa kipindi cha miaka saba. Mhe. Waziri uliteuliwa hapa kuwa Waziri wewe mwenyewe hukuwa na usoefu wa miaka saba, unamteuwaje. Yaani hapa mimi nawatetea vijana, mkiweka suala la miaka saba mbele katika uzoefu, mnawaogopa vijana katika kuwashirikisha katika kuongoza taasisi hizi? Maana

sisi ndio tunatoka *undergraduate* baada ya miaka mitatu tunakuwa tuna sifa za kuwa viongozi, mnatuundia tabaka uzoefu miaka saba, hilo Waziri haliwezekani. Narejea tena mfano nakuwekea wewe zaidi, umeteuliwa kuwa Waziri hujawa na uzoefu wa miaka saba. Sasa hawa kwa nini tunafika pahala tunaweka kipengele cha mtu awe na uzoefu serikalini awe na uwezo wa miaka saba, basi humu ingekuwa Waziri Mhe. Muhammed Aboud tu humu wengine wote huko hawafai.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwenye taasisi za maslahi ya umma kuwawekea watu miaka saba ni muda mrefu. Napendekeza kwenye jambo hili angalau tuchukue miaka mitatu tunaweza tukatunga sheria, kwanza inawatetea vijana. Kwa sababu leo hii miaka saba tena hawa wote mnachukua watu karibu na kustaafu, wewe iukasome mmeleta sheria kuwa uwe na *master* watu wa Afya wanasoma karibu miaka saba, akesha akachukue master unalimbikiza tayari miaka mengine, uje uchukue uzoefu miaka saba, wewe si tena si itakuwa karibu na kustaafu, mkisha ndio mnampendekeza huyo mtu awe Mkurugeni Mtendaji. Fani hizi tusiziwekee matabaka sana, mimi napendekeza katika jambo hili iwe ni miaka mitatu na mimi buti zangu zipo katika maeneo haya. Hili sijakubaliana na mimi mpaka tufike pahala tuunde sheria ambayo itazungumza maslahi ya wote katika taasisi zetu za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kifungu namba 9. Marekebisho ya kigungu namba 9 hapo chini kuna kifungu namba cha 7(1) cha Kuanzishwa kwa Idara za Wakala kama ifuatavyo, hizi Idara uchambuzi wake haukupatikana humu, tunaweza tukaja tukarudi tukaandaa ule mgongano wa majukumu katika hili. Sasa tafsiri yake sina uhakika katika sheria maana sheria sikuipitia lakini ni vizuri hizi Idara zitajwe na yale majukumu yake. Lakini Wakuu wa Idara hatukutaja sifa zao, sasa leo tumekuja na sifa ile moja tu ya kumtafuta Mkurugenzi na pengine inakuwa kama mmemlenga hivi, lakini sifa za Wakuu wa Idara hazikutajwa na zitatajwa wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 12(1) ambacho maelezo yake nimeshayatoa kwa hapa Uwakala inaweza kuanzisha Kamati za wataalamu ili kuzipa majukumu yake ya kutekeleza. Sasa Wakala mara nyingi ukiiweka wazi hivi utakuwa unamgusa yule Mkurugenzi Mtendaji ambaye ana majukumu yale. Kurudi ukamuacha huyu akaandaa hizi kamati akazipitisha hapa tunaweza tukapata Kamati za kuja kutumia fedha za umma. Ndio maana pale nikashauri kifungu hichi kipitishwe na Bodi, yaani Kurugenzi ile iandae lakini Bodi ile kule iwe na mamlaka ya kupitisha hizi Kamati zitakazoundwa na huyo Wakala au Mkurugenzi Mtendaji kwa niaba ya Wakala ziende kule.

Mapendekezo yangu nimeshayatoa nakazia katika kifungu hicho kwa sababu kama sikupata majibu mazuri hapa nitaweka buti *In shaa Allah*. Hapo hapo katika kuongeza kifungu cha 12(1), 12(2) nimesema kwamba tuongeze kifungu cha 12(3) kwa mantiki niliyoisema mwanzo kuwa Kamati zitakazoanzishwa na Wakala ziwasilishwe kwenye Bodi ya Ushauri kwa kuidhinishwa, sasa angalau yule Mkurugenzi Mtendaji imfunge asije akatuundia kamati tu za ovyo ovyo kwa sababu tayari huku keshapewa *room* kubwa utawala wake sasa unaishia kila siku tunapata kamati.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende tu katika kifungu cha 15(2) kuna wakala itandaa taarifa kwa kila muda na kuiwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya kujadiliwa na kuzingatiwa. Sasa hapa kuna kauli ya kila muda, muda huo muda gani, angalau tuende tuone inakwenda kama baada ya miezi sita, sasa tafsiri kamili kila muda, maana yake kila muda wiki wiki maana tafsiri haijakaa vizuri. Napendekeza kwamba tuiainishe kuwa iende katika mfumo labda wa kila baada ya miezi minne iwe inawasilisha hapa au vile ambavyo Mhe. Waziri utakuja kutwambia lakini ioneshe hii kila muda haikukaa vizuri, tuoneshe ule muda wenyewe ili tuone vile vikao basi vya kupokea ripoti viwe vinafanyika kwa utaratibu mzuri. Au vyenginevyo basi tukubaliane tukiwacha hivi tuongeze maneno ambayo tafsiri ya hapa itapatikana kwenye Kanuni ambazo zitaandaliwa kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa hichi chombo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kifungu cha 20, marekebisho ya kifungu cha I19(2), lakini chenyewe cha 19(1) kimeelezea hapa mfanyakazi wa Wawakala, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi au Kamati, atatakiwa kutaja maslahi aliyonayo yanahusiana na bidhaa yoyote ya tiba. Katika mazingira haya, hapa kuna Bodi ya ushauri, kuanzia Mwenyekiti na hao wengine hawakuainisha hapa, hawa wao maana kuna Bodi ya Wakurugenzi lakini kuna Bodi yenyewe ile ya Wakala hawakuainishwa hapa kupeleka wao katika utaratibu ambao umeelezwa na kifungu hichi.

Naomba katika kifungu hichi tuongeze na Bodi ya Ushauri pia nayo itajwe hapa ili kwa sababu wote hawa wanafanya kazi katika taasisi moja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kifungu cha 119(a) (2) naomba nikisome.

"Tamko la mgogoro wa maslahi litashughulikiwa kwa mujibu wa miongozo iliyotangazwa"

Sasa hapa naomba Mhe. Waziri atakapokuja anambie tu iliyotangazwa na nani. Ni vyema tukatoa tafsiri yake kwa nani atakaekuwa na wajibu wa kutangaza kati ya Bodi ya Wakala au Mkurugenzi Mtendaji.

Mwisho katika kuchangia Mswada huu naomba niende katika jaduweli ambalo linaloonyesha mwenendo wa vikao vya Bodi ya Ushauri, hapa kuna eneo linamtaja Makamo Mwenyekiti Namba 2. Kwa hapa inaonekana Bodi itachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti.

Kule nilisema hii iainishwe iwe ni sehemu ya kazi ya Bodi na isiwepo hapa, badala yake sasa baada ya kuondoshwa hichi kifungu kwenda kuainishwa kwenye kazi za Bodi za kumchagua huyo Makamo Mwenyekiti basi iseme tu hapa katika kipengele hichi Makamo Mwenyekiti, kuwa kutakuwa na Makamo Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri atakayechaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi. Lakini ilivyo sasa ihamie katika kazi za Bodi kama ambavyo inaelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wenzangu kuwapongeza wana Kamati lakini naunga mkono kwa asilimia 80, ishirini nahitaji maelekezo ya Mhe. Waziri mle mnamo vifungu ambavyo vile tumeshauriana marekebisho na nitakuwa na buti kama 6 au 5.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni kwa mchango wako, natumai Waziri ameusikia na ataufanyia kazi. Waheshimiwa Wajumbe nami naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Afya na Watendaji wake kwa kutuletea Mswada huu. Lakini pia shukurani za pekee ziende kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti mahiri Mhe. Mwinyihaji Makame kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawapongeza sana.

Naomba Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha niwataje wachangiaji wa mwanzo ambao watakaokuja kuchangia jioni tutaanza na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Hidaya Ali Makame. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima naomba niakhirishe kikao mpaka saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia mambo yangu machache katika mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, nikianza nitaanza na kifungu kipya cha 60A. Mhe. Mwenyekiti, hapa kimemtaja Wakala ambaye anatakiwa kusimamia kifungu 60A, 60B na 60C maelezo yake ambayo yametajwa…

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunapitia Mswada wa Marekebisho ya Vyakula, Dawa na Vipodozi ambao unasimamiwa na Wizara ya Afya, cha kusikitisha ndani ya Baraza hili hamna Waziri wa Afya wala Naibu Waziri wa Afya. Sasa sijui tunawaambia vipi wananchi ambao wanatuangalia sasa hivi hatuoni kwamba kile tunachokiimba siku zote juu ya dharau au kutothaminika kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuhusu utaratibu ni kweli kwa hivyo naomba niahirishe. Waheshimiwa Wajumbe naomba tuendelee kwa sababu yule aliyetoa kuhusu utaratibu alizungumza kuwa hamuoni Waziri lakini Waziri wa Afya naona ameingia. Waheshimiwa Wajumbe tuendelee.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hapa Kanuni inamtaja wakala na inampa kazi ya kusimamia hizi sheria. Mhe. Mwenyekiti, langu mimi liko hapa ninamuomba huyo wakala ambaye anasimamia hizi sheria, hizi sheria ni nzito na hizi sheria ni ngumu, tunamuomba kwa kazi hii ambayo kapewa akiisimamia vizuri mimi ninaamini kwamba hizi dawa za magendo na mambo mengine mengine yatapungua.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilimtaka wakala asimamie ipasavyo katika bandari hizi bubu, sasa hivi kumejitokeza bandari bububu ambazo bandari hizi zinaingia madawa, zinaingiza vyakula, zinaingiza na madawa mengine ambayo ni hatarishi mbali ya madawa ambayo yanatibu. Basi ninamuomba wakala huyu asimamie masuala haya, atakaposimamia masuala haya katika bandari hizi bubu ninaamini kwamba yale madawa ambayo hayana viwango maalum au vile vyakula ambavyo havina viwango maalum tunavyoviona vinavyoingizwa na bandari hizi bubu kama mfano michele mibovu, nyunga, mafuta ambayo yameshamaliza muda wake ninaamini kwa hapa litasaidia kwa kiasi fulani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kumejitokeza uingizaji wa ng'ombe kutoka sehemu tofauti tofauti. Ningemuomba Mheshimiwa kutokana na kifungu hiki ambacho kipo aje kunieleza je, ng'ombe wale ambao wanaingizwa katika nchi yetu wamekaguliwa. Je, ni salama kwa sisi kutumia.

Nikitoka hapo niende kwenye suala la huyu huyu wakala asimamie masuala ya wale wamachinga wanaoingia mitaani na kuuza bidhaa. Kuna bidhaa Mheshimiwa ambazo zinauzwa mitaani ambazo hazijathibitishwa, bidhaa hizi unazikuta dukani unanunua bei kubwa lakini ukenda mitaani unazikuta bidhaa zile ziko bei ya chini. Kama unavyojua wananchi wetu hali ya kiuchumi ni ndogo kwa vyovyote biashara zile watazivamia watazinunua bila ya kujali afya zao, bila ya kujali kwamba ziko nzima au la ni mbovu wanatumia. Pia wakati huo huo tunaona kwamba kuna watu wengi siku hizi mitaani wanajitokeza na kuuza zile dawa ambazo makaka zetu wanazitumia kwa ajili ya kuongeza nguvu fulani. Je, Mhe. Mwenyekiti, hizi dawa ambazo wanazitumia makaka zetu nimuulize Mhe. Waziri zina viwango na je, hizi dawa wamezipitia kiumakini? Kama hawakuzipitia kiumakini aje atueleze ni hatua gani ambayo wataichukua kupiga ili dawa hizi zinazosababisha mambo fulani zisiingie katika nchi yetu na kuwaharibu makaka zetu ambao tunawategemea kwa ajili ya kutupatia vizazi.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika wafanyabiashara tunawakuta kwamba pia kuna wale wafanyabiashara wa Darajani, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri je, wale ambao wanauza zile tomato, biskuti wanakaguliwa kwa njia gani na vile vitu ambavyo wanaviuza ni vizima vina uhalali wowote wa kuuzwa? Kama ni vizima sawa lakini kama vitakuwa havina uhalali wa kuuzwa basi atwambie ni hatua gani ataichukua kwa watu wale ili wasiweze kuingiza vyakula vile na kutuulia watoto wetu. Kwa sababu vyakula vingi wanaviuza pale tunaviona kwamba ni rahisi lakini mwisho wake ukija kuchunguza pengine tunanunua kifo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, *Bismillahi Rahmani Rahiim* na mimi nitaomba kuchangia Mswada huu wa Wakala wa Vyakula, Dawa na Vipodozi. Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba wakala huu wa madawa, vyakula na vipodozi ni suala muhimu sana katika jamii kuliko kitu chochote ninaweza kusema kwa sababu kimehusisha vyakula ambapo binaadamu ndio wanategemea, wakala imehusisha madawa ambayo ndio wanadamu wanatibiwa na imehusisha kwa upande mwengine mapambo ya binaadamu ambayo pia wanayategemea. Sasa kwa mswada huu ni

muhimu sana katika jamii na unatakiwa uwe katika ya kutahadharishwa sana katika masuala haya ambayo watakayokwenda nayo katika kuhakikisha hili suala linafanikisha kama malengo walivyoyazungumza.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, bado Zanzibar kuna matatizo ya vitu vingi feki, asilimia 80 ya vitu Zanzibar vilivyokuwepo vinavyotumika haviko kwenye kiwango kizuri kama vya nchi nyengine. Tukenda katika suala la chakula Mhe. Mwenyekiti, leo Zanzibar kuna mafuta. Kwanza tusifananishe vitu feki, kuna vitu feki vya nguo tunaona, kuna viatu kabila ya *nike* feki, kuna nguo nzuri nzuri feki lakini tukenda katika chakula ni suala tofauti kabisa. Mimi ningeomba sana kwanza wakala hawa wakawa makini zaidi, najua wako makini lakini wakawa makini zaidi ili kuhakikisha hivi vitu vipo vya *standard* iliyokuwa nzuri kama wanavyotumia nchi za wenzetu huko duniani.

Tukiangalia mfano mdogo tu basmati tunayotumia Zanzibar na tukenda hapo nchi za Afrika nyengine tu au *Middle East* au *Europe* au Amerika basi basmati ile iko *totally different*. Sukari tunayotumia sisi hapa ya *brown sugar* tukenda kule *grade* yao iko tofauti. Sasa hivi vitu vyote vinavyokuja Zanzibar hata tunapovitumia basi inakuwa *grade* yake si nzuri ni bora bei ipande kidogo lakini wananchi wapate vyakuka vyenye uhai na vizuri, kuliko vyakula viwe rahisi wakaumia wakaja wakafariki wakapata masuala ya *cancer* na madhara mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala langu la chakula, tumeona kuna mafuta ya kupikia yanauzwa mafuta kama yale ya *okay* yamejaa *cholesterol* yana maradhi mengi sana na yanauzwa kwa ma-*gallon*, mafuta yale ndio wanatumia wauza *chips* wanatumia wafanyabiashara wengi wa kiwango cha chini, matokeo yake wanapikia yale yanafika hata miezi 6 hawajabadilisha kwenye karai lao yanageuka rangi kutoka rangi ya dhahabu mpaka rangi nyeusi mafuta. Mhe. Mwenyekiti, yale yatasababisha *cancer*, yatasababisha maradhi mengi. Mimi ningeomba zaidi watapokuwa wanafanya hizi kazi zao wapite kuangalia pia madhara haya, najua wameshawahi kupita huko nyuma lakini hivi vitu vinatakiwa wapiti angalau kila mwezi wakahakikishe kwa sababu watu mafuta yale wanachukua zaidi ya miezi mitano, sita hawabadilishi wao wanapika tu, tena wakipika wenyewe watapika *chips* humo humo, kuku humo humo, mishkaki inakaangiwa humo na samaki na kila kitu hawajui kugawa. Mimi ningeomba kwanza wangewapa elimu, mafuta yale huwezi kukaangia kila kitu lazima kila kitu kinataka utaratibu katika suala la kupikia.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna masuala haya ya kuku, masuala ya samaki leo kuku tumeambiwa hivi juzi kwamba wanapewa madawa ili wakue wapate

kuuziwa wananchi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hili suala linasikitisha sana kuona kwamba kuku wale tunaokula wanaingiza maradhi, wanapewa madawa ya kuwakuza wengine wanauzwa katika jamii marikiti hata hawajafikiwa kiwango cha kuliwa lakini tayari kwa kuwa wamepewa tu madawa ya kulishwa kuku wakue watu wanauziwa na mamlaka hii naweza kusema kwamba inawaachilia. Kwa sababu *still* hivi vitu vipo marikiti vinauzwa, leo tunakuta kuna masamaki ambayo yanakaa zaidi ya miaka 2, mwaka mmoja kwenye *container* mapeduu, watu wanauziwa wakati hiki ni kisiwa. Sisi tulikuwa hatuna hana ya kula mapeduu, mapeduu wakale wenyewe Brazil na nchi nyengine, hapa Zanzibar tule vitu *fresh* tuna bahari yetu, tuna vyakula vyetu viko *fresh* kabisa lakini leo tumegeuka kila kitu sisi tunatumia maboksi, tunatumia vyakula vya makopo, matokeo yake yanasababisha *cancer* na maradhi mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaenda kwenye suala jengine ambalo la muhimu pale Mhe. Waziri wa Afya alieleza katika hotuba yake kwamba, mamlaka hii washasafiri karibu nchi 15 kwenda kukagua. Mimi wazo langu, wao wana elimu, wao wana mashine za ukaguzi kuna haja gani ya wao kusafiri kwenda nje ya nchi kwenda kukagua viwanda vya watu wakati kule wakaguzi wenyewe wapo. Kama elimu yao inawaruhusu kufika kule wakaweza kukagua, kwa nini elimu hiyo hiyo wasiitumie hapa Zanzibar vyakula vikifika bandarini wavikague wavizuie kwa wiki moja wavifanyie ukaguzi kilichokuwa hakuna kiwango wakaki-*destroy* kama vinavyokuwa *destroyed* vyengine na kama kina kiwango wakawaachilia. Lakini leo tukakuta wafanyabiashara wanalipishwa fedha kwamba watu wasafiri la kama kuna mtu hajawahi kusafiri anataka kusafiri kwa kutumia pesa za matajiri au za wafanyabiashara azungumze.

Lakini pointi hii ya hawa watu wanaotaka kusafiri katika mamlaka hii mimi sijaona umuhimu wake. Kwa sababu elimu wameshakuwa wanayo tayari ya kujua hicho chakula kibaya hiki kizuri, mashine wanazo wao wanaenda kusafiri kwenda kwenye viwanda kule kufanya nini, chakula wasubiri hapa hapa bandarini. Ama bandari kubwa au kuna bandari ndogo wakikikamata wakichunguze kwa muda wa wiki moja kama kizuri wakiruhusu kama kibovu wakiunguze au wakitupe. Lakini leo utakuta mtu anataka kusafiri nchi 15 pesa wanatoleshwa wafanyabiashara matokeo yake ni dhulma tupu.

Mimi ninarudia tena Mhe. Waziri wa Afya kama watendaji wa mamlaka haya hawana fedha ya kusafiri hawajawahi kusafiri wapeleke kwa mfuko wako wa Wizara ya Afya lakini wasikamuliwe wafanyabiashara kukandamizwa kwenye masuala kama ya kuwa-*push* kwamba lazima watu wasafiri wakague huko. Kama ni hivyo basi nchi itafilisika. Vitu vitavyoingia bandarini, *airport*, mtu

anapoleta mzigo wake basi uzuiliwe kwa muda wiki moja au siku tatu watoe *samples* wakazichunguze ndio wa-*release* ule mzigo. Lakini leo utaambiwa mtu mzigo ushafika mpaka kwenye duka halafu anazuia huo mzigo umepita wapi. Vitu vyote vinavyokamatwa Zanzibar vingi vyao vinakamatwa madukani havina kiwango viliingia vipi kama havina kiwango wakati mamlaka haya yapo ya kuzuia hivi vitu.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya ni muhimu narudia tena na hii ni jamii na bora vitu vipande bei kidogo lakini wale watu wale kitu *quality* kuliko vitu viwe rahisi watu wafe kwa *cancer* wafe na maradhi mengine. Tumeona masuala mengi, kuna masuala ya vinywaji, pombe hatutoizungumzia lakini pombe ndio inayowaua watu mara moja kwenye masuala ya sukari, pombe inamfanya mtu awe na wazimu akishakulewa hajijui hata anafanya nini.

Lakini hapa haizungumzwi pombe ina madhara, wakala huyu mimi sijamsikia bado kama kuna pombe kaizuia wakati kuna pombe zinatengenezwa Tanzania mashaka matupu. Ikiwezekana hata hizo pombe mimi kwanza simwambii mtu anywe pombe anayekunywa pombe atajijua mwenyewe huko akhera atakwenda kuhesabu hesabu zake. Lakini mashaka haya vinywaji kama hivi vya pombe, vinywaji vya *redbull* vinasema hasa kwamba ni hatari lakini *still* nchi hii vinaruhusiwa. Wanauza basi hawajali umri, hawajali chochote, wao ukenda na fedha yako unauziwa, ukiwa unataka pombe mia, unataka *crate* kumi utauziwa, huulizwi umri wako wala nani anaenda kunywa. Sasa vitu kama hivi viko vingi vyenye madhara. Leo soda ya *cocacola* wanasema madaktari ukinywa sana hata ganzi haipandi vizuri unapopigwa sindano ya ganzi. Sasa hivi vitu vina madhara vingi lakini vichunguzwe. Sio wananchi wanakaa tu kuwa vitu vinaletwa letwa vinaleta madhara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningekwenda kwenye masuala ya madawa, madawa hasa haya madawa *pharmacist* unakuta dawa imeandikwa hasa *made in* India lakini ukenda kule India haipo wanakwambia hawaitambui dawa ile. Mimi kuna dawa moja niliichukua kufika kule nikaiulizia *pharmacy* karibu sita wakanambia hii dawa haitengezwi India. Lakini nitachoomba nisije nikafuatwa na Wizara wakaja wakanambia tusaidie aa wafanye wenyewe hayo ndio mamlaka yao, mimi nazungumza tu kabisa, sitaki kuja kutoa ushahidi wala kumsaidia mtu, kazi waifanye wenyewe wasije wakanifata nina wananchi milioni tatu huko wananisubiri. Dawa zipo Zanzibar, *made in* India, *made in* China, *made in* Barazil ukenda Brazil dawa zile hazipo wala hawazitambui dawa hizo zinatoka au kuna Brazil mbili?

Mhe. Waziri wa Afya hili suala lipo, madawa yanayouzwa mabovu na mengi sana hayako kwenye kiwango. Ukenda nchi za wenzetu madawa haya hayatumiki lakini majaribio makubwa yanakuja Afrika kwenye madawa. Utakuta kuna madawa mengine huko wazungu wakeshayatengeneza huko moja kwa moja yataletwa Afrika kuja kujaribiwa. Sasa Mhe. Waziri madawa yote haya ya msaada au ya majaribio au yale ya kinga tunaomba sana muyachunguze. Kwa sababu hizo kinga nyengine tunazopigwa Zanzibar huko kwengine mbona hakuna tunakuja kupigwa huku tu Afrika. Kuna mashindano ya ajabu ajabu mtoto anazaliwa leo anapigwa sindano 100 mpaka akiwa mkubwa mwaka mmoja.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili suala lipo na madawa yanayouzwa na cha ajabu zaidi kwenye *pharmacy* siku hizi zimegeuka *super market,* ukenda ndani *perfume* zimo *chocolate* zinauzwa, yule muuzaji wa kuuza *perfume* na dawa za meno anauza dawa. Matokeo yake unataka ya tumbo anakupa dawa ya mshiba. Hayo mambo yapo tushaona na hasa wakati wa usiku, wale watendaji wanaopangiwa kuuza *pampers* wao ndio wanauza madawa akiwa hayupo yule muuza dawa. Haya masuala yapo na yanaachiliwa tu yanakwenda ndio maana unasikia kuna watu wengine wanakufa wamezidiwa, wamezidiwa na haya madawa wanaouziwa ya uongo uongo, watu wanaouza hawana kiwango elimu ndogo. lakini mamlaka haya wakala hawa kama hawajawa makini basi sifikirii kama wataweza hebu utendaji wa hali ya juu wasichoke, wafanye kazi kwa nia moja, wafanye kazi bila upendeleo wakandamize vitu wasiogope mtu kaingia hasara au hajaingia hasara wao vitu viko *low grade* wa *destroy* tu sifikiri kama kuna mtu anakuja walaumu katika masuala kama haya.

Wananchi wanaumia hii nchi ina wanyonge leo akiumwa hapa ndo hao unasikia hakuna hata pesa ya kwenda kumtibu tufwata siye waheshimiwa ndio kwanza tunazima simu hapa, tunazungumza kweli mtu mwananchi nina jimbo nina watu thelathini wangapi wanaumwa kwa siku wanyonge kwa sababu haya ya mavyakula mabovu mbona wazee wa zamani hawaumwi ovyo ovyo. Leo wanaumwa ovyo kwasababu mavyakula yanayoruhusia kuingia nchini mingi mabovu hayako kwenye kiwango kama nchi nyengine.

Leo ukileta mchele, sukari, unga, siagi, mafuta kila kitu mpaka hizi soda tunazokunywa sisi ladha yake tofauti na ukenda kunywa soda za nchi nyengine, kama Dubai na nchi nyengine. *Chocolate* tuliona juzi Malaysia wamekamata *chocolate* za *diary milk* zina mafuta ya nguruwe ndani wakadhani kabisa sasa hivi *chocolate* za *diary milk* ndani ya Malaysia haziingii. Lakini hapa sijui hata kama kunafanywa utaratibu kama tunanyishwa mafuta ya nguruwe, kama mafuta ya kuku sisi tumo tu tunakwenda kwenda tu na wakala huu bado

kitengo hiki ni kidogo hakiwezi kufanya kazi kabisa ndani ya Zanzibar kikajishoteleza lazima waweke watu wa kutosha wapewe vifaa vya kutosha, wapewe bajeti ya kutosha na wapewe mamlaka ya kutosha kwenye masuala haya sio kwasababu hawa wakala hawa, utakuta wanafanya kazi siku ya siku wanaendeshwa kama *remote.* Mamlaka kama mamlaka wenyewe hawana hawa kama *remote* wanaweza kukamata kitu ukaja kukuta kile kitu chenyewe hawana nguvu nacho.

Mimi ningeomba sana vitu vyovyote kama hivi vya muhimu vya wananchi ambavyo zinasabisha maradhi basi wapewe nguvu sana wao wenyewe ndio wenye mamlaka wa vitu vile. Lakini vile vile bajeti ambayo kama wanataka kusafiria basi naomba sana bajeti hiyo itoke Wizara ya Afya na wasitoleshwe wananchi au wafanyabiashara kwa lolote lile, la kama wamekamata ana-*forge* analeta vitu *fake destroy* mfunge mpige faini lakini usiwe na sababu ya kutaka kumtolesha mtu fedha lazima watu waondoke hicho kitu hakiwezekani kabisa. Lakini tukienda kwenye vipodozi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe Mwenyekiti: Mhe. Nadir una dakika 2 naomba umalizie.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti mimi ndio kwanza nina dakika saba labda umekosea samahani. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, vipodozi vilioko Zanzibar takribani vyote fake, vyote fake watu wanababuka uso wanauziwa madude ya kupaka usoni wanafanya mapele wanawake madawa wanaouziwa *fake*, wananchi bila ya shaka wa nchi za kimasikini wanaona wafate vitu rahisi kumbe vitu *fake*. Bora nchini viuzwe bei juu lakini wapate vitu vyenye afya, madude yote *fake* asinambie mimi hasa kama kuna vitu *quality* vinavyouzwa asimilia 3 tu natoa. Vinajulikana lakini vimezagaa huko mjini leo mtu *perfume* inauzwa akiitia tu anaanza kukohoa hapo hapo imejaa *sprit* na *acid* sijui na madude gani, ambayo yanaingizwa ndani kwenye masuala ya vipodozi vitu *fake* ndani ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, cha ajabu juzi tumesikia kwamba supu za pweza zinaingizwa *Viagra* na *still* Wizara ya Afya inamuachia mpaka leo wanauza supu za pweza.

Supu kama wameshagundua sehemu moja zinatiwa madawa wapige marufuku Zanzibar nzima na Pemba supu za pweza zisiwepo, hakuna mtu mwenye shida sote tuna nguvu zetu hatutaki *Viagra* wala nini, au vipi bwana sisi tuko fit hatutaki *Viagra* supu Mhe. Waziri zipige marufuku zote kamata kamata piga marufuku.

Mhe. Mwenyekiti mimi nina masuala yangu Mhe. Waziri aje anijibu haya hapa nayauliza.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri kanifanyia dawa hata kitabu cha maswali sikioni lakini naomba sana mimi nitakuja kuuliza maswali yangu japo baadaye kidogo nitaomba uniruhusu.

Mimi hoja hii naiunga asilimia 80, asilimia 20 nangojea kwenye maswali huko mbele tuje tufahamiane. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe Nadir kwa mchango wako sasa namuomba Mhe. Simai Mpakabasi akifuatiwa na Mhe. Salma Bilali na Mhe. Suleiman Sarahan ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: (Mpakabasi) Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kukushuru wewe na kiti kwa kunipa hii nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu lakini pia shukrani za pekee ziende kwa wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kutoka Kisiwa cha Uzi Ng'ambwa mpaka Dunga, Gogoni pamoja na Kinyongo pamoja na barabara ya Mwera kabla ya kuvuka daraja na wale wote wanaishi katika jimboni kwangu, kwa hivyo mimi naomba kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kuwepo hapa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nipongeze maoni ya Kamati na Wizara husika kwa kuweza kuleta mswada huu ambao ni muhumu kabisa kwa wananchi wetu, kwa Wazanzibari wote na pia upande mmoja au kwa njia nyengine kwa Watanzania. Kwa sababu mambo ambayo yamo katika mswada huu juu ya marekebisho haya ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi yanawagusa wananchi kila siku kila kukicha.

Mhe. Mwenyekiti nichukue fursa hii pia kuwapongeza wenzangu wote waliotangulia na nisingependa kurudia yale ambayo mazuri mengi wameyaongea na mimi nitapita katika eneo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Waziri kwenye maelezo yake nimefurahi sana kuona madhumuni na sababu juu ya marekebisho ya sheria hii katika mswada huu na kuna eneo hapa linasema nanukuu:

"wakala inayopendekezwa, hii itafanya kazi kama Taasisi isiyojitegemea kikamilifu ili kukuza mpango wa usimamizi, sera, viwango, miongozo na utaratibu kwa ajili ya usalama na ubora na dawa za binadamu na wanyama, chakula cha binadamu na wanyama pamoja na bidhaa zinazolingana na hizo"

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema awali kwamba mswada huu utaelekeza kutatua kero au mawazo ya wananchi ambayo yamekuwa yako mengi au kidogo lakini yale ambayo yanawagusa, ushauri wangu kwanza kwa Waziri ni kuhakikisha viongozi ambao watateuliwa kuendesha Taasisi hii wawe wazalendo, wanaipenda Zanzibar na wanawajali Wazanzibari wote kwa maslahi yote.

Hili linaweza lisiwemo ndani ya maelezo na sifa zilizoelezwa lakini tunayo Taasisi ambayo inasimamia *vetting* ya viongozi wetu ambao mimi pia kwa upande wa kamati yangu nasimamia ningemshauri sana ahakikishe anapata majina ambayo wanakaostahiki kuingia kati bodi. Lakini pia akahakikishe hao watakaokuja kuteuliwa huko mbele wanajaza fomu za Tume ya Maadili ya Viongozi kwa ile sheria ya umma, ambazo waweze kutangaza mali zao na wajulikane. Nasema hivi kwa sababu binadamu ni binadamu sisi na *temptation* au unaweza kupata hamu ya jambo lolote pale endapo makosa yamefanyika.

Kwa hiyo ni vizuri tukawatambua mali zao ili huko mbele tunapoelekea basi ikiwa kuna mtu kama anataka kuharibu au kuwapa fedha au chochote cha zawadi katika juu ya utendaji wa kazi yao kwa kuleta ufanisi, basi waogope sheria waogope Mwenyezi Mungu na walinde maslani ya Wazanzibari.

La pili ningeshauri pia waziri kuwa karibu sana katika kufanikisha haya malengo ambayo nimeyataja juu ya maelezi yake basi taasisi ambazo ni rafiki au zitakuwa zinahitajika kufanya kazi kwa ukaribu hasa kwa mfano za *Zanzibar Bureau of Standards* na zile nyengine zote basi yeye mwenyewe azisimamie kwa nguvu zote ili katika kulinda sheria hii na watendaji wake wote waweze kufanya kazi kwa ufanisi kabisa na ili tija ipatikane juu ya malengo yote.

Suala la tatu nataka niangalie ni suala ambalo nilikuwa napitia kwenye sheria kwenye kifungu labda hii ni masahihisho tu kidogo ukiangalia kwenye kifungu cha 19 na 93A nafikiria Mhe. Mwakilishi asubuhi Mhe. Wanu alikitaja hili suala la mtu anayehodhi alama ya dawa ambayo inadhaniwa, nafikira hapa inabidi Mwanasheria Mkuu atusaidie hili neno kidogo tuweke sawa.

Lakini pia kwenye kifungu namba 8 ambayo inataja kifungu cha 6 cha sheria mama kitafutwa na badala yake kuwekwa kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais". Hiyo (a) inasema ni Mzanzibar hakuna kitu kama Mzanzibar ina maana hapo ije ni Mzanzibari na pia iongezwe 'i' hii Mzanzibar nafikiri hiki kiswahili sijui

maana nimemsikia Waziri amesema yeye anaongea lugha saba naamini hapa basi atakuwa kapitiwa kidogo hili katika kuweka sawa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti suala zima la usimamizi wa hii Taasisi na uingizaji wa bidhaa Mhe. Mwakilishi alipopita alizungumza suala la kufanya kazi ukaribu na wafanya biashara na matatizo ambayo yalioko huko nje, mambo ya kusajili dawa na kuleta utaratibu huu ningemshauri Waziri atakapokuja kuzindua bodi yake pamoja na watenadaji hawa watakaokuwa kazini, basi kuangalia mfumo mzima juu ya uingizaji wa bidhaa pamoja wa uandishaji wa haya madawa ili kuwa *register* na zikatambulika hasa katika hizi *content* zake. Kwa sababu ukiangalia bidhaa zinazokuja hapa Zaanzibar au Tanzania ni nyingi sana tunaweza kuangalia katika upande wa madawa lakini dawa hiyo hiyo inaweza kuwa *metakelfin* au pengine ni *panadol* ikatengenezwa hata *contents* hizo hizo katika nchi tofauti na jina likawa ni jengine.

Lakini inapokuja kufika hapa wakati mtu anamazoea nao kutumia unakuta wakati mwengine hapa panaleta mvutano kati ya mfanyabiashara na bodi husika. Mimi naomba sana itambulike kwamba mfanyabiashara siku zote nasema humu ndani sio adui, yeye yupo kwa wakati mmoja kuja kufanya kazi zake. Lakini serikali kwa upande wake wao ni wasimamizi kuwa mtu anateswa, ananyongwa, anasumbuliwa inafika pahala mpaka mtu ile biashara anayoifanya anaona kuwa ni maudhi, tena sio maudhi inakuwa maudhi ya roho juu ya maudhi. Kwa hiyo naomba sana *spirit* ya sheria hii na serikali hii mliokuwa hapa nyote mawaziri katika mambo ya utendaji mtafute njia ambayo mtakayofanya kuwathamini hawa pia wanaofanya shughuli zao za kila siku.

Wanapoingiza bidhaa hizi mjue na wao wanahangaika wanapanga mahesabu yao na usumbufu kama huu kwenda kuandikisha madawa unakuta pahala wakati wengine hawa wanapoleta hizi dawa wanaagizwa na wazee wetu ambao ni wagonjwa, wanabeba hizi dawa kuwaletea lakini hapa dawa hujaiandikisha ibakishe hapo kuna dawa nyengine zinataka zikae kwenye fridge bei zake ni za ghali kabisa ambazo ni *perishable* na zinapokaa nje zinaleta hasara kwa wenye makampuni. Kwa hivyo tuangalie mfumo mzima katika uingizaji wa vitu ambavyo vinakuja hapa na ili kuthibitisha kama kuna njia ambayo mtu kaitambua kama alivyosema Mhe. aliopita hapa Mhe. Nabil amezingumza wakati mwengine vitu ambavyo vinatoka nje vinajulikana.

Lakini wakati mwengine mtu kwa kumkaba mwenzake tu hapa ama kwa nia mbaya au nia nzuri lakini katika utaratibu ambao uliokuwa haukubaliki utaratibu ambao mimi nitaita utaratibu ambao haustaaahiki kumnyanyasa mfanyabiashara, ikiwa yeye ni *pharmacist* au ni mtu ambaye analeta bidhaa

zake tafauti unakuta mtu ananyongwa mpaka anakuwa tafrani kwa kweli hili hatuwatendei haki.

Mimi ninasema mara nyingi mfanyabiashara sio adui wa nchi hii anatakiwa athaminiwe aheshimike kama sisi humu ndani tunaheshimiana kwa pamoja, tena hili lisitoke katika biashara mkubwa ambaye ana jina kubwa au duka kubwa litokane kutokana na mfanyabiashara aliyekuwa mkubwa mpaka mfanyabiashara ndogo ndogo uko mtaani anapoenda. Kwa hivyo kama ana bidhaa yake sio unafika pale unamchukua unambeba unamchota kwa sababu pengine utaratibu haupo, hata kama pia utakuta bidhaa ambayo tayari imesha *expire* usimdhalilishe kwa kumtoka kwenye TV. Wakati mwengine yeye mwenyewe kama ana *product* nyingi anakuwa hailewi wakati gani *product* imesha *expire* umueleweshe, umfundishe kuna utaratibu mwingi wa kumpiga mtu faini lakini kuliko mtu kumdhalilisha ukamtoa jina lake kwenye TV kutokana na biashara moja tu ya *tomato paste* imesha *expire* ana *product* zaidi ya hamsini elfu pengine ana-*deal* na *product* zaidi ya elfu mbili wewe *product* moja unakwenda mtu unamdhalilisha unaamtoa kwenye TV anaonekana yeye ni adui wa Wazanzibari kweli hiyo ni haki.

Wakati nyinyi mawaziri wakati mwengine mnakuja hapa mnakosea ipo wakati mwengine mnalidanganya Baraza tunakaa, tunakaa kimya tumeona, hata leo kuna wengine wamesema maneno ambayo sio sahihi tunamezea lakini wafanyabiashara wanapokosea tunawafahamu. Leo kuna waziri katamka humu ndani anazungumza lugha saba aje atwambie hizo lugha saba basi anazozijua, atutajia hilo lugha saba tuamini kama ni kweli. *(Makofi)*

Lakini wakati mwengine biashara zinavyokwenda anapokutwa mtu anakotolewa kuna mambo ya kufanya kazi kwa ukaribu, na hapa ndipo sisi tunapozungumza sisi kwa pamoja. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Mohammed Aboud Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ibara 59 page ya 5 ya kanunu zetu kwa mjumbe si vizuri kusema maneno ambayo yanayohusu serikali na ambayo mawaziri hawajayafanya. Kwa hivyo naomba Mhe. Simai aombe radhi kwa kusema mawaziri wanadanganya Baraza lako tufuku ama atoe ushahidi lini na waziri gani alidanganya Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mimi Mhe. Mwenyekiti, inawezekana niliteleza kwa sababu wakati mwengine mawaziri wanakuwa kweli wanasema maneno ambayo hatuna uhakika nayo lakini mimi ningesema

kama siyo sahihi leo waziri alitamka hapa anazungumza lugha saba basi naomba atuthibitishie hizo lugha sasa anazozizungumza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai na Mhe. Waziri ambaye ameomba kuhusu utaratibu kwanza nilikuwa sijawaruhusu nyote. *(Makofi)*

Nyote nilikuwa sijawaruhusu Mhe. Waziri kasimama kuhusu utaratibu amesoma tu sijaruhusu, na Mhe. Simai naye akasimama anamjibu Waziri sijaruhusu, lakini Waheshimiwa Wajumbe ninachokitaka kukisema hapa tunachangia mswada ambao uko mezani wa vipodozi kwenda kinyume na mswada huo au na michango hiyo si taratibu. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wajumbe mtakapochangia twende moja kwa moja katika huu mswada uliopo kwenye meza kuliko vyenginevyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Simai kama ulitamka hivyo na Waziri ametaja hapa kwa maelezo yako basi naomba uombe radhi. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, mimi nitasema vitu viwili nitaomba radhi lakini ninachokisema mimi wakati mwengine mawaziri… Mhe. Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi na maneno mazuri kabisa naliomba Baraza hili radhi kabisa, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai ulibakiwa na dakika kama tatu nakuomba umalizie hizo dakika zako ili tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuendelea na maoni yangu. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nazungumza wakati naendelea ni kwamba wakati mwengine unakuta mahusiano yalioko baina ya serikali na wafanyabiashara juu ya mvutano wa vitu vinavyotoka nje vinakuwa si vizuri. Kwa hivyo, *spirit* inayokuwepo ya kujenga umoja na kuweza kuwapatia wananchi wetu yale ambayo yanayostahiki basi ni vizuri tukahakikisha haya yanaendelea kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wetu wanafaidika na kila kitu.

Lakini la mwisho labda kumalizia Mhe. Mwenyekiti ni suala zima la kuweza kusimamia au kuangamiza vitu ambavyo vitakuwa havistahiki kwa ajili ya matumzi ya binadamu. Hili ni jambo ambalo tuwe makini sana najua kule jimboni kwangu Kibele tayari mambo haya yanafanyika, lakini athari wakati mwengine kuna vitu ambavyo vinavyotaka kuwa *destroyed* au kuangamizwa lazima viangaliwe je, kwa kisiwa chetu hichi unapochoma au kuangamiza vitu juu ya ardhi, tuhakikishe kwamba hayazami kwenda kwenye *water table*.

Hili ni jambo ambalo nimeliongea sana hata huko miaka ya nyuma nimelizungumza katika vikao vilivyopita na ni jambo la msingi kabisa. Kwa hivyo mimi baada ya mawazo yangu haya machache niliyotoa Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nitaomba pia wajumbe wezangu wa Baraza wakati wenzetu wanachangia basi na sisi kanuni kwenda mbele. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia jioni hii kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kuweza kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sheria Nam. 2 ya 2006.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake kwa kutuletea marekebisho mbali mbali ambayo yatasaidia kuboresha mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza nianze ukurasa wa 208 marekebisho Nam. 3(d). Hapa imesema kwamba kwa kuongeza tafsiri mpya wa maneno, sasa sijui kama wa maneno au ya maneno naomba maelezo. Halafu imesema kwamba maneno haya kwa mpangilio wa kiherufi kama ifuatavyo, lakini nikiangalia huo mtiririko wa tafsiri naona hazikukaa vizuri *alphabet* imeanzia vizuri (b) lakini imekwenda (w) halafu imerudi (m). Kwa hivyo, naona huu mpangilio kama walivyosema kwamba nahisi haukukaa vizuri. Ningeomba tafsiri ziende kwa utaratibu wa *alphabet* kama vile tunavyoona kwenye miswada ya Kiingereza inakuwa tafsiri zake zinakaa sawa na zinakuwa kwa *alphabet*. Kwa hivyo, ningeomba na hapa hapa parekebishwe kama *alphabet* zikae kweli ki-*alphabet* kwa sababu si huu tu miswada mingi ya Kiingereza inakuwa iko sawa lakini ya Kiswahili inakuwa shaghala baghala, inaanza z, kwa hivyo naomba marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nakwenda katika kifungu cha 5 katika ukurasa wa 210, kifungu cha 5(2) kifungu ambacho kinasema:-

> "Mtu hatoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi isipokuwa mtu huyo awe na elimu na uzoefu usiopungua miaka 10 katika sayansi, tiba, utawala au fani nyengine yoyote inayohusika na hizo".

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi ningeomba kigezo cha elimu kiwekwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda ukurasa huo huo wa 210, Kifungu cha 5(2)(c) inasema kwamba:-

> "Kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuhakikisha ufanisi wa bidhaa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kupambana na kupiga vita usimamizi na utumiaji wa bidhaa hizo na zilizo chini ya kiwango zinazosimamiwa na sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna wakala ambaye amewekwa kwenye marekebisho haya, lakini pia kuna Shirika la Viwango *ZBS*. Sasa mimi nilikuwa nataka Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja anieleze uhusiano wa mipaka wa kisheria kati ya wakala na Shirika la Viwango la *ZBS*.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nakwenda ukurasa wa 211 kwenye uwezo na wajibu wa bodi, kifungu cha 5B kinasema:-

> "Bodi itakuwa na uwezo wa kushauri katika utendaji kazi wa Wakala na kipekee itakuwa na uwezo wa:-

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi kipekee lugha za kisheria sizijui, lakini sasa hii kipekee sijui kama ipo sahihi ama ina ulazima wa kuwekwa ama laa. Kwa hi yo, nilikuwa naomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye ukurasa huo huo wa 211, kifungu cha 5B(1)(g) kinasema kwamba:-

> "Kupendekeza uajiri wa wafanyakazi na mipango ya kuendeleza wafanyakazi iliyoandaliwa na uongozi inalingana na rasilimali za wakala ziliopo kulingana na Sheria za Utumishi wa Umma".

Sasa hapa kuna mstari wa pili nilikuwa nataka kuongeza kitu kwamba kuwaendeleza wafanyakazi inayoandaliwa na uongozi. Nataka niongeze kitu ili kuhakikisha inalingana na rasilimali za wakala zilizopo kulingana na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo wa 211, kifungu cha 6(2)(c) Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kinasema:-

> "Ana uzoefu wa kazi angalau kwa kipindi cha miaka saba. Mimi ningeomba kuongeza katika fani inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda ukurasa wa 211, hili tayari Mhe. Simai Mohammed Said tayari ameshalirekebisha la Zanzibar, hili limerekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ukurasa wa 212 kinasema kwamba:-

> "Kamati ya Wataalamu zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha 1 cha kifungu hiki zinaweza kujiwekea utaratibu wao wa kuendesha vikao".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuuliza kwamba hii kamati ya wataalamu itakuwa ni sehemu ya wafanyakazi, kama sio sehemu ya wafanyakazi nataka kusema kwamba ni vyema kamati hii vikao vyao viwe na muongozo rasmi ili viweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa sababu hapa ukiweka tu hivi kuendesha vikao vyao ina maana wanaweza wakaendesha wanavyotaka wao. Kwa hivyo, mimi ninachoomba kwamba iongezwe hivi vikao vyao viwe na muongozo rasmi ambao watawekewa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye ukurasa huo huo Mkurugenzi Mtendaji Namba 13A(1), hapa pia naomba kwamba na kiwango cha elimu kianishwe. Mhe. Mwenyekiti, nadhani mengi yameshachangiwa na wenzangu kuna *point* ambazo nimeziweka lakini nyingi zimeshachangiwa, lakini kwa kuwa nimetaka kuchangia inabidi lazima na mimi niseme.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata fursa hii na mimi nipate kuchangia kidogo, na mimi nataka kutoa maelezo kidogo kwamba Mheshimiwa sheria hii imekuja naweza kusema kwa wakati muafaka, kwa sababu nchi yetu sasa hivi vyakula vinaingia bila ya utaratibu, kwa maana nyengine vyakula vilivyokuwa havifai kwa matumizi mazuri ya binadamu vinaingia sana. Wakati mwengine watu wanatupa misaada lakini inakuwa ndio kuleta kwenye jalala, lakini ikipenya ndio imekuwa chakula cha watu.

Mhe. Mwenyekiti, maneno yamekuwa mengi sana kuhusu habari ya chakula ambacho wananchi wa Zanzibar wanakula kwamba viwango vyake sio hasa vile ambavyo vinatakiwa. Lakini pia nizungumze kwamba Mhe. Waziri leo alitufafanulia vizuri katika maelekezo yake kwamba sasa hivi chakula kinajuulikana kuanzia kinywaji, chakula chenyewe pamoja na mambo mengi

ambayo yote yanaingia kwenye chakula. Sasa mheshimiwa sasa hivi ma-*juice*, pombe na madude mengine ambayo hayafai sisi tulikuwa tunayaacha kwa sababu tunamfanya tu kwamba mnywaji pombe awe pombe tu.

Mhe. Mwenyekiti, chupa ya pombe ambyo inatimia lita moja inatoka India inakuja hapa inauzwa shilingi 5000, ambayo ukiangalia hivyo viwango viachie mbali lakini hata wewe mwenyewe ifikirie hiyo *spirit* za mambo yote yanavyonunuliwa shilingi 5000 hapa inakuja kufanya nini, lakini ujue hayo ni kutokuwa na viwango. Mheshimiwa nchi yetu imepata bahati kubwa haina ulazima wa kuwa na pombe, ikiwezekana kama hatuna pombe zenye salama basi zote zipigwe marufuku.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie kabla sijaingia kwenye karatasi hii, hii bodi ambayo itashughulikia chakula na vipodozi, mimi nataka kusema Mheshimiwa vinaweza kuwa vipodozi vizuri vinakuja kutupambia dada zetu na wanaohusika, lakini utumiaji wao baadae ukaleta madhara ukimuuliza Mkemia atakwambia kitu kipo kizuri lakini baadae kumbe kinakuja kupata matatizo. Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wanatwambia sana kwamba hata hizi dawa za nywele ndio ukakuta watu wanaojitia dawa zile akiona mvua anakwenda mbio utafikiri kafukuzwa na mamba kumbe bwana anakimbia kichwa chake. Mhe. Mwenyekiti, tojo la mvua likimtojea kwenye nywele ile akiiramba tu siku ya pili yake anatoka mapele usoni kama mgongo wa chura.

Mhe. Mwenyekiti, lazima elimu iweze kutoka kweli kweli kuelekeza madhara haya. Kwa hivyo, tunaweza tukavikuta vyakula vyetu havina tatizo, lakini matumizi yake yanakuwa mabaya. Kwa hivyo, nilikuwa naishauri hii bodi isikae kama Wizara ya Afya ikakaa hospitali kusubiri mgonjwa, Mheshimiwa hii bodi inatakiwa ikae kwenye *TV* kila wiki ilimradi iwe inatoa maelekezo yaliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza hii bodi iweze kujibu hoja, sasa hivi mitandao inasukuma kila wakati chakula hiki hakifai, soda hii haifai, kitu gani hiki hakifai pengine wanachafuliana wafanyabiashara kwa wafanyabiashara. Lakini kwa sababu anayekinga kifua hayupo na msema kweli hayupo suala lile linabakia katika maelekezo ya watu kila mmoja anavyojipanga mwenyewe. Kwa hivyo, ningeshauri sana bodi hii ikawa na *defender* ambayo ikitoka alama fulani ya maeneo, basi suala hili likaweza kujibiwa *live* watu wote wakapata habari kwamba hiyo soda iliyoingia sio ya kweli na mtu huyu achukuliwe hatua. Lakini sasa hivi tumefanya mitandao yetu kuzungumzia mambo ya chakula kwa Zanzibar kwa kuchafuliana majina pengine au kwa mtu yeyote kutaka kutukashifu tu. Sasa ningeishauri Wizara ya Afya ikaunda mtu maalum

wa habari akawa anatutolea habari kwamba kitu kilichorushwa kwenye mitandao cha chakula fulani sio cha kweli na mtu yule akatafutwa akatoa ushahidi au uongo. Lakini tunapokaa kimya chakula kile tunakifanya sio halali na tutailamu serikali siku zote kwa sababu inatuletea vyakula sivyo kumbe hatujibu mapigo. Kwa hivyo, ningeshauri sana Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Habari katika sekta hii kikafanya kazi sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kidogo kabla sijamaliza huko nianze huku ili usije ukanikatisha muda.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mswada katika kifungu cha 7 ambacho hiki kinasema kuongeza vifungu vipya vya 5A na 5, B mimi niko katika kifungu cha 5A(2) kinasema:-

> "Mtu hatoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi isipokuwa mtu huyo awe na elimu na uzoefu usiopungua miaka 10 katika sayansi ya tiba, utawala, fani nyengine yoyote inayohusiana na hizo".

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi sijafahamu mtu huyu awe na elimu na uzoefu usiopungua miaka 10, awe na elimu ya miaka 10, uzoefu wa miaka 10 hii itakuwaje? Lakini Mheshimiwa mimi nataka niseme kwamba haya mambo ya uzoefu yanahitajika, lakini Mheshimiwa umri sasa hivi hatuna mtu akitimia miaka 40 ana sukari, ana *pressure*, ana kila aina ya maradhi. Tunakuwa sasa hivi tunajiwekea vikwazo vingi kwani lazima mtu atimie miaka 100 ndio awe na akili, hakuna ulazima huo. Tumemuona mtu huyu anatufaa hata kama amefanya kazi miaka mitatu mpaka miaka minne, uongozi wake tunamuona yuko makini apewe kazi wakati anaiweza.

Lakini leo lazima tumuwekee miaka kumia amesoma mpaka amemaliza *form IV* au *form VI* ana miaka 25, anasoma tena *degree* ana miaka 35 ukija ukimpa tena uzoefu ana miaka 55 halafu ndio uje umpe Uenyekiti, mwenyekiti kila siku akiitwa anasema mgonjwa leo, sukari imepanda nini imepanda. Mheshimiwa wakati umefika tutafute vijana wapo vijana wameshatuonyesha mwelekeo chungu nzima hapa mbona hawana uzoefu wa miaka mia. *AG* huyo hapo ana miaka mia, si huyo hapo kijana mbona anafanya kazi vizuri, sasa leo mpaka utafute mtu anayekwenda kwa mkongojo ndio umpe kazi, hatuwezi Mheshimiwa huko wapunguze, mambo ya elimu haina shida kama inaongezeka twende lakini uzoefu si lazima mtu afanye kazi hizo. Mhe. Mwenyekiti, hilo ilikuwa katika kifungu (a).

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika kifungu hicho hicho cha 7, 5A(3) ambacho waziri anasema kabla hajafanya uteuzi wa wajumbe chini ya kifungu kidogo cha 1(d) ya kifungu hiki atashauriana na taasisi husika kwa ajili ya kuhakikisha wajumbe wanakuwa na taaluma inayotosheleza na uzoefu katika fani hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mbona waziri hakusema kwamba watu hawa wawe na kigezo gani, wamesema watashauriana kwa nini wasituwekee na viwango vyake kabisa. Kuna watu sasa hivi ukimwambia tu kwamba wewe tushauriane tufanye vipi haipo, kama tumeamua kufanya vigezo na hapa vigezo vifanyike mtu awe na taaluma gani na uzoefu gani na *degree* gani na hapa pia waziri akitaka kuteua awe anajua kama huyu mtu ana nafasi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea mbele nakwenda katika kifungu cha 7(4) kimasema:-

"Bodi ya ushauri itamteua Mwanasheria na wakala kuwa Katibu wa Bodi".

Hii nilikuwa naisemea hivyo hivyo hapa kiwango kiwango cha elimu hajasema wala uzoefu hajasema, atuoneshe uzoefu atuoneshe na bodi atatakiwa awe vipi huyu, maana yake na yeye ni mtu mkubwa huyu Katibu wa Bodi. Kwa hivyo, Mheshimiwa hapo nilikuwa nataka liangaliwe hilo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea niko katika kifungu nambari 8(6)(1). Katika (6)(1) kuna (6)(2), katika (6)(2)(c) Mheshimiwa inasema kwamba:-

"Ana uzoefu wa kazi angalau kwa kipindi cha miaka saba".

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio tunayoyakataa bado atupunguzie waziri hii miaka saba, kumi, kumi na saba, yeye mwenyewe mtoto keshakaa uwaziri miaka 30 pale alipo bado kijana, ingekuwa tunamsubiri miaka 40 au 50 angekuwa vile na yeye pale alipo ni kijana shababi ambaye anafanya kazi kweli kweli. Mimi namsifu lakini mbona mdogo na yeye, sasa hivi ana umri wa miaka 20 uzoefu wa uwaziri na mambo mengine mbona tumemkubali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atupunguzie miaka ili na vijana wafanye kazi isiwe wazee tu kila siku inakuwa mashaka hawapatikani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye kifungu cha 11 ambacho kina 13A, lakini hicho sasa kiko nambari ya (1) anasema:

"Uteuzi wa Mchunguzi".

Nakuja tena Mheshimiwa hapa hakutuonesha tena viwango anavyotaka vya elimu, hakutuonesha uzoefu, hakutuonesha chochote, isipokuwa nimekikuta kitu kimoja nataka ukija unifafanulie. Katika sekta hii umemtaja *engineer* humu, *engineer* anafaa? Maana yake nimemuona *engineer* humu sasa huku kuna matibabu mengi sasa na huyu *engineer* sijui kama *engineer* wa nini, atakapokuja Mheshimiwa anifafanulie. Lakini hapa nilikuwa nahitaji pia tupate uzoefu wake na kila kitu. Kwa sababu tumeshaamua kutoa uzoefu basi tufanye, laa utaamua tu kwa mtu yeyote ningeshauri hilo halina tabu Mheshimiwa.

Ninakuja katika kifungu cha 13 ambacho kimeongezwa katika sheria 15A, 15B na 15C. Mimi nakuja kwenye 15B. 15B, umemtaja mtu yoyote hatoruhusiwa kutoa kwa mtu mwengine au taasisi yoyote taarifa aliyoipata katika utekelezaji wa kazi au wajibu wake chini sheria hii, inayohusiana na kazi au jambo lolote linalomuhusu mtu yeyote au kutumia taarifa hiyo kwa manufaa binafsi au kwa faida ya muajiri wake.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nauliza kwa mtu yeyote au kwa mfanyakazi? Maana hapa nimeona kilicho *base* zaidi ni mtu mfanyakazi ndio unaemfunga. Mtu wa kawaida akipata siri ataitoa tu, lakini hapa sijui kama umemfunga mtu yeyote ambaye ni mfanyakazi au mtu yeyote ambaye anayetaka mwenyewe kusema. Hapa nilikuwa nalizungumzia hilo ili niweze kuliweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena kwenye kifungu cha 15C(1) ambacho kinazungumza kwamba:

> "Wakala itaanzisha Mfumo wa Kimataifa wa Usimamizi na Tathmini utakaohusika na kufanya mapitio na kukadiria Wakala katika utekelezaji wa kazi zake".

Hapa nilikuwa naangalia kwamba itaanzisha mfumo wa kimataifa wakati sisi wenyewe naona tuko kwenye mataifa, tunaanzisha mfumo upi ambao mwengine tunakuja kujadiliana baadae ili kuchanganya madawa. Maana yake hapa kila tukiweza kuweka mifumo mingi tunajichanganya. Mimi naona kwamba mfumo tuliouweka unatosha hakuna haja ya kuongeza mazonge mengine itakuwa kama tunajichanganya.

Mhe. Mwenyekiti, 16 katika kifungu cha 60A(2)(c):

> "Uchukuaji hatua za fidia kwa waathirika wa madhara ya dawa za uwasilishaji wa taarifa katika mfumo wa usimamizi wa kimataifa".

Hapa nataka uje ufafanue, kwa sababu hii fidia kwa huyu aliyepata madhara inatoka serikalini, hii fidia kwa yule aliyemsababishia, hii fidia kutakuwa na kitengo maalum kitakachomfikisha. Mimi sijakifahamu utakapokuja hichi naomba unifafanulie kwa manufaa ya watu wote, maana hapa kuna neno fidia tumeshalifurahia sana hili kwamba fidia tutalipwa.

Chengine pia kuna kifungu hicho hicho cha 60A kinasema...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Sarahani nakuomba umalizie dakika zako zimekwisha nakuongeza nusu dakika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa basi niunge mkono tu, nusu dakika nitasema nini? Mheshimiwa basi naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Sarahan kwa mchango wako, Waheshimiwa Wajumbe naomba niwakumbushe tena, mnapochangia mna maelezo mengi mwisho wa siku hapa kama Mhe. Suleiman Sarahan alivyoanza mwanzo, akasema dakika zake nimezibinya na sikuzibinya lakini ulianza na mambo mengi kuliko kwenye ule mswada wenyewe. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa tuchangie pale unapohisi umeweka mwenyewe mambo unayotaka kuchangia kuliko maelezo mengi yale ambayo unayatoa. Nawaomba sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kusimama hapa jioni ya leo nikiwa mzima na afya njema. Pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kupongeza huko mbele kwa tunavyong'ara akinamama. Hii inadhihirisha kwamba akinamama tunaweza bila ya kuwezeshwa, mambo yangeng'ara vizuri zaidi ingekuwa na mbeba siwa pia angekuwa mwanamke basi ingezidi kung'ara zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza Mwenyekiti na wajumbe wake wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa maoni na marekebisho ambayo wameyatoa katika mswada huu. Naamini kwamba maoni haya yameimarisha zaidi mswada huu. Lakini pia nichukue nafasi hii kabisa kupongeza Wizara yetu ya Afya kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuleta Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sheria Nam. 2 ya Mwaka 2006. Hii inamaanisha kwamba tunakwenda na wakati na nchi za Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mimi sitokuwa na mchango mkubwa nitaheshimu maneno ambayo umeyatamka, kwa hivyo, nitakwenda moja kwa moja katika mswada wenyewe. Nianzie katika ukurasa wa 210 kifungu Nam. 5A(1)(iii) inasema kwamba:-

"Wakili wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu".

Katika mambo ambayo itakapoanzishwa hii Bodi ya Wakala kutakuwa na wajumbe wafuatao:

Mmoja atakuwa ni wakili wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, hii mimi inanipa shida na namuomba Mhe. Mwanasheria kwa vile yupo nadhani atatusaidia. Ninavyofahamu mimi katika taasisi zote za serikali zinakuwa na Mwanasheria ambaye anatoka Aisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa hapa sioni haja ya kuwepo wakili wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria kwa vile mwanasheria yupo katika taasisi hiyo. Kwa hivyo, naomba basi ikiwezekana tufanye marekebisho ya kwamba Mwanasheria awe katika taasisi ile ile husika.

Jengine nikija katika ukurasa wa 211 kifungu Nam. 8(6)(1) kinasema:

"Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais"

(a) Atakuwa ni Mzanzibari. Mimi hilo sina tatizo nalo, lakini

(b) Kifungu kinasema kwamba, awe na elimu angalau Shahada ya Pili ya Chuo Kikuu kinachotambulika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani sote tunafahamu kwamba elimu ya kufanyia kazi ni Shahada ya Kwanza na sio Shahada ya Pili, lakini kifungu hiki pia kinaweza kumbana Rais kuweza kumteuwa mtu ambaye ana uweledi mzuri, ana uzoefu wa utendaji lakini akapata shida katika uteuzi wake kutokana na sifa hii ya Shahada ya Pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyvo mimi namuomba Mhe. Waziri kama tutakubaliana afanye marekebisho kwamba mtu awe na elimu angalau Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu na kuendelea lakini sio Shahada ya Pili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niingie katika ukurasa wa 216 Mwenendo wa Vikao vya Bodi ya Ushauri. Kifungu Nam. 1(4) kinasema kwamba:

"Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha dharura, baada ya kuombwa kwa maandishi na wajumbe wengi ikizingatiwa kwamba vikao vya dharura havitozidi vikao vitatu".

Sote tunafahamu kwamba sasa hivi nchi yetu baadhi ya wafanyabiashara wanaingiza bidhaa zisizo na kiwango, sasa kifungu hiki kinaonesha kwamba baada ya kuombwa kwa maandishi na wajumbe, sasa hii serikali wakati mwengine inawezekana ina jambo la dharura na muhimu au pengine kuna bidhaa imeletwa nchini bila ya serikali kujua lakini hatimaye wakatambua kwamba bidhaa ile pengine ina sumu Mwenyezi Mungu atuepushie mbali.

Sasa pana umuhimu wa kuitisha kikao hichi cha bodi. Hivyo, kauli hii inaonesha kwamba urasimu utakuwepo mzunguko mkubwa mpaka watafutwe wajumbe walio wengi wakutane, waandike barua, wakubaliane halafu ndipo kikao kifanyike. Mimi ningeomba kifungu hiki kisomeke kwamba:-

"Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha dharura pale panapotokea dharura"

Na sio kwamba mpaka atafute wajumbe wengi na waandike barua kwa maandishi ndio ikutane bodi hiyo.

Pia Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawezekana ana jambo la dharura lakini itamuwia vigumu kusema kwamba kikao hiki kikutane ili kiweze kupitisha mambo yao. Kwa hivyo, mimi naomba kama nilivyosema mwanzo isomeke kuwa Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha dharura pale panapotokea dharura na sio vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nikimalizia kuna ukurasa wa 212 kifungu cha 13A kinasema kwamba:

"Mkurugenzi Mtendaji anaweza baada ya kushauriana na bodi na kwa kutoa tangazo...".

Hii inaonesha kwamba Mkurugenzi Mtendaji atashauriana. Mheshimiwa ushauri ndio ushauri, unaposema kwamba kwa kushauriana ina maana kwamba ushauri unaweza ukapokelewa au unaweza kakataliwa. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri marekebisho yangu yasomeke kwamba, "Mkurugenzi

Mtendaji anaweza baada ya kuthibitishwa na bodi na kwa kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi".

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema mwanzo kwamba sitokua na maneno mengi nitaingia moja kwa moja katika mswada, naomba niseme kwamba naunga mkono mswada huu ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi kuweza kuchangia jioni hii ya leo mswada huu adhimu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehema aliyetujaalia tukakutana hapa jioni, kwa ajili ya kikao hiki adhimu kuujadili Mswada huu kwa ajili ya mustakabali wa wananchi wetu waliotutuma hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitu ambacho nilikuwa naomba dua kije kilikuwa ni huu mswada, mswada huu wa Chakula, Dawa na Vipodozi ni kilio cha Wazanzibari. Kwa sababu wenzangu wengi waliochangia katika mswada huu wameonesha jinsi gani wanavyoumizwa na uingizaji wa bidhaa ambazo haziko kwenye kiwango zinazoliwa na wananchi wetu wa Zanzibar, hasa upande wa chakula, dawa na vipodozi ambapo ni ukweli usiopingika kwamba ni matumizi ya siku hadi siku, yaani ni matumizi ya siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kuzungumzia kidogo kuhusu chakula. Chakula kama tunavyokijua sisi Zanzibar hapa chakula chetu kikubwa ni mchele na idadi kubwa ya mchele unaoingizwa unatoka nje. Lakini hapa kumezungumzwa suala la udhbiti wa chakula na mimi napata kigugumizi kuhusu udhibiti huo kwa sababu moja.

Kwa sababu mzigo unapoingia bandarini mathalan hawa watu waliopo bandarini wanathibitisha vipi kwamba bidhaa yote iliyoingia ni bora wakati bidhaa ile inakuja kwenye kontena na watu wetu hawafungui makontena yote wanachukua *sample* tu kidogo. Inawezekana mfanyabiashara kwa kutumia ujanja wake aka-*pack* mzigo mzuri akachanganya na mbaya. Sasa naomba kwa sheria hii iwekwe kipengele au iundwe kanuni ya kuweza kuthibitisha bidhaa zote kwa maana ya zote na bodi yenye jukumu hili iweke nembo maalum kwenye bidhaa hizo zinazokuja ili ziweze kutambulika kama zimeingia nchini kihalali na kupimwa na kuthibitishwa kama ziko salama kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hili litatupunguzia madhara kwa wananchi, wananchi wetu wengi leo wamekuwa ni wagonjwa kwa sababu ya bidhaa mbovu zinazoletwa kwa ujanja wa wafanyabiashara ambao sio waaminifu. Mimi naipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuliona hili na kulitungia sheria na hatimaye nawaomba waharakishe kutunga kanuni ambayo itakuwa ni muongozo wa sheria hii. Vyenginevyo tutakuwa tunaendelea kutunga sheria nzuri nyingi lakini utekelezaji na usimamizi hakuna, ambapo kama tutashindwa kusimamia sheria tutakuwa hatujawatendea haki wananchi wetu waliotutuma hapa leo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikirudi kidogo katika kuchangia mswada huu nilikuta katika kifungu cha 60A(1) kinachosema:-

Kifungu cha 60(A)(1)

> "Wakala itaanzisha programu ya ufuatiliaji wa madhara yanayosababishwa na dawa, ili kusimamia na kutoa taarifa kuhusu usalama wa bidhaa tiba".

Sasa kutoa taarifa ya usalama wa bidhaa tiba, bidhaa chakula je, bidhaa vipodozi je, ambazo zote zinatumika hazihitaji taarifa. Kwa hivyo, mimi naomba kutoa mapendekezo kwamba kila kinapotajwa kitu kimoja, ziende sambamba na mswada wenyewe unavyosomeka, isiwe dawa tu, iwe chakula, dawa na vipodozi itajwe kila nukta kila sehemu ambapo imetajwa iwe ni muendelezo wa sentensi, iwe ni adhabu au iwe ni chochote kitajwe kuwa chakula, dawa na vipodozi katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa kwa hii bodi ya ushauri 5(1), kidogo linanitia wasi wasi, kwa sababu inasema neno "bodi" unaanzishwa, kwa nini isitajwe. Turudi kwenye 5(A)(1). Mhe. Mwenyekiti, kidogo naona sioni. Mhe. Mwenyekiti, tuondoke kwenye hiyo 5(A)(1) turudi kwenye 60(b), marekebisho ya maneno sasa, twende kwenye mstari wa nne. Kuna neno "zilozo" naomba lifanyiwe marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, katika 60(2)(c) kuhusu uchukuaji wa fidia. Lakini fidia kama nilivyorejea kusema kwamba ni kwa ajili ya dawa tu. Kwa hivyo, mimi napendekeza tena kwamba hapa kwenye hiki kifungu cha 60(2)(c) kama alivyosema mwenzangu, uchukuaji wa fidia kwa waathirika wa madhara ya dawa na uwasilishaji wa taarifa kama mfumo wa usimamizi wa kimataifa. Mimi napendekeza narudia tena kwamba ni vyema kabisa huu uchukuaji wa fidia uwe ni kwa *item* zote kama zilivyotajwa kwenye mambo yote yaliyotajwa kwenye mswada, na ikiwezekana hizi fidia zenyewe zielezwe kutokana na madhara, kwamba madhara yakiwa kiwango hiki anastahiki hili na yakiwa hivi

yanastahiki hivi kwenye hizo kanuni, kanuni zieleze hayo. Sio tu kwamba ielezwe kuchukua fidia.

Pengine mtu kaathirika kwa kiasi ambacho ni kikubwa, leo ukenda kumpa fidia pengine shilingi 10,000 imeshakuwa tayari ni fidia. Kwa hivyo, ni bora katika utungaji wa kanuni, kanuni zieleze viwango vya kuathirika na viwango vya fidia ambazo anapaswa mtu kulipwa kutokana na madhara yaliyosababishwa na dawa, chakula au vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa leo mimi nilikuwa nataka nimalizie kwa hicho kifungu cha 60(c)(a) ambacho kinasomeka;

Kifungu cha 60(C)(a)

> "Ataamuru mtu aliyeruhusiwa kutoendelea, maana yake mwanzo inaanza pale ambapo Mkurugenzi Mtendaji atagundua kuwa bidhaa yoyote au dawa haipo katika viwango vya utambuzi, kuwa na uwezo, ubora na usafi haipo katika maelekezo yoyote yaliyoelezwa katika nyaraka za usajili, Mkurugenzi Mtendaji ataamuru mtu aliyeruhusiwa kutoendelea na uuzaji idadi iliyobaki kwa namna yoyote itakavyowekana".

Kwanza hapo kuna *error* napenda pia isahihishwe na isomeke "itakavyowezekana", badala ya itakavyowekana.

> "(b) Atasitisha kiwango cha idadi kilichouzwa, ataitisha kiwango cha idadi kilichouzwa.

Sasa hiki kiwango kilichouzwa atakiitisha vipi wakati kimeshauzwa, atakifahamu vipi. Mimi nafikiria na ninashauri watu wetu ambao watapewa dhamana hii, wawe ni makini kwa kufuatilia, wasilisubiri mpaka likaroa, wakinge kabla ya tiba. Wanasema wenyewe kinga ni bora kuliko tiba, kwa sababu kama tumeshagundua kuwa hii imeshakwisha muda wake na imeshauzwa utawezaje kuirejesha, ina maana huwezi kuirejesha itaendelea kubaki majumbani, watu wataitumia na wataendelea kupata madhara.

Kwa hivyo, mimi kutokana na uzuri wa mswada huo, kwamba umekuja kwa wakati muafaka, sipendi nitie chumvi maneno mengi yakaja yakaharibu. Lakini wito wangu kwa wizara. Maana yake katika kusoma huku nimeona wizara nyingi zimeunda hii bodi, lakini pia nilipendekeza kuwepo na *One Stop Centre* ambayo itarahisisha utendaji kazi, kwa sababu leo tumeona kama hapa. Mswada ni wa Wizara ya Afya, lakini chakula kinachoingizwa masuulia ni

watu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambapo kwa pamoja wote wanakuwepo bandarini na ndio utaratibu ulivyo. Lakini je, tujiulize kukiwa na duka la dawa *for OTC* zile Wizara ya Afya wanatoa leseni, Halmashauri pengine na wao wanatoa leseni na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wanatoa leseni, nani anakuwa mas-uli.

Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba kuwepo na *One Stop Centre* kwa mambo haya ambayo yataturahisishia kutambua makosa yoyote yanayojitokeza katika mambo haya ya kudhibiti madawa, chakula na vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya natamka rasmi kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa michango yako. Sasa namwita Mhe. Machano Othman Said, akifuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukuwe nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni hii ya leo. Aidha napenda nichukuwe pia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuweza kutoa mchango wangu katika sheria hii au mswada huu wa wakala wa chakula, dawa na vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri au kumpongeza pamoja na watendaji wake, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutekeleza jambo hili, ni matumainio yangu kwamba sheria hii itatusaidia katika kuweka mambo yetu sawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba sina tatizo na mswada huu na nianze kwa kuunga mkono mswada huu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninayo maoni yangu kidogo nataka kuyatoa katika mswada huu. Kwanza nataka kujua kupitia kwa Mhe. Waziri, wakala huu ni muhimu je, wizara yake kwa kupitia wakala huu mnao wafanyakazi wataalamu wa kutosha wa kukabiliana na changamoto za mamlaka hii. Kwa sababu tunaelewa kwamba chakula, madawa na vipodozi ni vitu vya kila siku kwa mwanadamu, lazima ule, na wagonjwa lazima wapate dawa, na watu lazima wapate vipodozi katika kujiweka sawa. Sasa kama tatakuwa na wafanyakazi wenye taaluma kidogo basi inawezekana mashaka yakawa makubwa.

Pia nataka kujua tukiwa na wakala huu je, hao wafanyakazi wataendelea kuwa makao makuu tu ya wakala au pengine kuna utaratibu na mpango wa kuwapeleka hadi wilayani kufanya ukaguzi huu. Nasema hivi kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa ukaguzi ambao unafanywa katika maduka ya madawa mjini, maduka ya vyakula mjini na maduka ya vipodozi mjini ni tofauti sana na ambao unafanyika katika maduka ya madawa katika sehemu za vijijini na sehemu ya baadhi ya Pemba, wakaguzi hawa hawaendi na wakienda taarifa zao zinakuwa zimefika, kwa hivyo vile vitu vilivyokwisha muda hawawezi kuviona.

Vile vile niwaombe sana kwamba kuna baadhi ya maduka na zaidi maduka ya madawa wanauza watu ambao hawana taaluma nayo na zaidi vijijini. Kwa hivyo, mtu anauza duka la madawa, lakini dawa yenyewe matumizi yake yeye mwenyewe haijui vizuri, hatimaye mtu anatumia dawa na anapata madhara mengine zaidi ya dawa. Je, hili likitokezea nani anastahiki kulipa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kumuuliza Mhe. Waziri anisadie nilijuwe. Yapo madai ya wenye maduka ya madawa zaidi yale makubwa, kwamba wanapoingiza mzigo mpya wa madawa, wanatakiwa walipe fedha pengine kwa ile aina ya dawa isiyopungua dola 5,000. Je, hili lina ukweli gani na kama lipo kwa nini linafanyika hivi na linasaidia nini katika kupunguza uzito wa maisha ya wananchi wa Zanzibar katika bei ya dawa. Kwa sababu wenye maduka ya madawa wakubwa wakileta dawa kama wanalipa hivyo, ina maana na yeye ataweka bei kubwa ambayo itamfanya mwananchi asiweze kumudu bei ya dawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia lipo tatizo la vyakula. Wenzangu wamelizungumzia sana vyakula ambavyo tunavipata vinakwisha muda na ni vyakula ambavyo haviko katika kiwango kizuri. Vyakula, vipodozi na dawa. Kuna kipindi ilikuwa katika mitandao ya kijamii unaoneshwa dawa ya panadol imekatwa lakini ndani ina kama vyuma vyuma, sasa sijui kama ni mtandao tu lakini hali halisi iko hivyo. Namuomba Mhe. Waziri atusaidie pia kutuelezea uhusiano au mashirikiano ya taasisi hii muhimu ya serikali na taasisi nyengine muhimu ya serikali ya *ZBS*. Yaani ile Mamlaka ya Viwango Zanzibar ambayo iko chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wana uhusiano gani na wanafanyakazi vipi katika kuwalinda watu wa Zanzibar katika madhara ya vyakula, dawa na vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, nije pia katika kifungu cha 7 katika bodi ile. Kwanza niseme kwamba wajumbe wale wa bodi ya ushauri ukiwaangalia karibu wote ni watu wa serikali, isipokuwa mmoja ambaye anatoka katika jumuiya ya

wafanyabiashara na wenye viwanda. Sijui kama siku hizi hawaiti na wakulima hilo sina uhakika nalo. Lakini mimi nashauri kwa nini kusiwe na jumuiya ya kuwalinda walaji. Kwa sababu katika taasisi nyingi au nchi nyingi watu hawa wapo, kuwe kuna taasisi ya kuwalinda walaji ambao nao mjumbe wao anaeleza kuwa ni mjumbe wa bodi ya ushauri, katika kulinda maslahi ya walaji, kwa sababu wanaoumia sana ni walaji.

Mhe. Mwenyekiti, tunasoma magazeti, tunawasikiliza watu wa Wizara ya Afya na tafiti mbali mbali zinaonesha kwamba Wazanzibari sasa ndio watu ambao wanapata maradhi makubwa. Ukienda Dar es Salaam katika hospitali ya *Ocean Road,* hata Muhimbili wateja wao wakubwa wa maradhi ya sukari, homa ya ini, maradhi ya saratani ni kutoka Zanzibar. Sasa je, hatuoni kwamba hivi vyakula, dawa na vipodozi vinasababisha maradhi haya kuongezeka? Kama inasababisha hatua gani serikali inatumia katika suala?

Lakini pia najua kwamba mswada huu wa sheria una lengo la kujiimarisha kutokana na pengine makubaliano katika Afrika ya Mashariki, na sisi Zanzibar tukiwa sehemu ya Afrika ya Mashariki. Lakini wenzetu nchi nyengine jirani wanavyo viwanda ambavyo watakapotengeneza sheria hii ya chakula dawa na vipodozi, pia watakuwa wamelenga katika kuvilinda viwanda vyao. Je, sisi Zanzibar tuna mpango wa kuvilinda viwanda vyetu, hasa hivi ambavyo vinachipukia?

Kwa mfano, sasa hivi tuna kiwanda cha maziwa kinazalisha maziwa mazuri cha Bakharesa, lakini je, tutaruhusu tena maziwa yaingie ovyo ovyo hapa Zanzibar. Lakini nimewasikia wenzangu wanazungumzia sana kwamba tunapokea juisi ambazo zimepitwa na wakati na hazina viwango. Kwa nini tusiwe na sheria kwa kupitia pengine sheria kama hii, ya kuwahamasisha na kuwalinda wananchi wa Zanzibar, ili waweze kuwa na viwanda vya ndani vya juisi za uhakika na ambazo hazina matatizo, ili ziweze kuwasaidia wananchi ili waweze kufanikiwa katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kumekuwa na utaratibu. Zamani Wizara hii ya Afya ilipiga marufuku utoaji wa matangazo kwa waganga wa jadi, matangazo mengine ya vyakula tu. Lakini sasa hivi naona kama wamepigwa chenga. Sasa hivi ukisikiliza FM nyingi usiku, yaani wamekuwa kama ni vipindi rasmi, sio kama vipindi vya matangazo, yaani kuanzia saa 3:00 mpaka saa 4:00 redio utaikuta inazungumzia dawa hii na dawa hii. Sina uhakika kama Wizara ya Afya wanajua, wanafuatilia na wamejua kama madhara hakuna katika utoaji wa habari hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kama miaka mitatu minne nyuma tulikumbana na kadhia ya chakula kibovu. Tunakumbuka uliletwa unga wa ngano mwingi sana, na ulitugharimu sana kuupeleka kwenda kuuharibu Bara. Ilikuwa ni mpira aharibu nani, aupeleke nani, afanye nani na hata huko Bara wenyewe walikuwa wanaukataa ule mzigo, kwa sababu ulikuwa ni mzigo mkubwa na ulikuwa una gharama sana, nafikiri uligharimu karibu shilingi milioni mia tatu au mia nne. Sasa mambo kama haya chakula kinakaa bandarini pale mpaka unga wa ngano unatoka maji tena yanakua ya rangi ya manjano, inakuwa ni hatari sana Mhe.Mwenyekiti, na hii mamlaka ipo. Sasa labda pengine wakati ule ilikuwa hii sheria inawabanabana, lakini sasa wamekuja kurekebisha. Lakini lazima tujuwe kwamba wananchi wa Zanzibar wanateketea na wenye dhamana ni watu wa mamlaka hii na Wizara yenyewe ya Afya ina mamlaka dhamna sana. Maana kama tutaruhusu vyakula viingie vibovu, halafu hawa watu wa Wizara ya Afya watumie fedha wanununuwe dawa wawatibu watu, inakuwa ni tatizo sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi naona sina mengi, niunge tu mkono tena mswada huu. Lakini pia nataka nije nipate maelezo kwa yale ambayo nilimuuliza Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said. Sasa nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali, na Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum ajitayarishe.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii sasa hivi na mimi kutoa maoni yangu kuhusu mswada huu ulio mbele yetu wa sheria ya chakula, dawa na vipodozi. Lakini pamoja na maelezo yake kwamba twende moja kwa moja kwenye *point*. Naomba nikueleze Mhe. Mwenyekiti, kwamba utamu wa ngoma ni lele. Kwa hivyo, lazima japo kidogo tupige lele lele kidogo ili ngoma inogee.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza serikali kwa kupitia Wizara ya Afya kwa kuona umuhimu wa jambo hili la masuala ya chakula, dawa na vipodozi kwa mswada huu kuufanyia marekebisho na kuongeza vifungu ambavyo vina umuhimu kwa maslahi ya wananchi wetu. Kwa hivyo, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia mswada huu kwa kusema kwamba Bodi hii ya Ushauri tunayoianzisha sasa hivi ni sawa na mdomo, ambapo mdomo ukiruhusu chakula kiingie tumboni kwa hivyo ama tumbo litaathirika au litapata manufaa zaidi kama hautaruhusu kuingia chakula mdomoni, kwa hivyo

bodi hii ndio itakayosema kwamba chakula hichi kinafaa hichi hakifai, kwa hivyo kikiwa makini kitaweza kufanya kazi na sisi kutunusuru.

Kwa hivyo naomba sana iwe ni bodi ambayo kuwa imeridhika isiyokuwa na tamaa ni lazima wajumbe wote wawe ni wenye kuridhika na wasiwe na tamaa kabisa ndio wataweza kufanya kazi shughuli zao vizuri. Kwa hivyo pia niipongeze kamati ambayo iliipokea mswada huu na ikakalia vyema na ikaitambua kifungu kwa kifungu na hatimae ikatuletea mbele yetu hapa leo tunashirikiana katika kuiboresha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika marekebisho ya Mswada huu kifungu Namaba 9 kinachosema kwamba kunaanzishwa Idara ya wakala kama ifuatavyo, hizi idara kifungu cha 7(i) ilichoanzisha idara hizi tatu Idara ya udhibiti wa Chakula, Idara ya dawa na vipodozi na aina nyengine za bidhaa za dawa, Idara za huduma za maabara na huduma za huduma za wakala. Katika idara hizi kwa kweli ni muhimu sana, lakini hii idara ya dawa naiomba sana ifanye kazi kubwa ya kuzikagua hizi dawa zile zinazoongezeka huku mitaani za tiba asili, kwani tumekuwa tukiona kila mmoja anasifu dawa yake na hujui dawa hii imetengenezwa wapi, kwenye kiwanda gani hicho kiwanda kina leseni kimekaguliwa au na hiyo dawa imekaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia bodi hii ifanye kazi kubwa ya kuzichunguza hizi dawa watu wanazouziwa mitaani kwani zimekuwa zimezagaa sana. Lakini pia vile vile katika idara hizi ilioko katika kifungu Namba 7(c) Idara ya huduma za maabara, hii huduma za maabara nayo ni idara muhimu sana, kwa sababu ili itambulikane chakula hichi kina madhara lazima ipitie maabara naomba sana Serikali iwezeshe kuwepo kwa maabara hii na iweze kufanya kazi mia juu ya mia ndio hiyo kazi ya kutoa taarifa itawezekana badala ya kukisia.

Lakini ni vyema pia niendelee katika kifungu namba 11 ambapo kifungu hiki kimefanywa kuwa upya pale kipo kifungu namba 13A(1):

> "Naomba kupata mchunguzi kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii ya Chakula na Vipodozi".

Nnapendekeza kwamba huyu mchunguzi atakayekuwepo kwa sababu ndie atakayetoa ripoti kuisaidia bodi hii ya Ushauri kwamba ale kiapo cha utii, huyu mchunguzi tunayetaka kumuajiri hapa kuwa nae lazima napendekeza sana aweze kula kiapo cha utii, kazi atakayoifanya ni muhimu na ya hatari kama ataifanya kinyume nyume.

Lakini pia vile vile kifungu 13A(2):

> "Mchunguzi hatokuwa na maslahi katika bidhaa inayohifadhiwa au kuingizwa".

Je ni mbinu gani tutakazohakikisha kwamba huyu mchunguzi ambae kuwa tunae hana maslahi, naomba hili tuangalie ni vigezo gani tutakavyovitumia kuona kwamba huyu mchunguzi ambaekuwa tunae hana maslahi na mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika kuchangia kifungu No. 16 cha Mswada huu wa sheria pale ambapo kuwa kimeongeza vifungu sita vifungu vya 60 A mpaka C hivi vifungu kweli ni muhimu sana lakini visimamiwe bila ya muhali, visimamiwe vifungu hivi vilivyoongezwa hapa 60A, B na C bila ya muhali ndio tutaweza kufanya kazi na kuleta manufaa yaliyokuzudiwa. Kulikuwa na marekebisho ya maneno hayo hapa kifungu 60B na C lakini mwenzangu alitangulia ameshayaona sina haja ya kuyarejea.

Sasa niende moja kwa moja kifungu 18 pale kinaposema kwamba kimerekebisha na kuanzisha kifungu kipya 73A kutoa taarifa ya madhara ya dawa hatari, naomba Waziri anieleze dawa hizi zilizoamua kwamba kituo cha afya cha Serikali au cha watu binafsi ndio kitakachotoa taarifa. Sasa hii bodi si ilikagua hizi dawa kama dawa zilikaguliwa na bodi sasa inakuwaje mpaka ende akatoe kituo cha Serikali au cha mtu binafsi kwamba hizi dawa ni hatari. Naomba hapa kidogo atuwekee wazi ili tuweze kuelewa kwa sababu hivi tayari vimeshachunguzwa kwa hivyo naona wao ndio itakuwa masuula zaidi hii bodi iliyochunguza madawa haya kuingia nchini.

Mwisho, karibu ya yote ni bodi hii katika utendaji wa kazi zake itakabiliwa na changamoto ambazo kwamba kuna bidhaa zitakazoingia bila ya kuzikagua kwa kupitia bandari bubu au njia zisizo rasmi. Kwa hivyo niombe Serikali kwa mashirikiano makubwa ya vyombo vyetu hivi vilioko katika shehia zetu kuwatumia masheha, pamoja na wananchi ili waweze kutoa taarifa pale ambapo kuwa kumeanzisha bandari bubu wao watakuwa wanazijua waondoe muhali. Kwa sababu huu muhali utaweza kutuathiri tukiruhusu mambo haya kuingia bila ya kukaguliwa. Lakini na wananchi pia vile vile nao washiriki katika kufichua mambo haya bandari ambazo kuwa ni bubu hazitambuliki hazina ukaguzi.

Lakini pia vile vile kwa wale wananchi ambao kuwa watatoa taarifa hizi napendekeza wawekewe motisha, kwanza walindwe na watoe motisha kwa sababu wakibainika kwamba fulani alikwenda kusema kuna bandari bubu au kuna mfanya biashara ameingiza bidhaa hizi bila ya kukaguliwa anaweza kuhatarisha maisha yake. Kwa hivyo alindwe lakini pia ipatikane kupewa motisha.

Mwisho naomba sana pamoja na kupitisha sheria hii Mhe. Waziri, aandae kanuni za kuweza kutekeleza sheria hii kwa haraka iwezekanavyo, kwa sababu sheria nyengine tunasikia zinaundwa hapa na zilizopita lakini zinakosa kanuni kwa hivyo zinakosa kufanyiwa kazi kwa sababu ya kanuni hakuna.

Mwisho naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu ulio mbele yetu wa Chakula, Dawa na Vipodozi, baada ya shukurani hizo pindi ya kuwa kanuni 152 inakataza kabisa kwa Mjumbe kutoa shukurani lakini ningekuomba ukanipa ruhusa ya kushukuru kidogo wananchi wangu wa Ndagoni kwa uchaguzi kwa kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi kumchagua tena kwa nafasi ya Udiwani Ndugu Arafa Kassim Abasi.

Lakini pia vile vile nimshukuru Mhe. Jecha Salim Jecha Mwenyekiti wa tume ya Uchaguzi wa kushiriki nae kikamilifu kuhakikisha kwamba uchaguzi ule umekwenda salama na kutembelea vituo vyote vya wadi ile ya Ndagoni, nasema kwamba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe nguvu zaidi na abakie kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi mpaka 2025.

Mhe. Mwenyekiti baada ya shukurani hizo sasa niende kwenye suala la mswada, hapa Zanzibar tunaona kila biashara Made in China hata ule uji Made in China, siku nyengine biashara zinatengenezwa humo vijijini lakini wanasema Made in China. Kwa hivyo mimi nataka niulize hapa hawa watu wenye mamlaka hii wanaohusika masuala haya huwa wako wapi maana siku nyingine unakuta mpaka yale maji yanayotiwa kwenye vikopo utaambiwa Made in China.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Khamis Bakari, alizungumzia hapa kuhusu suala la madawa mule madukani ambamo ni vijijini ni kweli na mimi naungana nae kwamba baadhi ya maduka utakuta dawa za *Panadol* na nyengine wale wanaouza hata ule uelewa wa kuuza zile dawa jinsi ya kutumia hawana, sasa sijui utaratibu huu uko je.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye masuala ya uingizaji wa vyakula bandari bubu Zanzibar zimekuwa tena ni adha kusema la ukweli, lakini bandari hizi zipo na ni kweli zinaingiza vyakula kutoka sehemu mbali mbali na kuingia katika nchi yetu, lakini vile vile niiombe Wizara hii ya Afya kuweza kushirikiana zaidi na Wizara ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ili kuhakikisha kwamba vitendo hivi vya uingizaji wa vyakula kupitia njia za bandari bubu wanalikomesha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 73A kutotoa taarifa ya madhara ya dawa hatari. Mhe. Mwenyekiti, hapa inasema kituo cha afya cha Serikali na cha binafsi kitatoa taarifa kwa wakala kuhusu madhara ya dawa hatari. Kwenye kituo cha Serikali nakubaliana nayo lakini hivi vituo vya binafsi nina mushkeli kidogo, kwa sababu yeye mfanyabiashara yule zaidi hutizama mfuko wake tu hana habari ya yule aliyekwenda kununua kwamba ni mteja wake na kwamba ni mwananchi apate maisha hapa niwaombe kidogo wawe makini zaidi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 93A mtu anayehodhi alama ya dawa ambayo inadhaniwa kuwa sio halali atakuwa ametenda kosa la jinai, lakini hapa ndipo hapo niliposema kwamba mambo mengi na biashara nyingi ni Made in China hapa mimi mwenyewe nathibitisha kwamba baadhi ya dawa nyengine hususan zile za kienyeji zile za kienyeji za mafuta na mambo mengine huwa wanahodhi ile alama wakachukua alama ya mtu mwengine wakaweka pale. Kwa hivyo na hapa niiombe Wizara iwe na uangalifu sana na kuhakikisha kwamba hawa watakaokamatwa basi wachukuliwe hatua zaidi tena za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi isipokuwa naunga mkono hoja asilimia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii leo ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria Chakula, Madawa na Vipodozi wa Namba 2 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza ningependa nianze na madhumuni ya Mswada huu, madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Dawa Chakula na Vipodozi Namba 2 ya Mwaka 2006, marekebisho haya yanafanywa kutekeleza mapendekezo ya Sheria ya usimamizi wa bidhaa tiba ya umoja wa Afrika pamoja na mapendekezo ya Baraza la kisekta la Sheria na masuala ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa hili

ningependa niipongeze Serikali, naipongeza Serikali kwamba nimeona umuhimu kwa kuwa Serikali yetu ni sehemu ya Afrika ya Mashariki kwa hivyo imeona umuhimu wa suala hili kulifanyia kazi na matokeo yake ndio maana tumeweza kupata mswada huu leo hii tunauchangia.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kutekeleza mapendekezo haya yatatufanya sasa tuweze kuwa na chombo ambacho tulikuwa tunakihitaji kwa muda mrefu ili sasa kuhakikisha kwamba bidhaa zote zilizotajwa na Sheria hii kweli zinafanyiwa ukaguzi unaostahiki, na sio tu tusubiri bodi kwa ajili ya kupitia katika sehemu zile. Kwa hivyo kuwa na wakala baada ya bodi inaonekana kwamba hili ni jambo ambalo tumekwenda kwenye hatua kubwa zaidi, kwa hivyo Serikali itakuwa imefanya jambo la maana kuhusu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye kifungu Namba 4 cha Mswada huu kinazungumzia marekebisho ya kuanzishwa kwa wakala, wakala huu unlioanzishwa itakuwa ni vizuri ikiwa utafanya kazi na baadhi ya vyombo ambavyo viko chini ya Wizara hii hii ili kuweza kufanikisha. Kwa sababu baadhi ya bodi hizo au Mabaraza yaliyoko katika Wizara hii kuna bodi ya Chakula na Vipodozi, kuna Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala na wakala wenyewe ikiwa utafanya kazi kwa pamoja, pamoja na Baraza hili na Bodi hii nafikiri itakuwa jambo la maana na ni bora kukawa na ushirikiano kwa sababu wote wana lengo moja lililokusudiwa kuhakikisha kwamba afya za Wazanzibari zinalindwa. Kwa hivyo mimi ningependelea zaidi kama hawa watachukua jukumu hilo hizi sehemu tatu zikafanya kazi kwa pamoja ili kuweza kuleta mafanikio katika hii kazi ambayo tumetegemea kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningependa niende kwenye kifungu Namba 17 cha Sheria hii kuongeza kifungu kipya ambacho ni kuangamiza bidhaa za tiba, wakati tunatajiwa watu watakaoshiriki au watu watakaochaguliwa kutoka katika sehemu tofauti walitaja Mwakilishi kutoka Mazingira, huwa kuna malalamiko ya watu wa Mazingira kwamba watu wa bodi wanapokuwa wanataka kuangamiza huwa hawashirikishwi kikamilifu isipokuwa huwapa taarifa pale ambapo wanatakiwa kufanya lile jambo. Mimi nafikiri kufanya hivi haikuwa sahihi kwa sababu suala la Mazingira lina eneo lake maalum sio tu ni suala labda la kuwapa taarifa, kwa kuwa wale ndio wahusika wakuu, ni suala la kuwashirikisha likawapa nafasi yao kwa sababu pindipo chochote kibaya kikitokea na kuharibu mazingira itakuwa sasa lawama iko kwao kwa sababu wamefanya kazi ambayo haiwahusu.

Wao wanaweza wakasema kwamba hichi kinahitajika kuangamizwa kwa hivyo watu wa mazingira washirikishwe kikamilifu katika shughuli hiyo na sio

kuwaita tu kuja kushuhudia au kuwapa taarifa, nafikiri kufanya hivyo sio asahihi. Kwa hivyo matumaini yangu ni kwamba Wakala mtalifanyia kazi jambo hilo na waweze kushirikiana na wenzao vizuri ili tuweze kuleta manufaa kwa kile ambacho tunakikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kamati yetu ya Ustawi wa Jamii, kwa hili kwa kweli wamelitendea haki na wamefanya vizuri, kwa hivyo nimeona sitofanya vyema kama kamati hii sikuipongeza kwa udhati wa kazi waliyoifanya, hongereni sana watu wa kamati hii kwa Mswada huu. Kwa hivyo baada ya kusema hayo machache mimi nafikiri niunge mkono hoja kama vile ambavyo wengine walivyofanya na nafikiri hakuna mengi kwa sababu yote yamekwisha, kwa hivyo niunge mkono hoja hii. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache juu ya Mswada huu wa Sheria uliopo hapa Barazani, mimi ningependa kuchangia kwanza katika kifungu hichi cha 5A kinachozungumzia kuhusu Wajumbe wa Bodi hii ya Ushauri, unapoangalia wajumbe wenyewe kwamba nadhani wapo kama wanane. Kuna Mwenyekiti wa Bodi, kuna Mkurugenzi Mtendaji, kuna Mfamasia Mkuu, kuna Wajumbe wangine wanaoteuliwa na Mhe. Waziri kama wanne. Sasa unapokwenda ndani zaidi juu ya Wajumbe hawa utaona kama kwamba una Wajumbe wenye uwakilishi wa aina mbili.

- Kuna Wajumbe ambao wanawakilisha utaalamu na hawa wanatoka katika sekta ya Afya.

- Kuna wajumbe wanawakilisha wazalishaji kama vile wenye viwanda, Wizara ya Biashara, Wizara nyenginezo mbali mbali ambazo zimetajwa hapa,

- Kuna sehemu ya tatu ambapo mjumbe mmoja aliwahi kuchangia na mimi nataka kusisitiza ni hii sehemu ya (*consumer)* watumiaji, hawa tumewasahau kabisa kabisa na kwa kweli wao ndio wahusika wakuu katika sheria hii ambayo tunaipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kama idadi hii tunahisi kwamba imewekwa na sheria na hatuwezi kuibadilisha labda kulikuwa na sheria nyengine, lakini kama ni hivyo basi miongoni mwa wajumbe hawa wengine wanaoteuliwa na Waziri, basi ingefaa zaidi mmoja wapo akatoka katika *consumers* ama wanawezekana katika jumuia au njia nyengine yeyote. Lakini kwa kweli ni watu muhimu sana juu ya masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema hivyo kwa sababu chombo hichi ni chombo cha maamuzi, sasa anayeamuliwa mambo yake na akawa hajashirikishwa kidogo itakuwa tumemuweka pembeni. Nadhani Mhe. Waziri ataweza kuiona ile mantiki kwamba suala hili linahusu pande nyengine zaidi ambayo itakuwa tumesahau kuingizwa katika Bodi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulisema ni nyongeza ya hili hili, mara nyingi tunadhani kwamba suala la utungaji wa sheria tunalifanya *technical* sana na kwa maana hiyo inaathiri hata katika uteuzi wa Bodi zetu, kumbe utungaji wa sheria ni kweli una *technical* zake lakini pia ina *social aspect* yake lakini pia kuna *legal aspect* yake hiyo hiyo, halafu pia iko *economic aspect*. Kwa hivyo hii sehemu ya *society* ni muhimu sana kuzingatiwa kwa kweli na hii huzingatiwa katika sehemu zote za utungaji wa sheria. Nadhani tunajua lakini inapofika wakati wa utungaji tunasahau. Kwa sababu utungaji wa sheria *process* yenyewe inatwambia katika hatua fulani tuwashirikishe hawa wananchi na sisi wawakilishi tunaambiwa kabla hatujaja katika Baraza kuchangia tuwaeleze wananchi wetu kama kuna sheria hii na hii tupate maoni yao. Lakini pia na ikishapita tuna wajibu. Kwa hivyo hapa nawakumbusha Wawakilishi wenzangu kwamba itakapopita sheria hii pia tunawajibu wa kuwaelimisha wananchi juu ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala hili la Idara. Kuna idara ambazo zimeshatajwa katika sheria, lakini pia kuna kifungu kinatoa uwezo wa Bodi kuanzisha idara nyengine pale inapoonekana inafaa. Sasa nataka nisisitize katika nukta hii kwamba ni vyema Idara zikaundwa kwa mujibu wa madhumuni na malengo. Hili ni muhimu sana tusijeanzisha tu Idara kiholela, lakini lazima tuwe na misingi ya kuianzisha Idara hiyo kwa kuzingatia haja, kwa kuzingatia *performance*, kwa kuzingatia malengo hivi viwe ni vigezo muhimu sana katika kuunda idara hizi. Idara hizi ni lazima zipangiwe kazi zake *right from the beginning* ijue hasa tunaiunda idara fulani kazi zake na hizi na tujiridhishe kama kweli hizi ni kazi za kuundiwa idara au ni kazi za kuwa *section* ni jambo muhimu sana. Wakati mwengine tunaipa idara kazi lakini ukitizama pengine kazi ile ingeweza kufanywa na ki- *section* au ki-*unit*, kwa hivyo ni lazima jambo hili tulisikilize sana katika kuunda Idara.

Mhe. Mwenyekiti, ningetamani kwamba idara ambazo tutaziunda katika Wakala huu basi iwe ni idara bora na iwe ni mfano kwa idara nyengine, natamani iwe hivyo kwa kweli. Kwa sababu tunaamini kwamba wataweza kufanyakazi kwa viwango. Bodi hii kimsingi ni ya Viwango kwa hivyo na utekelezaji wa kazi zake uwe wa viwango vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ambayo ningependa kuichangia ni kwamba ili kuweza kuitekeleza vyema sheria hii, lakini pia na wakala wenyewe kuweza kufanya kazi ipasavyo, elimu ya muamko wa sheria inahitajika katika jamii yetu. Lazima watu wetu waelewe, wale niliowataja, *consumers* waelewe kwa mapana na marefu, Wizara, *producers*, *suppliers* wote waelewe kwa mapana na marefu, hapo ndivyo tutakuwa na uhakika kwamba sheria hii itatekelezwa vilivyo. Kwa utaratibu tuliouzoea wa kupitisha sheria halafu tutakaa kimpya lengo letu lile la kujenga afya litakuwa gumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi mimeitafsri sheria hii katika ujumla wake ni kulinda afya zetu wananchi kwa hivyo litachelewa kufika. Lazima mara kwa mara tuhimizane, tukumbushane juu ya uweledi wa sheria. Hii ningetamani pia Mwenyekiti, kwamba ipo haja sio kwa Wizara ya Afya lakini katika ujumla wake, hebu tufanye utafiti tutizame kiwango cha *literacy* katika sheria hapa Zanzibar. Katika elimu tunafanya *literacy* ya wanaujua wanaojua kusoma na kuandika lakini ningetamani pia hebu tutizame kiasi gani, na hiyo itatusaidia kuweza kujenga misingi imara na mikakati imara ya kutoa hii elimu ya sheria. Tunaposema elimu ya sheria hapa hatuna maana taaluma yaani *certificate*, *diploma*, *degree*, hapana ila watu wawe na (a), (b), (c), ya kujua yale mambo yapo vipi na athari yake. Nadhani ipo haja ya kuangalia hilo *literacy* katika sehemu hii ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ambayo ni muhimu ninayotaka kumalizia ni kwamba Wakala ambayo tutaianzisha ni muhimu sana kupewa *resources* zinazohitajika katika kuifanya kazi hii. Tunaweza kuianzisha tukateuwa *body of directors* na idara ikaanzishwa lakini kama *resource* ni chache kwa kweli itakuwa ni vigumu kuweza kutekeleza. Kwa hivyo muundo wa idara, muundo wa *body* na mambo mengine yote kama haijafanya kazi basi itakuwa haina maana. Kwa hivyo matarajio yetu ni kwamba Wizara ya Afya baada ya sheria hii kupita Bodi hii itawezeshwa kupatiwa *resources* zinazohitajika ili kuweza kufanya kazi ipasavyo na lile lengo letu tulilolikusudia la kulinda afya zetu liweze kufanikiwa.

Baada ya kusema hayo niseme kwamba nashukuru sana kabisa kabisa Wizara ya Afya, kwa kuleta Mswada huo ambao kwa kweli tulikuwa tunauhitajia kutokana na umhimu wake na mimi naunga mkono kwa ukamiliku Mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kwa mchango wako, wachangiaji wamemalizika, naomba nimwite Mhe. Waziri Afisi wa Makamo wa Pili wa Rais atoe kanuni ya kutengua muda ili tuwape nafasi

Waziri wa Afya na Naibu na Watendaji wake kesho waje kufanya majumuisho ya hoja za wajumbe zilizotolewa.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri Afisi wa Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kwa mujibu wa *Order Paper* ya leo shughuli zetu zimekamilika na kwa kuwa Mhe. Waziri ameomba muda ili aweze kujitayarisha kwa ajili ya kufanya majumuisho, naliomba Baraza lako tukufu liahirishe kabla ya muda wake mpaka kesho asubuhi tarehe 21 saa 3:00 za asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwapongeze wachangiaji wote waliochangia Mswada huu pamoja na wale waliochangia kwa maandishi kwa hivyo naomba niahirishe mpaka kesho saa 3:00 asubuhi tukijaaliwa ili tuwape nafasi Waziri na Watendaji wake wote waje watupe majumuisho. Ahsanteni sana na nawatakila kila kheri, safari njema.

(Saa 1:06 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 21/2/2017 saa 3:00 asubuhi)